# Nipashe

Ijumaa Februari 1, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579830

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter … shetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Nyoka wa ajabu aua watano Sumbawanga

UKURASA 2



Ukurasa 19
Siku Waziri Mgalu alipowasha taa ya historia kijijini

Ukurasa 14
Hifadhi Ruaha katika staili mpya, utalii kutoka angani kwenye puto

BUFE

Ijumaa Februari 1, 2019
Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Boti iliyotengenezwa kwa mabaki ya plastiki kufanya safari ya kihistoria

PRISCA
Muuguzi mtarajiwa aliyejikuta anaangukia kuomba mitaani

Na Elizabeth Zaya

INAENDELEA UK.16

UCHUMI
Habari katika picha

Ukurasa 17

UKURASA 13

# Msuguano mkali Ndugai, Chadema

• **Ni** baada ya bosi huyo kudai Bunge limelipa mil. 250/- kumtibu Lissu... *Endelea ukurasa wa 2*



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akishiriki katika sala ya jeneza wakati wa mazishi ya Hidaya Omar, Mke wa Mufti wa Tanzania, Abubakary Zubeir (kushoto kwa Waziri Mkuu), yaliyofanyika kijiji cha Kwamdolwa wilayani Korogwe mkoani Tanga, jana. Wengine ni Sheikh Mohammed Kigoda (wa pili kushoto) aliyeongoza sala hiyo na Sheikh wa Mkoa wa Dar es Salaam, Alhad Mussa Salum. Habari Uk. 5. **PICHA: OWM**

## YALIYOMO


UKURASA WA 3

**WAPIGAKURA WAPYA MIL. 4 KUANDIKISHWA**

SERIKALI imesema itaanza mchakato wa uboreshaji wa daftari la kudumu wapigakura hivi karibuni kwa kuandikisha...

UKURASA WA 4

**KESI YA KINA MBOWE YAPATA HAKIMU MPYA**

KESI inayomkabili Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe, na...


## Masharti magumu kuzipata dola, euro

UKURASA 2

## Zitto matatani kisa Tril. 1.5/-



UKURASA. 3


**MICHEZO** MAZOEZI SIMBA YAPAMBA MOTO UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Mvutano mkali Spika, Chadema

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

WAKATI Tundu Lissu akidai hajapewa fedha za matibabu yake na Bunge, Spika Job Ndugai, amesema Mbunge huyo wa Singida Mashariki (Chadema) ameshakabidhiwa Sh. milioni 250.

Hata hivyo, kauli hiyo ya Spika Ndugai imepingwa na uongozi wa Chadema ambao umedai fedha zilizokabidhiwa kwa Lissu kutoka Ofisi ya Bunge ni mishahara na posho zake za kibunge.

Katika kikao cha jana cha Bunge jijini Dodoma, Spika Ndugai alitoa taarifa kuhusu kiasi cha fedha ambacho kimetolewa mpaka sasa na Bunge kwa ajili ya kugharamia matibabu ya mbunge huyo.

Kwa zaidi ya mwaka sasa, Lissu amekuwa katika matibabu ya kibingwa Ubelgiji kutokana na kushambuliwa kwa kupigwa risasi na watu wasiojulikana akiwa ndani ya gari, nje ya makazi yake eneo la Area D jijini Dodoma Septemba 7, 2017.

Kabla ya kuanza kutoa ufafanuzi huo, Spika Ndugai alisema jambo ambalo anataka kulisema na alikuwa anakataa kulisemea tangu mwanzo, linamhusu Lissu na kwamba sasa ofisi yake imejipanga kuanza kumjibu.

"Tangu mwanzo, kwa sababu tulikuwa tunaamini kuwa bado yupo kitandani na haipendezi watu wazima kubishana na mgonjwa, lakini moja ya madai yake makubwa ni kuwa Bunge hili halijawahi kumpa wala kumjali kifedha tangu apate matatizo Septemba 7, 2017.

"Bado tunaendelea kumpa pole maana jambo hili ameendelea kulisema sana na haipendezi na bado anaendelea kulisemea na tutaendelea kutoa ufafanuzi kadri siku zinavyoenda.

"Lakini, itoshe tu kusema kwa Watanzania kwamba Bunge hili kupitia ofisi yangu, toka Septemba 7, 2017 hadi Desemba bila kujumuisha za Januari, kupitia ofisi yangu tumeshamlipa Lissu malipo mbalimbali ya jumla ya Sh. milioni 207.872," Spika Ndugai alisema.

Kiongozi huyo wa Bunge alisema ukijumlisha na michango ya wabunge waliyotoa kwa ajili ya matibabu iliyolipwa katika Hospitali ya Nairobi, Kenya alikokuwa amelazwa (Sh. milioni 43), Lissu amepatiwa Sh. milioni 250 na Ofisi ya Bunge.

"Unapoendelea kusema kila mahali kwamba, Bunge hili halijawahi kutoa hata senti moja kwa ajili yake, katika jambo hili ni jambo la uongo, uongo, uongo kabisa," alisema.

**CHADEMA WAJIBU**

Wakati Spika Ndugai akiyasema hayo, uongozi wa Chadema umekanusha taarifa yake na kusisitiza kuwa Lissu hajapatiwa hata senti moja kutoka kwa uongozi wa Bunge kwa ajili ya matibabu, mbali na michango ya wabunge.

Taarifa kwa vyombo vya habari iliyotolewa jana jioni na Hemedi Ali, Mkuu wa Idara ya Uenezi, Chadema Makao Makuu, ilidai kuwa Lissu ametibiwa na Chadema, mwanachama mmoja mmoja na mashirika mbalimbali ya ndani na nje ya nchi.

Taarifa hiyo pia ilidai kuwa matibabu ya Lissu yamegharamiwa na Watanzania waishio ndani na nje ya nchi na wabunge mmoja mmoja walichanga Sh. milioni 43 kutoka katika posho zao kama walivyofanya Watanzania wengine.

"Lissu ni mbunge halali wa Bunge la Tanzania na kwa mujibu wa Sheria ya Bunge, anastahili kulipwa mshahara wake wa kibunge na posho mbalimbali na pia kutibiwa na Bunge," ilielezwa katika taarifa hiyo.

"Takribani Sh. milioni 207 alizopatiwa Lissu ni stahiki zake halali za kibunge na si pesa ya matibabu kama ilivyoelezwa na Spika. Spika amedai kuwa anazo nyaraka za uthibitisho wa malipo ya matibabu, tunamtaka atoe hizo nyaraka hadharani na si kutishia."



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe, akisalimiana na aliyekuwa Mbunge wa Singida Kaskazini, Lazaro Nyalandu, kabla ya kusikilizwa kwa kesi yao katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Nyoka wa ajabu aua watano Sumbawanga

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

MAOFISA Maliasili wa Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga mkoani Rukwa, wameamua kushirikiana na mtaalamu wa tiba za jadi wa kijiji cha Kinambo, Tarafa ya Milepa, kumsaka nyoka wa ajabu anayedaiwa kuua watu watano kwa nyakati tofauti kijijini hapo.

Diwani wa Kata ya Milepa wilayani Sumbawanga, Aporinali Macheta, alisema jana kwamba, nyoka huyo aina ya koboko anadaiwa kugonga na kusababisha vifo vya watu watano katika kipindi cha miaka minne tofauti.

Alisema jambo la kushangaza ni kwamba nyoka huyo amekuwa na kawaida ya kugonga watu kila mwaka katika moja ya siku ya Jumapili.

Alisema siku kama hiyo ya Jumapili mwaka 2016 nyoka huyo aliwagonga watu wawili ambao walifariki dunia muda mfupi baadaye.

Alisema kuwa msako dhidi ya nyoka huyo umeanza baada ya juzi kumgonga na kumsababishia kifo Ndoti (60), mkazi wa Kijiji cha Kinambo, ambaye alifariki muda mfupi baada ya kugongwa na nyoka huyo.

Alisema nyoka huyo anapatikana katika mti mmoja wa mwembe ambapo baada ya kumgonga mtu hutokomea porini.

Macheta aliongeza kuwa baada ya tukio hilo wanakijiji walimwandikia barua Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo kuomba wataalamu wa Maliasili ambao walifika kijijini hapo jana.

Alisema walifika na kuanza kuendesha msako dhidi ya nyoka huyo kwa kumtumia kijana aitwaye Seif Sikanda, ambaye ni mtaalamu wa tiba za asili.

"Msako wa nyoka huyo unaendelea, lakini leo (jana) tulifanikiwa kumuua kwa risasi nyoka mdogo mwenye urefu wa futi saba aina ya koboko... tunaendelea kumsaka yule mkubwa ambaye ndio tishio la maisha ya wananchi wa kijiji hiki," alisema.

Ofisa Mtendaji wa kijiji hiko, Richard Sungura, alisema pamoja na nyoka huyo kumgonga na kusababisha kifo cha Ndoti, pia amesababisha vifo vya Elezina Kasele (68), Saise Shigela (21), John Mboganzuri (63) na Benedicto Kasele (14).

Alisema nyoka huyo pamoja na kuua watu hao kwa nyakati fofauti, pia amekuwa aking'ata mifugo kama ng'ombe, mbuzi na mbwa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Rukwa, George Kyando, alithibitisha kuwapo kwa taarifa hiyo, lakini alisema kwamba hajapata taarifa rasmi kuhusu nyoka huyo.

# Masharti magumu kuzipata dola, euro

**Na Salome Kitomari**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT), imesema kuanzia sasa huduma za kubadilishia fedha za kigeni zitapatikana katika benki na taasisi za fedha zinazoendesha biashara nchi nzima.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na BoT, benki na taasisi za fedha zinatakiwa kutoa huduma hiyo kwa wateja wote.

"Benki Kuu imehimiza benki na taasisi za fedha kuendelea kutoa huduma za kubadilisha fedha za kigeni kwa wateja wote, wakati uchunguzi wa maduka ya kubadilisha fedha za kigeni na maduka bubu unaendelea," ilisema taarifa hiyo.

Taarifa hiyo ilisema kuwa wananchi watakaopata usumbufu wowote watoe taarifa BoT kwa ajili ya kupatiwa ufumbuzi.

"Benki Kuu pia inapenda kuutahadharisha umma kutotumia huduma zisizo rasmi za ubadilishaji wa fedha za kigeni kutokana na hatari mbalimbali zinazotokana na huduma hizo ikiwamo kuibiwa au kupewa fedha bandia," taarifa hiyo ilieleza zaidi bila kueleza kuhusu hatima ya maduka ya kubadilishia fedha.

Aidha, taarifa hiyo ilisema utumiaji wa huduma zisizo rasmi ni kinyume cha sheria za nchi na kwamba hatua kali zitachukuliwa dhidi ya watoaji na watumiaji wa huduma hizo (black-market).

Novemba mwaka 2018, BoT iliratibu operesheni maalum ya maduka ya kubadilisha fedha za kigeni na baadhi ya maduka bubu ambayo hayana leseni, lakini yalikuwa yakiendesha biashara hiyo kinyume cha sheria katika Jiji la Arusha.

Kutokana na operesheni hiyo, maduka hayo yalifungwa kwa muda kupisha uchunguzi unaoendelea kwa lengo la kubaini maduka yaliyokuwa yanaendesha biashara kinyume cha sheria.

Maduka hayo yalidaiwa kutumika katika biashara haramu ya utakatishaji fedha.

## HABARI KITAIFA

# Mashirika 21 yalaani mauaji watoto Njombe

**Na Salome Kitomari**

MASHIRIKA 21 yasiyo ya kiserikali yanayojihusisha na utetezi wa haki za wanawake na watoto, yamelaani mauaji ya watoto 10 mkoani Njombe, huku yakiwakumbusha Watanzania kuheshimu na kulinda haki za watoto.

Aidha, Baraza la Wanawake wa Chadema (Bawacha), limelaani vikali ukatili dhidi ya watoto hao, na kwamba wanatambua maumivu makali yasiyo na mfano ambayo familia zimelazimishwa kupitia kutokana na matendo ya kifedhuli ya baadhi ya wanajamii wenzetu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana, jijini Dar es Salaam, tukio hilo ni la kinyama na linakwenda kinyume cha haki za binadamu.

Walitoa wito kwa serikali kuwa pamoja na jitihada zinazofanyika sasa kuhakikisha uchunguzi wa kina unafanyika kubaini kiini cha mauaji hayo ili wahusika wakamatwe na kufikishwa mbele ya mkono wa sheria.

"Tunaisihi serikali kuchukua hatua za haraka na za makusudi za kuongeza ulinzi dhidi ya watoto hasa katika maeneo yenye viasharia vya ukatili dhidi ya watoto," alisema.

Aidha, waliwataka waandishi wa habari kuendelea kukusanya habari na kuwaripoti wanaokiuka haki za watoto, kwa kuwa tukio hilo ni zao la kufumbiwa macho kwa matukio madogo madogo ya ukiukwaji wa haki za watoto.

"Tunawaomba wafiwa wote na Watanzania kwa ujumla, kuendelea kuwa watulivu katika kipindi hiki ambacho Jeshi la Polisi linachunguza ili wahusika wafikishwe kwenye vyombo vya sheria na kukabiliana na mashtaka yao," alisema.

Pia, waliwataka wanajamii kuhakikisha kuwa wanaheshimu sheria zinazolinda haki za watoto, kutimiza wajibu wa kuwalinda watoto bila kujali uhusika wa moja kwa moja kwa kuwa wanahitaji ulinzi kutoka kwa jamii nzima.

Kadhalika, wamewataka kutoa taarifa wanapohisi mtoto hayuko salama na kumpeleka sehemu salama, wazazi kuwa karibu na watoto wao na kujua walikokwenda na kuacha kuamini mila potofu zinazosababisha uvunjifu wa haki za binadamu ikiwamo haki za watoto na kusababisha watoto kupitia mateso makali na kupoteza maisha.

Mashirika yaliyotoa tamko hilo ni Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania

INAENDELEA UK. 8



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (kulia), akisalimiana na Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Dk. Severline Laika, katika hafla ya pamoja na wateja na wafanyabiashara jijini Mwanza juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Zitto awekwa kiporo kisa tril. 1.5/-

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amesema anamweka kiporo Zitto Kabwe kutokana na Mbunge huyo wa Kigoma Mjini (ACT-Wazalendo) kuishikia bango kashfa ya madai ya ubadhirifu wa Sh. trilioni 1.5 zinazotajwa kwenye ripoti iliyopita ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Kiongozi huyo wa Bunge amedai Zitto ni muongo, lakini wakati wa kumpeleka mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge haujafika.

Muda mfupi baada ya kumalizika kwa kipindi cha 'Maswali' bungeni, Spika Ndugai, aliyekuwa anaongoza kikao hicho cha tatu cha mkutano wa 14 wa Bunge la 11, alimshukia Zitto kwa kitendo chake alichodai kuandika uongo katika ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa Instagram.

"Huyu Zitto aliandika katika ukurasa wake wa Instagram kwamba, CAG alikuwa amefanya ukaguzi Hazina na katika ukaguzi huo, aligundua wizi mkubwa, ubadhirifu wa Sh. trilioni 1.5 na ametoa ripoti maalum ya ukaguzi huo na ripoti hiyo imefika Ofisi ya Spika na Spika amekalia ripoti hiyo," alisema.

Spika Ndugai aliongeza: "Sasa hayo mengine nilikuwa siyajali sana, kuhusu mimi kwa mfano kutuhumiwa kwamba nimekalia ripoti hiyo na hasa kwenye Instagram ya tarehe nane (Januari 8, 2019), ningependa kusema mbele ya Bunge hili na kwa wananchi wa Tanzania kwamba, ndugu yetu Zitto anapenda sana tabia za kusema uongo na haipendezi mtu mzima kusema uongo huo, siyo utamaduni wetu."

Huku akionekana kukerwa na mbunge huyo, Spika Ndugai, alidai kuwa kama hiyo barua imetoka kwa CAG na imeenda kwa Spika, wabunge walikuwa likizo na anashindwa kuelewa Zitto alijuaje wakati hafanyi kazi Ofisi ya Spika wa Bunge wala Ofisi ya CAG.

Spika Ndugai alisema: "Wewe (Zitto) unajuaje pale katikati? Unafanya kazi Ofisi ya CAG au inakuwaje? Lakini, niseme tu kwamba barua tajwa yeye alisema tarehe 8, mimi nimeletewa Ofisi ya Dar es Salaam tarehe 16, mwezi huu (Januari). Kwa hiyo, haikuwa kweli.

"Lakini pia, baada ya kuipata tarehe 16, muda mfupi baadaye nikawa nimeipeleka kwenye Kamati ya PAC (Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali) kama ilivyo ada, kwa sababu hata ninyi

INAENDELEA UK. 8

# Wapigakura wapya mil. 4 kuandikishwa

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

SERIKALI imesema itaanza mchakato wa uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura hivi karibuni kwa kuandikisha wapigakura wapya milioni nne.

Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Kazi na Ajira, Anthony Mavunde, aliiambia Bunge jijini Dodoma jana, kuwa uandikishaji utaanza wakati wowote baada ya serikali kumaliza kufanya maandalizi hayo. Mavunde alitoa kauli hiyo alipokuwa anajibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum, Cecilia Paresso (Chadema), aliyetaka kujua ni lini serikali itatatua changamoto zilizojitokeza katika daftari la wapigakura.

"Mchakato wa kuboresha daftari la kudumu la wapigakura ulianza Agosti, 2018, kwa kufanya maandalizi ya kuhuisha kanzidata ya daftari la kudumu la wapigakura na kuboresha mifumo ya uandikishaji na utunzaji wa kumbukumbu za daftari," Mavunde alisema. Alisema kwa mujibu wa Kifungu cha 15(5) cha Sheria ya Uchaguzi, Sura ya 343, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), iko katika hatua za maandalizi ya uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura kwa mara ya kwanza.

Alisema uboreshaji huo utafanyika kwa mara ya kwanza na uandikishaji wa majaribio kwa baadhi ya mikoa ili kuona ufanisi au changamoto zinazoweza kujitokeza unatarajiwa kuanza hivi karibuni. Mavunde pia alizungumzia changamoto ya ubovu wa mashine za kielektroniki zinazotumika kuandikisha wapigakura, akieleleza kuwa serikali imejipanga kuboresha mifumo yote kwa kupeleka vifaa vipya wakati wa mchakato huo.

Tangu kumalizika kwa uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikilalamikia kutokuandikishwa kwa wapigakura wapya kwamba vijana wanaofikisha umri wa miaka 18 wanakosa haki yao ya kikatiba kushiriki katika uchaguzi mbalimbali ambao umekuwa ukifanyika.


Group of Russian State Universities RACUS together with Russian-Tanzanian Cultural Centre invites you to

**Educational EXPO**
**«STUDY IN RUSSIA 2019»**

**5th February** 10a.m. till 4p.m.
**Venue:** The Russian-Tanzanian Cultural Centre (RTCC) Sea View Road, Plot 2043/3 P.O. Box 7722, Dar es Salaam

FREE ENTRY



The group of more than 20 Russian state universities offers more than 500 medical, engineering, technical, economic specialties in Russian & English languages of studies for BACHELOR'S, MASTER'S AND POST GRADUATE programs

**ADMISSION IS OPEN**
General Medicine; Dentistry; Pharmacy; Veterinary Medicine; Economics; IT; Oil and Gas Engineering; Mining Engineering; Geology; Mechanical Engineering; Telecommunications; Agronomy; Piloting; Air Navigation Maintenance; Civil Engineering; Architecture; Computer Science; Electrical Engineering; Management; International Relations, etc.

Average tuition and accommodation fees are **2700-3500 USD** per year depending on the specialty/university (provided is the reduced subsidized price).

Study in RUSSIA RACUS

To get more information on RACUS in Tanzania please contact:
The Russian-Tanzanian Cultural Centre (RTCC)
Tel: +255 22 213 6578 Mobile: +255 715 902270 / +255 713 307169
E-mail: rtcctanzania@gmail.com
Sea View Rd, Plot 2043/3 (near Aga Khan Hospital - Upanga)

**WWW.EDURUSSIA.RU**

# Kesi ya kina Mbowe yapata hakimu mpya

**Na Hellen Mwango**

KESI inayomkabili Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe, na wenzake wanane wanaokabiliwa na mashtaka ya uchochezi imepata hakimu mpya.

Jana kesi hiyo ya jinai namba 112/2018, ilitajwa mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Mfawidhi, Kelvin Mhina, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam.

Awali, kesi hiyo ilipangwa kusikilizwa mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu wa Mahakama hiyo, Wilbard Mashauri, ambaye sasa amepanda cheo na kuwa Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania. Mahakama ya Rufani Tanzania, imepanga kusikiliza rufani ya Jamhuri Februari 18, mwaka huu, dhidi ya walalamikiwa hao.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa na wanasubiri rufani iliyopo Mahakama ya Rufani. Wakili wa utetezi, Prof. Abdalah Safari, alidai kuwa rufani hiyo imepangwa kusikilizwa Februari 18, mwaka huu.

Hakimu Mhina alisema kwa sababu kesi hiyo imepangwa kutajwa mahakamani hapo, washtakiwa waliopo nje kwa dhamana wataendelea na dhamana na Mbowe na Mbunge wa Tarime Mjini, Esther Matiko, wataendelea kukaa ndani hadi uamuzi wa rufani utakapotolewa.

Mbali na Mbowe na Matiko, washtakiwa wengine wanaokabiliwa na kesi hiyo ni Naibu Katibu Mkuu wa Chadema, Zanzibar, Salum Mwalimu na Naibu Katibu Mkuu Bara, John Mnyika, ambaye pia ni Mbunge wa Kibamba.

Wengine ni Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche; Mbunge wa Kawe, Halima Mdee; Mbunge wa Bunda, Esther Bulaya; Katibu Mkuu wa chama hicho, Dk. Vincent Mashinji na Mbunge wa Iringa Mjini, Mchungaji Peter Msigwa.

Washtakiwa hao kwa pamoja wanakabiliwa na mashtaka 13, likiwamo kula njama, kufanya mkusanyiko wenye ghasia, kuhamasisha hisia za chuki, kushawishi hali ya kutoridhika, uchochezi na kushawishi utendaji wa kosa la jinai kati ya Februari 1 na 16, 2018, jijini Dar.

## Hofu ya usalama Jiji la Tanga

**Na Dege Masoli,** TANGA

HALMASHAURI ya Jiji la Tanga limekumbwa na mtikisiko wa matukio ya mauaji kwa raia na hali hiyo imesababisha hofu kwa wakazi na kuitaka Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilaya ya Tanga kubuni mbinu mbadala ya kuondoa shaka hiyo kwa wananchi.

Meya wa Jiji la Tanga, Mhina Mustaph, aliyesema hayo kwa niaba ya madiwani wa halmashauri ya Jiji hilo kwenye kikao cha kawaida cha baraza hilo ambapo alidai kuwa matukio ya mauaji ya kinyama, unyang'anyi na watu kujeruhiwa yanalitikisa Jiji hilo.

Alisema ni jukumu la Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilaya kuangalia namna ya kukomesha matukio hayo.

Mustaph ambaye ni maarufu kwa jina la SeleBoss, alisema hali hiyo inaathiri shughuli na maisha ya watu na kwamba licha ya matukio hayo kufanyika lakini hakuna aliyekamatwa. Aiitaka Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilaya kudhibiti matukio ya mauaji na uporaji wa mali za wananchi unaoendelea ili kurejesha amani na utulivu Wilayani hapa.

Katika kikao hicho ambacho kilihudhuriwa pia na wajumbe wa kamati hiyo ya ulinzi akiwamo Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Thobias Mwilapwa, Mustaph alisema hali ya utulivu wa Jiji la Tanga haijatengamaa kutokana na matukio mbalimbali ya mauaji ya watu wasiokuwa na hatia sambamba na watu kuporwa na kujeruhiwa na kwamba ni jukumu la kamati hiyo kutembea.

"Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya, bahati nzuri na wewe upo hapa, tuseme ukweli nami mara nyingi ndiyo utamaduni wangu, hali siyo nzuri, ifike wakati sasa tuangalie mbinu mbadala ya kukabiliana na hali hii watu wanaishi kwa hofu kubwa" alisema Mustaph.

Alisema licha ya matukio hayo kupungua katika baadhi ya kata jijini hapa, lakini hali haijakuwa shwari kwa baadhi ya kata ikiwemo kata ya Maweni na Nguvumali.

Alisema tatizo la uharifu kwa Jiji la Tanga kuwa bado ni kubwa kwa baadhi ya kata na kuomba kuwepo kwa doria ili kuimarisha ulinzi ipasavyo kwasababu mambo hayo ni ya udhalilishaji kwa wananchi na serikali yao.

Kwa upande wake, Mwilapwa alisema Kamati ya Ulinzi na Usalama wa Wilaya imejipanga kuhakikisha uhalifu huo unakoma kwa gharama yoyote ili kurejesha hali ya wakazi hao katika utulivu kama ilivyokawaida.

Aliiomba jamii kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama kutoa taarifa za watu, vikundi vya watu vinavyojihusisha na vitendo vya uvunjifu wa amani katika maeneo yao ili kuweza kudhibiti matukio hayo.



Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Richard Kasesela (kushoto), akiteta jambo na Askofu wa Dayosisi ya Iringa KKKT, Blaston Tuluwene Gavile (katikati) na Askofu mstaafu wa dayosisi hiyo, Owdenburg Mdegela, baada ya mkutano mkuu maalumu wa kuchagua msaidizi wa askofu, ambao uliofanyika katika Kanisa la KKKT Usharika wa Ipogolo. **PICHA: GEORGE TARIMO**

## Gesi asilia sasa yatua nyumbani, viwandani

**Na Salome Kitomari**

RIPOTI ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, kwa mwaka wa fedha 2015/16, ilibainisha kuwa bomba la gesi asilia linatumika kwa asilimia sita, huku Shirika la Umeme (Tanesco) likiwa ndiyo mtumiaji pekee wa bomba hilo.

Katika ripoti yake hiyo, CAG Assad, alisema suala hilo ni kinyume cha matarajio ya wengi kwamba gesi hiyo ingenufaisha wananchi wengi.

Katika kutekeleza mapendekezo ya CAG Assad ambaye alishauri gesi hiyo itumike kwa mambo mengine mbali na ufuaji wa umeme, Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC) limeanza kusambaza gesi asilia kwenye nyumba za wananchi katika maeneo ya Mikocheni na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Vilevile, gesi imewekwa kwenye viwanda mbalimbali, ikiwa ni pamoja na viwanda vya Coca-Cola na Bidco, vilivyopo Mikocheni. Awali gesi hiyo ilikuwa inatumika kwenye nyumba za TPDC pekee.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa TPDC, Maliki Munisi, alisema usambazaji umefanikiwa baada ya kazi hiyo kuanza mwaka jana kwa kutoa gesi kupitia bomba dogo kwenye Kituo cha Ubungo kwenda kwenye maeneo husika.

"Gesi asilia inasambazwa kutoka Ubungo kupitia Barabara ya Sam Nujoma hadi Mikocheni, na huko njiani nyumba zilizoko jirani na bomba zinashawishiwa kuunganishiwa huduma hiyo," alisema.

Aliyataja maeneo yatakayopata gesi hiyo kuwa ni UDSM, ambayo kwa sasa wataanza na mgahawani, wakifuatwa na Sinza, Mlalakua, Shekilango, Mwenge na Mikocheni.

"Tayari ujenzi umeanza kwenye nyumba 24 ambazo wanajengewe mfumo na kuungwa kwenye mita, pia mgahawa wa UDSM nao unaungwa, kazi hiyo

INAENDELEA UK. 8

# Majaliwa aongoza mazishi mke wa Mufti

**Na Mwadishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, jana alimwakilisha Rais John Magufuli katika mazishi ya mke wa Mufti na Sheikh Mkuu wa Tanzania, Sheikh Aboubakary Bin Zubeir, yaliyofanyika Kwamndolwa, Korogwe mkoani Tanga.

Akitoa salamu kwa niaba yake, Majaliwa alisema Rais Magufuli aliweka nia ya dhati kushiriki mazishi haya ila kwa bahati mbaya jana alikuwa na Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki jijini Arusha, ambapo yeye ni mwenyekiti.

"Mheshimiwa Rais amenituma nije nikupe pole wewe, watoto, familia na wote walioguswa na msiba huu. Mheshimiwa Rais anawaombea kwa Mungu ili mpate utulivu katika kipindi hiki kigumu cha kuondokewa na nguzo katika familia. Haya yote ni mapenzi ya Mwenyezi Mungu," alisema.

Waziri Mkuu alishiriki mazishi hayo ya mke wa Mufti, Bibi Hidaya Omar leo (Alhamisi, Januari 31, 2019).

Kadhalika, Waziri Mkuu, aliwasihi wafiwa na waombolezaji wote waendelee kuwa watulivu na kumwombea marehemu kila mmoja kwa imani yake, ili Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahala pema.

Kwa upande wake, Sheikh wa Mkoa wa Dar es Salaam, Sheikh Alhad Mussa Salum, akizungumza kwa niaba ya familia alimshukuru Rais Magufuli kwa kumtuma Waziri Mkuu amwakilishe katika mazishi hayo. Pia aliwashukuru watu wote waliojitokeza kwa ajili ya kuifariji familia kutokana na msiba walioupata.

Viongozi wengine waliohudhuria mazishi hayo ni Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu; Waziri wa Nchi -TAMISEMI, Selemani Jafo; mke wa Rais mstaafu, Salma Kikwete; Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martine Shigella; masheikh wa Mkoa wa Tanga na viongozi mbalimbali.



Spika wa Bunge, Job Ndugai (kulia), akimsikiliza Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Dk. Maulid Banyani, alipomtembelea ofisini kwake Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# Maombi ya Zitto kuhusu CAG Feb. 15

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania, Kanda ya Dar es Salaam, Februari 15, mwaka huu, imepanga kusikiliza kesi ya kikatiba kuhusu kinga ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), kwa mujibu wa Katiba ya nchi na Mamlaka ya Bunge katika kuwaita na kuwahoji watu mbalimbali.

Mahakama hiyo iliyoketi chini ya jopo la majaji watatu, likiongozwa na Mwenyekiti na Firmin Matogolo, Dk. Benhajj Masoud na Elinaza Luvanda ilikubali ombi la mlalamikaji la kutaka maombi hayo yasikilizwe.

Awali wakili wa mlalamikaji, Fatuma Karume, aliomba mahakama hiyo kufanya mabadiliko ya maombi hayo ikiwamo kuondoa ombi la (CAG), Prof. Musa Assad, kuitwa kuhojiwa na Kamati ya Bunge.

Wakili wa Serikali Mkuu, Elisia Mbuya, alidai kuwa si utaratibu kufanya mabadiliko ya kuondoa baadhi ya maombi yao na kwamba walipaswa kufungua upya.

Hata hivyo, Karume alidai lengo la kuondoa ombi hilo ni kwamba limepitwa na wakati, hivyo litapoteza muda wa walalamikiwa kujibu.

"Naomba kuondoa ombi langu la kufanya mabadiliko ya kuondoa ombi la pingamizi la kumhoji CAG, kesi iendelee," aliomba Karume.

Jopo la majaji hao lilisema limekubali ombi la mlalamikaji, upande wa walalamikiwa watawasilisha majibu ya ndani ya siku 14 kama Sheria inavyoelekeza na maombi ya msingi yatasikilizwa Februari 15, mwaka huu.

Kesi hiyo ya kikatiba namba 01/2019, imefunguliwa Mahakama Kuu, Masijala Kuu na Mbunge wa Kigoma Mjini, Zitto Kabwe, dhidi ya Spika wa Bunge, Job Ndugai.

Katika kesi hiyo, Zitto ambaye pia ni Kiongozi Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, anaiomba Mahakama Kuu itoe tafsiri ya kinga ya CAG iliyopo kikatiba na tafsiri ya Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge katika kushtaki watu wanaosemekana kulidharau Bunge.

Zitto alifungua kesi hiyo baada ya Spika kupitia kwenye vyombo vya habari na baadaye kumwandikia barua CAG, Prof. Assad, akimtaka afike mbele ya Kamati ya Bunge kuhojiwa kutokana na kauli aliyoitoa akiwa Marekani kuwa Bunge ni dhaifu.

Profesa Assad alitoa kauli hiyo kama maoni yake wakati akihojiwa na Idhaa ya Kiswahili ya Redio ya Umoja wa Mataifa, kulingana namna taarifa zake za ukaguzi zinavyofanyiwa kazi.

Kesi hiyo ilisajiliwa Januari 21, mwaka huu baada ya kushindikana awali kutokana na upungufu wa kisheria.

# Mvumbuzi tanzanite kuzikwa kesho Same

**Na Romana Mallya**

MVUMBUZI wa madini ya tanzanite, mzee Jumanne Ngoma (85) aliyefariki juzi katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), anatarajiwa kuzikwa kesho Makanya Wilaya ya Same mkoani Kilimanjaro.

Kwa mujibu wa mtoto wa marehemu, Hassan Ngoma, baba yao atazikwa Jumamosi Makanya ambapo leo taratibu zitakazofanyika jijini Dar es Salaam ni dua na kumswalia katika msikiti wa Masjid Maamur Upanga na baadaye safari kuelekea Same.

Akizungumza na Nipashe juzi jioni, Hassan alisema kuwa baba yake alifariki dunia siku hiyo baada ya kufikishwa chumba cha dharura akitolewa hospitali ya Boch iliyoko Kimara jijini Dar es Salaam.

Hassan alisema baba yake hadi umauti unamkuta alikuwa akisumbuliwa na maradhi ya kiharusi.

"Baba yetu alilazwa jana (juzi) hospitali ya Boch, Kimara na ilipofika mchana alihamishiwa hospitali ya Muhimbili lakini wakati akiwa chumba cha dharura Muhimbili majira ya saa 7:00 mchana alifariki dunia," alisema.

Aprili 6, mwaka jana Rais John Magufuli alitangaza kumtambua Mzee Ngoma kuwa ndiye mvumbuzi wa madini ya Tanzanite na alimpatia Sh. Milioni 100 ili zimsaidie kwenye matibabu kutokana na maradhi yaliyokuwa yanamkabili.

Rais Magufuli alitangaza kumtambua mzee Ngoma akiwa mji mdogo wa Mirerani uliopo wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara wakati akizindua ukuta uliozunguka machimbo ya madini ya Tanzanite uliojengwa na kikosi cha majeshi ya ulinzi Tanzania.

"Nimeona nimlete hapa ili Watanzania wamtambue, ili kusudi akatibiwe vizuri, Serikali itampa Sh. milioni 100 ili akazitumie katika matibabu yake na kujisitiri mambo mengine, fedha hii itawekwa kwenye akaunti yake kesho au kesho kutwa zimsaidie," alisema siku hiyo Rais Magufuli wakati akimueleza mzee Ngoma.

# Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Kila la heri mnunuzi mkubwa wa korosho

**BAADA** ya kampuni mbalimbali ya ununuzi wa korosho kutoonyesha nia ya kukunua zao hilo kutoka kwa wakulima, na serikali kuamua kujitosa kununua korosho hizo msimu huu, hatimaye kitendawili hicho kimeteguliwa. Sasa amepatikana mnunuzi mkubwa wa zao hilo Kampuni ya Indopower Solutions ya Kenya, mbayo tayari imenunua tani 100,000 za korosho kwa Sh. bilioni 418, fedha ambazo zitalipwa ndani ya siku saba kuanzia juzi.

Mkataba wa mauziano ulitiwa saini juzi jijini Arusha kati ya Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko, Hussein Mansoor na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Indopower Solutions, Brian Mutembei na kuhudhuriwa na viongozi waandamizi wa serikali akiwamo Waziri wa Katiba na Sheria, Prof. Palamagamba Kabudi, Waziri wa Viwanda na Biashara, Joseph Kakunda, Naibu Waziri wa Kilimo, Innocent Bashungwa, Gavana wa Benki Kuu Tanzania (BoT), Prof. Florens Luoga, makatibu wakuu wa wizara hizo na Balozi wa Kenya nchini, Dan Kazungu. Kwa mujibu wa Prof. Kabudi, mauziano hayo yataipatia Tanzania Sh. bilioni 418 kama bei ya jumla na fedha hizo zitaingizwa BoT moja kwa moja.

Waziri Kakunda alisema kampuni ya Indopower Solutions ni kati ya kampuni 18 zilizoonyesha nia ya kununua kiasi hicho cha korosho ghafi. Zingine hazikufanikiwa kukidhi masharti.

Kwamba kuuzwa kwa kiwango hicho cha korosho kunafanya korosho ambazo zimebaki kwenye ghala kuwa tani 63,000. Jitihada za serikali za kutafuta kampuni makini, zenye uhakika na zenye uwezo mkubwa kwa ajili ya kununua korosho ni za kupongeza kwa sababu bila kufanya hivyo, wangepatikana wanunuzi ambao lengo lao ni kujinufaisha; kwa maana ya kumlipa mkulima fedha ndogo ambazo ni sawa na kumnyonya.

Nia hiyo ovu ya wanunuzi wababaishaji ilibainika mwaka jana wakati serikali ikijaribu kuzungumza nao kufikia mwafaka wa masuala mbalimbali, ikiwamo bei ya kununulia. Ndiyo maana baada ya kampuni hizo kuweka wazi kuwa ziko tayari kulipa shilingi 3,000 kwa kilo moja, Rais John Magufuli alikataa na kusema serikali itabeba jukumu la kuzinunua korosho hizo kwa bei ya shilingi 3,300 kwa kilo moja.

Rais Magufuli kutokana na kuona ubabaishaji huo aliagiza kuachana na kampuni zilizokuwa zimepewa muda wa kujitokeza kuzinunua korosho hizo, huku akisisitiza kwamba hakuna sababu ya kuendelea kuzibembeleza kwa kuwa huko mbele zitaendelea kusumbua kila msimu wa ununuzi wa zao hilo. Kupatikana kwa mnunuzi huyo mkubwa ni kithibitisho kuwa korosho za Tanzania ni bora na zinakubalika katika masoko ya kimataifa, hivyo kilichobaki sasa ni kwa wakulima wetu kuzingatia karatibu na kanuni za uzalishaji wa korosho zenye ubora unaozingatia viwango vya kimataifa.

Kwa kuwa serikali imeshalijumuisha zao la korosho katika mazao matano ya kimkakati, italipa kipaumbele kwa kutumia wataalamu kufuatilia uzalishaji wake ili zikidhi viwango vya kimataifa. Hili lifanyike kwa wataalamu hao hawanabudi kuwashauri wakulima na kuwapa mbinu za kisasa za uzalishaji. Kwa upande wa serikali kupitia bodi za mazao na wizara husika inawajibika kufuatilia masoko ya korosho na mazao mengine kuhakikisha mazao yanauzwa kwa bei nzuri na bila kuwanyonya wakulima.

Pamoja na kwamba kuna baadhi ya watu wanadai kuwa sio kazi ya serikali kufanya biashara, lakini kuna mazingira ambayo inabidi likiwamo sakata la korosho, ambalo lilisababisha serikali kutimiza wajibu wake wa kuwalinda wakulima kwa kuweka bei elekezi ya zao hilo na kuamua kuinunua baada ya kuwabaini wanunuaji hawana nia njema.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mhariri Wikiendi:** Epson Luhwago
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com





## Muungwana Lazima Nilonge

# Tuchukue hatua zaidi, usalama vituo vya mafuta

Na Yasmine Protace

JANA katika safu hii, niliandika mtazamo wangu dhidi ya tabia mbalimbali za makondakta wa daladala, wanapohudumia abiria wao.

Mtazamo mkuu ulikuwa matumizi ya kauli chafu kutoka kwa ndugu hao wanapohudumia magari hayo, baadhi yao wanatoa ujumbe mchafu zaidi.

Ikumbukwe katika mtazamo mpana, ndugu hawa wana mwingiliano mtambuka katika maisha halisi walio nayo dhidi ya wasafiri.

Kuna kingine kinachowahusu zaidi madereva, hasa wanapokuwa katika vituo vya kuweka mafuta, wakisisitizwa kuzima magari yao, ikiendanana mengine ya watu wasivute sigara, na kuzima simu zao.

Tujiulize kidogo, ni jukumu la nani kumwambia mteja achukue hatua stahiki dhidi ya hayo?

Ni kawaida mtu akiwa ndani ya vituo vya mafuta, mara moja ataona tangazo la kukataza kupitia picha zinazokataza. Najua kuwapo ujumbe huo, kunamaanisha kuweka usalama katika kituo cha mafuta.

Hili ni la msingi linalopaswa kuzingatiwa, kwa sababu chochote kinaweza kutokea na kusababisha watu kupoteza uhai wao.

Pamoja na kukatazwa huko, kunashuhudiwa magari bado yanaingia katika vituo vya mafuta na kuhudumiwa bila ya kuzimwa na wahudumu wa kituo cha mafuta wanaendelea kuweka mafuta, kana kwamba hakuna hatari yoyote.

**Kuna kingine kinachowahusu zaidi madereva, hasa wanapokuwa katika vituo vya kuweka mafuta, wakisisitizwa kuzima magari yao, ikiendanana mengine ya watu wasivute sigara, na kuzima simu zao.**

Kuna madereva wengine, sambamba na baadhi ya abiria wanatumia simu zao wakati huduma za kujaza mafuta zinaendelea. Sasa sijui nani anatakiwa kutupiwa lawama kwa kuendekeza hivyo vitu ambayo ni hatari.

Ni kawaida hakuna mwekaji mafuta, anayemzuia dereva, hata inapotokea hajazima gari, ni adimu kumkuta mfanyakazi wa kituo cha mafuta analalamika.

Masingi mkuu ni kwamba, anatakiwa awapo mhudumu wa kituo cha mafuta kuwa makali na makini, dhidi ya ukiukwaji wa kanuni hiyo ya usalama.

Pia, nadhani kuna haja ya elimu zaidi ikatolewa juu ya athari zinazoweza kutokea, pale magari yanapoendelea kuunguruma wakati wa kujaza mafuta yake.

Inawezekana hata waliopo katika kituo cha mafuta, uelewa wao ni finyu kuhusu kanuni na sheria zao za kazi na mahali pa kazi.

Elimu ikiendelea kutolewa, jamii itajua athari za kujazwa mafuta, huku gari halijazimwa, kunakuwapo hatari. Kwa kutotolewa elimu ya kutosha hali, maboresho ya kiusalama tutayaona.

Jamii ikifika hatua ya kuwa na elimu ya kutosha, inakuwa katika hatua nzuri ya kupambana na madereva wanaoshindwa kuzima injini za magari wanapoweka mafuta.

## BARUA/MJADALA

# Tanesco Tegeta wajibikeni

**Mhariri,**

*NAKUPONGEZA kutokana na unavyotoa gazeti lenye habari za kutuelimisha, kutupasha na kutuburudhisha.*

*Pia nakupongeza sana kutokana na ukurasa wako huu kuchapisha taarifa zenye kero mbalimbali zinazoigusa jamii.*

*Nimeandika barua hii kueleza jinsi ninavyopata usumbufu kwa wafanyakazi wa kitengo cha luku Tanesco wilaya ya Tegeta mkoani Dar es Salaam.*

*Mimi mteja wa shirika nilitoa taarifa na kupewa namba 3697 kuhusu mita yangu ya Luku kuwa na tatizo la kunata ninapoweka umeme, hivyo kugoma kuingia.*

*Nilitoa kwanza taarifa kitengo cha dharura zaidi ya wiki moja, wakatuma fundi akaondoka akidai wahusika ni watu wa mita za luku na kuwa amewapa taarifa.*

*Nilikwenda mwenyewe kesho yake ofisi ya Luku nikaahidiwa kuwa watatuma fundi na atanipigia kabla ya hapo, lakini kila siku nikipiga simu wananiambia fundi atakuja bila kueleza nitasaidiwaje.*

*Kwa kweli urasimu huo nimeuchoka na nimeathirika kwa kuwa sina umeme kwa wiki nzima sasa.*

*Nauomba uongozi wa juu wa Tanesco unisaidie na pia kufuatilia huduma za ofisi hii kwa sababu inaelekea wateja wengi wanatendewa sivyo.*

*Nashangaza kuona kipindi hiki ambacho serikali ya Rais John Magufuli inahimiza uwajibikaji bado kuna watumishi wa umma hawajali shida za wananchi.*

**Ni mimi, mkazi wa Mbweni Tegeta, Dar es Salaam.**

**WASILIANA NASI:**

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**

# Kisarawe tuwe makini uuzaji ovyo ardhi zetu




**Na Amri Lugungulo,**
KISARAWE

MCHEZA kwao hutunzwa. Nami nianze kwa kumwaga sifa kwa wilaya hii kongwe - Kisarawe, ambayo ina nafasi yake katika ustawi na maendeleo ya jamii, jirani na inakofika bidhaa zake.

Ni wilaya ambayo huko nyuma ilikuwa moja na Mkuranga na nyuma zaidi, mkoa wake wa Pwani ulikuwa kitu kimoja na Dar es Salaam

Hapo ndipo kwenye kioo cha uzalishaji mihogo kitaifa na kuna simulizi nyingi, kumtoa mwanamuziki maarufu nchini, Marehemu Mbaraka Mwinshehe Mwaruka.

Nikirejea shule ya Minaki, ambayo ni matunda ya waseminari, nayo ina mengi ya kusimuliwa katika kutusaidia sisi na taifa letu kwa jumla.

Ardhi ya Kisarawe iko nzuri sana tangu zamani hadi leo hii. Ninaweza kudokeza zao la muhogo, ubora na utamu wake, niko bega kwa bega kwa wakazi wa Dar es Salaam.

Niseme, migogoro ya mipaka baina ya vijiji vilivyoko na kata katika wilaya ya Kisarawe, mkoa wa Pwani, inabidi kuchukuliwa tahadhari, ili kuondokana na udanganyifu unaofanywa na baadhi ya viongozi wa maeneo hayo, baada ya vikao vya usuluhishi.

Hivi karibuni kumezuka migororo ya kutakaa kupanua maeneo ya vijiji na baadaye yakauzwa kwa watu wa nje, kwa manufaa yao.

Baada ya kupata maeneo hayo, watu hao kamwe hawayatumii kwa ajili ya kuwekeza katika miradi yao ya maendeleo.

Nimebaini kutokea mizozo mikali, hadi baadhi ya viongozi wa kisiasa, wakiwamo madiwani wanaingilia kati usuluhishi.

Migogoro mingine imejadiliwa kwenye vikao vya Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya Kisarawe na kutolewa uamuzi kwa watendaji kusimamia kumalizika migogoro.

Aina ya migogoro hiyo imezuka kuanzia katika vijiji, viongozi wakahitaji, lakini yakawa mazito hadi kudai msaada wa ngazi za juu. Walifanya kazi ya ziada kusuluhisha migogoro hiyo.

Mathalan, naukumbuka mgogoro kati ya kijiji cha Palaka, kilichoko katika Kata ya Marumbo na kijiji cha Kidugalo, kata ya Kurui wilayani humo.

Nilichobaini ndani ya mtazamo wa uchunguzi wangu binafsi ni kwamba, migogoro kama hiyo bado inaendelea kwenye vijiji vingine.

Kote huko, hatima yake imeonekana ni madhumuni ya watu waliokuwa mstari wa mbele kugombea mipaka ardhi, wajiongezee maeneo, ili kujinufaisha kwa njia ya kuyauza.

Wahitaji wanaonunua ardhi hiyo, wanatoka nje ya vijiji husika, wilaya na hata mkoa. Sote tunajua 'ardhi ni mali.'

Niseme, udanganyifu huo unaoendelea katika baadhi ya vijiji wilayani humo, unatokana na wananchi wa kawaida kuona ardhi si mali kwao na wanaamua kushiriki katika biashara ya uuzaji mashamba yao mithili ya karanga, wakibakiwa katika hali ya 'patupu.'

Migogoro ya ardhi kwa ujumla au inayohusu mipaka, inachangiwa na baadhi ya viongozi wasiozingatia Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya Mwaka 1999.

Hivi sasa tulikofika, kuna vijiji vinavyodaiwa kuuza maeneo zaidi ya eka kati ya 51 na 500, wakati sheria ninavyoielewa, kijiji mwisho wake ni kuuza ekari zisizozidi 50.

## KABWELA NA FADHIL MOHAMMED



# Zitto awekwa kiporo kisa tril. 1.5/-

INATOKA UK. 3

wenyewe ubadhirifu wa Shilingi trilioni 1.5, hivi Spika anakaliaje?"

Alisema kama Bunge lilihangaika na hoja ya Zitto katika sakata lililohusu kuchotwa kwa fedha katika akaunti ya Escrow zaidi ya Sh. bilioni 300, haoni sababu leo Spika kukalia sakata la Sh. trilioni 1.5.

Katika maelezo yake, Ndugai alidai kitendo hicho cha Zitto kuandika alichokiita uongo, ni kupakana matope na taifa zima linamwona Spika ni mtu wa ajabu ajabu.

"Na haya yanatokana na ninyi wenyewe wabunge kuipaka matope ya kila aina Ofisi ya Spika. Sasa, sijui kwa madhumuni gani. Kwa hiyo, niseme kwamba taarifa hiyo haikuwa ya kweli, ni taarifa ni ya uongo," alisema.

Spika Ndugai aliwakumbusha wabunge kuwa Aprili 20, mwaka jana, wakati Rais John Magufuli anawaapisha majaji Ikulu Dar es Salaam, alimuuliza CAG Prof. Mussa Assad, kuhusu kutomsomea taarifa hiyo kabla hajaiwasilisha bungeni na kumwambia habari ya kutoonekana kwa matumizi ya Sh. trilioni 1.5 zilizokusanywa na serikali. "Ninyi wote mliosikiliza, CAG alimjibuje pale? Kasema hakuna mambo kama hayo mbele ya Rais, Ikulu," Spika Ndugai alisema.

"Na wiki iliyopita, nilipeleka jambo hili kwenye Kamati ya PAC na iliulizwa pia kama kuna wizi wa aina hiyo, yeye mwenyewe (CAG) akiwapo, 'Deputy' (Naibu) CAG, akajibu hakuna wizi wowote wala ubadhirifu wa Sh. trilioni 1.5."

Spika Ndugai alitoa ushauri wake kwa wabunge kwa ujumla wake kwamba, ni vyema wakajikita katika ushindani wenye tija badala ya kuendesha siasa zisizokuwa na maana na kutoa taarifa zinazoenda dunia nzima kama vile kuna jambo fulani ambalo halina tija.

"Leo natoa tu kwa Watanzania wajue katika hili, Zitto ni muongo, na akitaka nimfanyie utafiti wa mengine ya uongo wa ambayo ameyasema, yapo ya kutosha, badilika, badilika ndugu yangu, mbona mimi sijawahi kukusingizia, hujisikii vibaya, yaani kwenye moyo wako?" Spika Ndugai alisema.

Siku moja baada ya kuwasilishwa bungeni kwa ripoti ya ukaguzi wa CAG kwa mwaka wa fedha 2016/17, Zitto aliitisha mkutano na waandishi wa habari jijini Dodoma na kueleza kuwa ameipitia ripoti hiyo na kubaini kutoonekana kwa matumizi ya Sh. trilioni 1.5 zilizokusanywa na serikali.

Serikali kupitia kwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, ililazimika kutoa ufafanuzi wa suala hilo bungeni wakati wa Bunge la Bajeti, lakini PAC ilisema itajiridhisha zaidi kuhusu suala hilo kwa kuwaita CAG, Gavana wa Benki Kuu (BoT), Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha Zanzibar, ili watoe ufafanuzi mbele ya kamati hiyo.



Mkurugenzi Mkuu wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Lilian Liundi, akiwaelekeza jambo wanawake viongozi wa asasi zisizo za kiserikali walipokuwa kwenye semina ya siku mbili iliyoandaliwa na Chama cha Wanawake katika Maendeleo na Sheria (WiLDAF), kwa ajili ya kujadili masuala mbalimbali yanayowahusu wanawake. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Gesi asilia sasa yatua nyumbani, viwandani

INATOKA UK. 4

inafanywa na TPDC yenyewe na mafundi wetu wapo kazini kwa sasa," alisema.

Aliongeza kuwa nyumba 55 za maeneo ya UDSM, nazo zitaunganishwa huduma hiyo baadaye kwa kuwa lengo ni kuhakikisha Watanzania wananufaika na huduma hiyo na kuachana na matumizi ya mkaa.

Kwa mujibu wa Munisi, wanashindwa kusambaza gesi asilia hadi maeneo ya ndani, kwa kuwa hakuna miundombinu mizuri na kwa sasa wanapitisha kwenye barabara zenye miundombinu mizuri na nyumba zilizoko maeneo hayo.

Alisema iwapo watajitokeza wananchi wakaungana kati ya 10 hadi 20 na kuwa tayari kuunganishwa na huduma hiyo, TPDC itafanya hivyo kwa kuwa ndiyo itakuwa rahisi kuliko kuunganisha mtu mmoja au wawili kwenye eneo moja.

"Kila mteja ataungiwa huduma hiyo baada ya kuletewa mita. Tunawahimiza watu waungane, walete maombi nasi tutawaungia huduma hiyo," alisema.

Munisi alisema lengo la serikali ni kusambaza gesi asilia kwenye maeneo yote nchini, ili kuachana na matumizi ya mkaa.

"Mkoa wa Mtwara na Lindi nako tumeanza kutengeneza mifumo, nyumba zinazostahili kulipwa fidia kupisha mradi zimeshafahamika. Changamoto ni upatikanaji wa vifaa ambavyo vingi vinaagizwa nje ya nchi kwa oda maalum ambayo huchukua muda mrefu kukamilika," alisema.

# Mashirika 21 yalaani mauaji watoto Njombe

INATOKA UK. 3

(Tamwa), Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu Tanzania (LHRC), Msichana Initiatives, Agaoe Aids Control Program, Faidika Wote Pamoja, Paralegal Primary Justice na Jumaewape.

Mengine ni PEMCO, KIWOHEDE, Children Diginity Forum, K.O.K Foundation, ZAFAYCO, Msichana na Uongozi na Micheweni Islamic Development, Environment Conservation and AIDs Control (MIDECAC).

Mengine ni Door of Hope to Women and Youth Tanzania, Zanzibar Aids Association for Children Advancement, Morogoro Paralegal na Mbeya Hope for Orphans na Tanzania Youth Potential Association.

Watoto hao waliuawa wiki iliyopita kwa kukatwa koromeo, kunyofolewa sehemu za siri, masikio na ulimi kwa kile kilichoelezwa kuwa ni kulipiza kisasi na imani za kishirikina.

Naye, Mwenyekiti wa Bawacha, Halima Mdee, alisema wanaungana na wanawake wa Njombe na maeneo mengine nchini kuwalilia watoto hao ambao uhai wao umekatizwa bila hatia yoyote.

"Bawacha tunasema hakuna sababu yoyote inaweza kukubalika ndani ya jamii iliyostaarabika na inayotambua haki za binadamu kuhusu mauaji hayo. Tunaitaka serikali kupitia vyombo vya dola ichukue hatua zote zilizoko ndani ya mamlaka yake kisheria," alisema.

Mdee alisema Bawacha inasisitiza udhibiti wa mtandao wa wahusika kwa sababu katika miaka ya hivi karibuni Watanzania wameshuhudia kuongezeka kwa vitendo vya utekaji, mauaji na kutelekezwa kwa miili ya watu waliouawa, lakini hawaoni hatua madhubuti za kukomesha hali hiyo kutoka kwa mamlaka husika hususani vyombo vya dola.

"Matukio haya yanazidi kujirudia, kushamiri na kusambaa sehemu mbalimbali za nchi yetu. Tunaitaka serikali kuchukua hatua za haraka, za muda mfupi na mrefu na kuutaarifu umma, ili kuondoa hofu inayokumba watoto wa Njombe na wazazi wao."

# Mbaroni tuhuma za kubaka mtoto wa dada

**Na Gedion Mwakanosya,**
SONGEA

JESHI la Polisi mkoani Ruvuma limemtia baroni Erick Ndomba (38), mkazi wa kijiji cha Mbaha wilayani Nyasa kwa tuhuma za kumbaka msichana wa umri wa miaka 15 (jina limehifadhiwa) ambaye ni mtoto wa dada yake ambaye alifariki dunia mwaka jana. Kaimu Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Ruvuma, Pill Made, alisema tukio hilo lilitokea katika Kijiji cha Mbaha ambapo inadaiwa katika siku zisizofahamika kwa nyakati tofauti Januari mwaka huu, binti huyo ambaye ni mwanafunzi wa Shule ya Msingi Mbaha, alifanyiwa kitendo cha Kinyama na mtuhumiwa ambae ni mlezi wake. Alifafanua kuwa Msichana huyo inadaiwa alikuwa anaishi nyumbani kwa Mjomba wake Ndoma baada ya kufiwa na mama yake Mzazi na kwamba mtuhumiwa alitumia mbinu ili aweze kufanya mapenzi na Mjomba wake ambaye alikubaliana kufanya nae Mpenzi kwa Ahadi ya kumnunulia madaftari.

Alisema baada ya kurubuniwa na mtuhumiwa, mtoto huyo alimfuata porini wanakofugia ng'ombe, kwa kisingizio kuwa alikuwa anafuata maziwa, ndipo mtuhumiwa alipopata nafasi ya kufanya uhalifu huo.



Mkurugenzi wa Mikopo wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Augustino Chacha (Katikati), Meneja Mkuu wa Kampuni ya Mbolea ya YARA Tanzania, William Ngeno (kulia) na Mkurugezi wa Taasisi ya Kilimo ya Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki (kushoto), wakibadilishana nyaraka mara baada ya kusaini makubaliano ya kuwainua wakulima na kuendeleza kilimo ikiwamo upimaji wa afya ya udongo ili kuchochea uzalishaji wa mazao nchini. **MPIGAPICHA WETU**

# Kampuni ya mbolea TADB, TARI kuwainua wakulima

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI tatu nchini zimeingia makubaliano ya kuwainua wakulima na kuendeleza kilimo ikiwemo upimaji wa afya ya udongo ili kuchochea uzalishaji wa mazao hapa nchini. Taasisi hizo zilizoingia katika makubaliano ni Kampuni ya Mbolea ya YARA Tanzania, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ya Uyole.

Wakizungumza baada ya kusaini randamu ya ushirikiano huo unaotarajiwa kuleta mageuzi katika sekta ya kilimo, Meneja Mkuu wa Yara Tanzania,William Ngeno, alisema makubaliano hayo ni hatua muhimu ya kumsaidia mkulima na kuleta mageuzi katika sekta ya kilimo.

"Makubaliano haya ni muhimu sana kwani yatasaidia kubadili maisha ya wakulima wadogo ili waweze kufanya na kilimo chenye tija kitu ambacho YARA imekuwa ikisimamia kwa miaka mingi tangu kuanzishwa kwake Tanzania, alisema Ngeno. Ngeno aliongeza kuwa wakulima wamekuwa wakipata changamoto mbalimbali ikiwamo upatikanaji wa mikopo, usambazaji wa pembejeo na kukosekana kwa ubunifu, hivyo makubaliano hayo yataenda kutatua changamoto hizo na kupelekea ongezeko la uzalishaji.

"Kwa miaka mingi sekta ya kilimo imekuwa ikikabiliana na changamoto nyingi ikiwamo ukosefu wa elimu ya kutosha kwa wakulima, uchelewashaji wa pembejeo na upatikana wa mbolea yenyewe kwa wakati, nina hakika makubaliano haya yanaenda kumgusa mkulima moja kwa moja na kutatua changamoto za muda mrefu katika sekta hii," alisema Ngeno.

Mkurugezi wa Mikopo waTADB, Augustino Chacha, ambaye alimwakilisha Mkurugenzi Mtendaji wa benki, Japhet Justine mbali ya kupongeza makubaliano hayo, alisema elimu juu ya afya ya udongo ni muhimu ikawafikia wakulima ili kuongeza tija katika uzalishaji.

"Wakulima wamekuwa na changamoto nyingi na hivyo makubaliano haya yakatafsiriwe katika kuzitatua changamoto hizo," alisema na kuiongeza kuwa TADB itahakikisha inashirikiana na wadau katika sekta ya kilimo kwa kumkopesha mkulima ili apunguze gharama za upatikanaji pembejeo.

Chacha alisisitiza umuhimu wa kuwapo uaminifu zaidi miongoni mwa taasisi na wadau mbalimbali wanaojihusisha moja kwa moja katika sekta ya kilimo ili kuchochea maendeleo na ukuaji wake.

Naye Mkurugenzi wa TARI Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema makubaliano hayo yatasaidia kuondoa changamoto mbalimbali ambazo wakulima wamekuwa wakikabiliana nazo kwa muda mrefu bila kupata suluhu yake.

"Kwa kawaida pH inayotakiwa ni 6.5 hadi 7 lakini katika maeneo mengi ya Kanda za Nyanda za Juu Kusini tindikali imepungua mpaka kufikia pH 4.2 hadi 5.3 hali hiyo inasababisha kupungua kwa uzalishaji, hivyo makubaliano haya ya maana kubwa katika kuinua uzalishaji," alisema Dk. Bucheyeki.

YARA Tanzania kwa kushirikiana na wadau wengine imekuwa mstari wa mbele kuhamasisha upimaji wa afya ya udongo kama njia muhimu ya kumsaidia mkulima kupata mafanikio katika kilimo.

# Tigo yazawadia mawakala bora

**Na Mwandishi wetu**

KAMPUNI ya Tigo Tanzania, imetoa zawadi ya Sh. milioni 60 kwa mawakala waliofanya vizuri katika promosheni ya mwisho wa mwaka 2018 ya Wakala Chief Promosheni.

Akizungumza wakati wa kukabidhi fedha kwa washindi hao, Mkuu wa Huduma za kifedha wa Tigo, Hussein Sayed, alisema wakala aliyefanya vizuri zaidi ni Vicky Ibrahimu, ambaye alipewa zawadi ya Sh. milioni 20.

Aidha, alisema washindi wengine wamejishindia Sh. milioni 40 kwenye viwango tofauti tofauti, na promosheni hiyo imewekwa maalum kwa ajili ya kuwashukuru na kuwazawadia wanaofanya vizuri katika kipindi cha mwisho wa mwaka.

Hussein alisema washindi 20 kutoka kanda nne ambazo ni Pwani, Kusini, Kaskazini na Kanda ya Ziwa walipatikana na kila kanda ilitoa washindi watano ambao kila mmoja alijinyakulia zawadi ya Sh. milioni 2.

"Jumla ya mawakala 90,000 walishiriki promosheni hii nchi nzima iliyoanza Desemba mosi na kumalizika Desemba 31, mwaka 2018," alisema.

Naye, Mkuu wa Bidhaa Huduma za kifedha kwa njia ya simu, James Sumari, alisema mawakala wa Tigo wamewezesha huduma za kifedha kufika kwa Watanzania wengi hadi vijiji na hivyo kurahisisha huduma za kifedha.

Naye, Mshindi wa jumla wa promosheni hiyo, Ibrahimu, akizungumza mara baada ya kukabidhiwa hundi ya mfano, alisema fedha alizojishindia zitamsaidia kupanua biashara yake katika jiji la Dar es Salaam.

# Msako wakamata 71 kwa tuhuma za uhamiaji haramu

**Na Gurian Adolf,** NKASI

IDARA ya Uhamiaji mkoani Rukwa imewakamata wahamiaji haramu 71, walioingia nchini na kuishi katika vijiji vilivyopo mwambao wa Ziwa Tanganyika.

Pia imewakamata watu wanaodaiwa kuwa ni mawakala wanaofanya kazi ya kuwapokea wahamiaji hao na kuwaingiza nchini bila kuzingatia sheria za uhamiaji.

Naibu Kamishna wa Uhamiaji wa Mkoa, Elizius Mushongi, alisema kuwa wahamiaji hao haramu ni kutokana na msako maalum unaofanyika katika vijiji vitatu vilivyopo katika Tarafa ya Wampembe.

Alisema watu hao wamekuwa wakiishi katika vijiji hivyo, ambapo walikuwa wakijishughulisha na shughuli za uvuvi, na kwamba waliingia nchini kinyume cha taratibu na kufanya shughuli hizo na pia bila kufuata sheria za nchi.

Alivitaja vijiji ambapo maofisa uhamiaji wamefanya msako ni Msamba, Lupata na Kasanga ndogo vilivyoko mwambao wa ziwa ambavyo wakazi wengi wa vijiji hivyo ni wavuvi.

Alisema kati ya wahamiaji hao 14 wamefukuzwa nchini na kurudi kwao kutokana na kuwa wagonjwa na wengine kuwa na watoto wachanga.

Kwa upande wake Ofisa Uhamiaji Wilaya ya Nkasi, Josephat Bulale, alisema licha ya changamoto ya vitendea kazi katika msako wa kukamata wahamiaji haramu zoezi hilo litakuwa endelevu.

# Waajiri watakiwa kuwahisha michango mifumo ya jamii

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Jenister Mhagama, ameitaka mifuko yote ya hifadhi ya jamii kuhakikisha kuwa waajiri wanafikisha michango ya wafanyakazi katika mifuko hiyo baada ya kuwakata katika mishahara yao.

Mhagama alisema hayo bungeni jana, alipokuwa akitoa jibu la nyongeza kwa Mbunge wa Viti Maalum, Catherine Magige (CCM), ambaye alitaka kujua ni lini serikali itawalipa wafanyakazi 545 wa Kilitex-Arusha na wale wa hoteli ya Sabasaba ambao bado wanadai pensheni baada ya mwajiri wao kutowasilisha michango yao kwenye mfuko wa PPF.

Alisema bado tatizo la malipo ya pensheni kwa wafanyakazi ni tatizo kutokana na baadhi ya waajiri kutofikisha michango ya wafanyakazi kwenye mifuko kwa wakati.

"Ni muhimu kuhakikisha kuwa michango inafika kwa wakati ili kuondoa adha hii katika taifa letu," alisema.

Akizungumzia suala la wafanyakazi wa KILTEX na wa hoteli ya Sabasaba ambao wafanyakazi wake hawalipwa pensheni, Mhagama aliwataka viongozi watendaji wa mifuko inayohusika na wafanyakazi hao kukaa pamoja kutatua tatizo hilo.

Awali akijibu swali la msingi la mbunge huyo, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Ashatu Kijaji, alisema kwa mujibu wa kumbukumbu na nyaraka zilizoko na taratibu za ufilisi ulikamilika na wafanyakazi wa KILTEX walilipwa stahili zao.

Kijaji alisema hata hivyo, baadhi ya wafanyakazi walilipwa mafao yao ya kiinua mgongo kwa mkupuo na wengine walirejeshewa michango yao kadri walivyochangia.

Alisema utaratibu huo wa malipo ulifanyika baada ya mfilisi kushindwa kulipa riba, adhabu na malimbikizo ya michango kwenye mfuko wa pensheni wa PPF.

"Uamuzi huo ulifikiwa kutokana na ukweli kwamba, mauzo ya mali za kiwanda yalikuwa ni madogo ikilinganishwa na jumla ya madai na gharama halisi za ufilisi," alisema.

Kijaji alisema watumishi wa Kiwanda cha KILTEX walilipwa stahili zao kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni namba 46 ya mwaka 1931, ambayo ilitumika kufilisi kiwanda mwaka 1995.

Alisema kwa mujibu wa sheria hiyo, mfilisi alitakiwa kuuza mali za kiwanda na kutumia fedha za mauzo kulipa madai mbalimbali, ikiwa ni pamoja na stahili za watumishi ndani ya muda maalum kulingana na tangazo la ufilisi.

Alisema kufuatia tangazo la mfilisi kwenye vyombo vya habari, wadai waliwasilisha madai yao na mfilisi alilipa madeni hayo kulingana na fedha za mauzo zilizopatikana.




**Habari zote na Godfrey Mushi,** DODOMA



Kamishna Jenerali wa Magereza, Phaustine Kasike, akisaini kitabu cha ukaguzi katika ujenzi wa Ofisi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi Stadi na Ofisi ya Waziri Mkuu, Ajira, Vijana na Walemavu, jana jijini Dodoma. **PICHA:MAGEREZA**

# Walimu waonywa matumizi ya viboko

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

WALIMU wametakiwa kufuata sheria na taratibu katika kutoa adhabu ya viboko na yeyote atakayetoa adhabu hiyo kinyume cha sheria iliyowekwa atachukuliwa hatua ya kinidhamu.

Onyo hilo lilitolewa jana na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, alipokuwa akitoa jibu la nyongeza bungeni kuhusu utoaji wa adhabu hiyo shuleni.

Alisema utoaji wa adhabu hiyo haina lengo la kuongeza ufaulu ila ni moja ya taratibu za kuwafanya wanafunzi kufuata taratibu za shule.

"Nawaomba nao wanafunzi kufuata taratibu bila shuruti, ili kuepukana na adhabu hiyo ambayo inaweza kuepukika," alisema.

Awali akijibu swali la msingi la Zainab Katimba, Naibu Waziri wa Wizara hiyo, William Ole Nasha, alisema adhabu ya viboko hutumika pale mwanafunzi anapofanya vitendo vya utovu wa kinidhamu uliokithiri na utolewa kwa utaratibu maalum.

Alisema kanuni ya 3(I) ya Sheria ya Elimu, Sura ya 353 marejeo ya mwaka 2002, inasema adhabu ya viboko itatolewa endapo patatokea utovu mkubwa wa nidhamu.

"Makosa haya yanaweza kutokea ndani au nje ya shule ambayo yatashusha heshima ya shule, lakini lazima sheria na taratibu za adhabu hiyo zifuatwe," alisema.

Nasha alisema waraka wa elimu namba 24 wa mwaka 2002, unaelekeza kuwa adhabu ya viboko itatolewa na Mwalimu Mkuu au aliyeteuliwa kwa kuzingatia ukubwa wa kosa, jinsi, afya ya mtoto na isizidi viboko vinne kwa wakati mmoja.

"Hivyo serikali itaendelea kusisitiza matumizi sahihi ya adhabu kwa wanafunzi, ili kuleta tija katika ufundishaji na ujifunzaji," alisema.

Aidha, naibu huyo alisema kumekuwa na tafiti mbalimbali zilizofanywa kuhusiana na adhabu hiyo ya viboko duniani.

Alisema utafiti uliofanywa na Hamza Nampoto wa mwaka 2018 unakubaliana na adhabu ya viboko kama njia ya kudumisha nidhamu na hatimaye kuongeza ushiriki wa wanafunzi katika ujifunzaji.

Alisema hata hivyo, utafiti uliofanywa na Maria Jose Oganda na Kimly Pelis mwaka 2015 Ethiopia, India, Peru, na Vietnam, unasema adhabu ya viboko haina tija na usababisha madhara ya kisaikolojia na kimwili kwa wanafunzi.

Aidha, alisema utafiti uliofanywa na Lomasontfo Dlamini na wenzake 2018 (Swaziland) na Yusuph Maulid Kambunga na wenzake (2018) unasema adhabu ya viboko inaweza kutumika pamoja na njia nyingine ili kudhibiti nidhamu kwa wanafunzi kwa lengo la kuongeza kiwango cha ufaulu shuleni.

## Diaspora sasa kutambuliwa

WIZARA ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, imekamilisha kuandaa Sera ya Mambo ya Nje, ambapo pamoja na mambo mengine imeangalia namna ya kuwatambua na kuwajumuisha diaspora kwenye juhudi za kuleta maendeleo ya taifa.

Hayo yameelezwa na Naibu Waziri wa wizara hiyo, Dk. Damas Ndumbaro, wakati akijibu swali la msingi lililoulizwa na Mbunge wa Gando (CUF), Othumn Omari Haji, aliyetaka kujua mpango wa serikali wa kuandaa sera mpya ya mambo ya nje ukoje. "Moja kati ya malengo makuu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ya mwaka 2017/2018, ilikuwa ni kukamilisha kuandaa sera mpya ya mambo ya nje, je, mpango huo umefikia wapi? Je, ni maeneo gani mapya ya kisera?" Alihoji.

Dk. Ndumbaro alisema wizara yake imekamilisha uandaaji wa Rasimu ya Sera ya Mambo ya Nje kama ilivyopendekezwa na wadau wakati wa kufanya tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje ya mwaka 2001.

"Rasimu hiyo ya sera hivi sasa iko katika hatua ya kusambazwa kwa wadau mbalimbali kama vile wizara, idara na taasisi za serikali, sekta binafsi na Taasisi zisizo za kiserikali, ili kupata maoni yanayolenga kuboresha zaidi," alisema.

Aidha, Dk. Ndumbaro, alisema maeneo mapya ambayo yamejumuisha katika sera iliyopendekezwa ni pamoja na kutambua na kuwajumuisha diaspora kwenye juhudi za kuleta maendeleo ya taifa, kutambua mihimili mingine kama wadau wa sera (Bunge na Mahakama) na kuzingatia mikakati na mipango ya muda mrefu ya nchi na Jumuiya za Kikanda na Kimataifa.

Alisema maeneo mengine ni utekelezaji wa sera kufikia hadi ngazi ya wilaya na mikoa, vijana na tasnia ya michezo na burudani kutumika kama njia ya kuitangaza Tanzania nje.

"Aidha, rasimu ya sera inaelekeza nchi kuimarisha uhusiano na nchi nyingine yanayolenga kukuza uchumi wa nchi kwa kuzingatia mipango ya muda mfupi na mirefu ya serikali." Aidha, katika swali la nyongeza, Haji, alitaka kujua sera ya Tanzania ya ukombozi kwa nchi ambazo bado hazijapata uhuru kama Sahara Magharibi na Palestina.

Alisema Tanzania imejijengea heshima kubwa sana kwa sera yake ya ukombozi katika nchi za Afrika na kusisitiza kuwa heshima hiyo bado iko, kwa sababu bado sera ya Tanzania kwa ukoloni wa kutawala nchi yoyote uko pale pale.

# Marais wa EAC kukutana Arusha leo kuhudhuria mkutano wa 20

**Na Mwandishi Wetu,**
ARUSHA

MKUTANO wa 20 wa wakuu wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), unatarajiwa kuanza leo Arusha ambako ni makao makuu ya jumuiya hiyo.

Mkutano huo unafanyika baada ya mkutano kama huo kuahirishwa mara mbili Novemba 30 na Desemba 27, mwaka jana.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Rais Yoweri Museveni, alisema kuahirishwa kwa mkutano wa Novemba 30, kulitokana na Rais wa Burundi au mwakilishi wake kushindwa kuhudhuria kikao hicho.

"Tuliahirisha mkutano mpaka 27 Desemba, 2018, wakati sisi wote tutakapokuwapo kwa sababu mkataba wa Afrika Mashariki unasema mambo mawili, moja lazima tuwe na mkutano mmoja wa kawaida kila mwaka," alisema.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mkuu wa Idara ya Mawasiliano ya Sekretarieti ya Afrika Mashariki, Owora Richard Othieno, mkutano wa leo ulitanguliwa na mkutano wa 38 usio wa kawaida wa mawaziri wa Afrika Mashariki pamoja na vikao vya makatibu wakuu wa wizara vilivyomalizika juzi.



Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Annamringi Macha, akimbebesha gogo mmoja wa wachimbaji wadogo wa mgodi wa dhahabu wa Nyagalata Kata ya Lunguya, katika Halmashauri ya Msalala, kwa ajili ya kutengeneza njia ya kuingia chini ya mgodi huo kwenda kuwaokoa wachimbaji watatu walisadikiwa kufukiwa na kifusi. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Walimu 600 wapata mafunzo ya vitendo

**Na Cynthia Mwilolezi**,
ARUSHA

SERIKALI imelipongeza shirika lisilo la kiserikali la Helvetas kwa kushirikiana na Chama cha Walimu nchini, (CWT), kupitia mradi wa uboreshaji elimu kwa mfumo wa Queets na kuwezesha walimu zaidi ya 600 kupata mafunzo ya ufundishaji wa vitendo kwa wanafunzi ili kuongeza ufaulu.

Mkurugenzi Msaidizi wa Elimu Msingi kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Dk. George Jidanva, alisema mafunzo hayo yanasaidia kujenga msingi imara kwa wanafunzi ambao baadaye wataweza kujenga Tanzania ya viwanda.

Aliwataka walimu wanaopata mafunzo hayo kutoka mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara, kuhakikisha wanafundisha wenzao waliokosa fursa hiyo ili kueneza mbinu walizopata kwa walimu wengi zaidi.

Dk. Jidanva alisema mafunzo hayo yanatolewa wakati mwafaka wakati serikali ikiandaa mpango mkakati kuhakikisha walimu wanapatiwa mafunzo kazini ambayo yatawasaidia kupanda kwa madaraja.

"Nawapongeza mliobuni mafunzo haya sababu serikali tupo katika maandalizi ya kutoa mafunzo kazini na kila mwalimu atatakiwa kupata au kujiendeleza, ili apate haki ya kupanda daraja na kuachana na utaratibu wa zamani wa kupandisha walimu madaraja kwa mazoea, pia tutaangalia ujazaji wa mfumo wa Opras na mafunzo ya muhusika," alisema.

Alisema lengo la mafunzo hayo ni kujenga umahiri wa ufundishaji na kuachana na mazoea ya siku za nyuma ya kufundisha kwa kukariri.

Aidh, aliwaagiza walimu kuacha kusoma vitabu wanavyopatiwa kazini ili waongeze maarifa na kuwaonya kuacha tabia ya kuhama navyo vitabu hivyo. "Mnapohama acheni vitabu shule husika na mkienda shule nyingine mtavikuta huko, lakini nataka pia mfahamu serikali tunaboresha mfumo wa uhamisho siku za usoni, mtatumia mfumo wa elektroniki kuhama, ili unapotaka kuhama unaangalia katika mtandao shule isiyo na walimu wengi ndio itafunguka utajaza nafasi, lengo ni kupunguza mrundikano shule za mjini," alisema.

Pia aliwataka kushirikisha kamati za shule na wazazi kuhakikisha watoto wanapata chakula cha mchana shuleni ili kuongeza ufaulu.

Naye Mwakilishi wa Katibu Mkuu CWT, Reginald Christoncia, alisema mpango wa SITT umebadilisha walimu na kupenda kufundisha masomo ya Kiingereza, Hesabu na Sayansi ya Mazingira ambao ndio walegwa wa mpango huo, huku pia wanafunzi wakiongeza ufaulu. Aliomba serikali kuangalia wakati wa uhamisho kutohamisha walimu waliopata mafunzo hayo, ili kutoharibu mpango huo kwa sababu kila shule inapatiwa walimu watatu wa masomo hayo.

Meneja Mradi wa Shirika la Helvetas, Donatioan Marusa, alisema mpango huo tayari umenufaisha shule zaidi ya shule 1,800 kutoka mikoa hiyo mitatu iliopo kwenye mradi wa Queets kupitia mpango wa SITT.

## Kamati ya RC yaibua mazito mauaji ya twiga

**Na Allan Isack,** ARUSHA

TAARIFA ya kamati ya uchunguzi wa mauaji ya wanyamapori, iliyoundwa na Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, kuhusu mauaji ya twiga wilayani Longido, imeitaja kampuni ya uwindaji kuhusika na ujangili katika eneo hilo.

Wengine waliotajwa ni wakuu wa vituo vya polisi vya Namanga na Longido, ambao wanalalamikiwa kushiriki vitendo vya ujangili na kutokutoa ushirikiano kwa kamati.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake wakati akisoma taarifa ya kamati hiyo jana, Gambo, alisema kamati imependekeza kwa Waziri wa Maliasili na Utalii, kuunda timu ya uchunguzi kuhusu tuhuma na malalamiko dhidi ya kampuni ya Green Mile Safari Ltd na wengine.

Alisema mapendekezo hayo yanashauri kuratibu, kuendesha mashtaka na upelelezi na uendeshaji wa kesi za ujangili kwa mujibu wa sheria.

Aidha, Gambo alitoa pendekezo kwa Wizara ya Maliasili na Utalii kuwachukulia hatua kali za kisheria Ofisa Wanyamapori wa Wilaya ya Longido na Ofisa wa Kikosi cha Kuzuia Ujangili Kanda ya Arusha, kutokana na kutokutoa taarifa sahihi za ujangili na kushindwa kusimamia uratibu katika kufanya doria kwenye vitalu vyao.

"Mkuu wa kituo cha Longido aliitwa na kamati kujieleza, lakini alikataa kwenda na alisema yeye hawezi kwenda kuhojiwa mbele ya kamati iliyoundwa na mkuu wa mkoa mpaka apate maelekezo kutoka kwa wakubwa wake," alisema Gambo.

Kaimu Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Arusha, Longingus Tibishumbwamu, alithibitisha kuwashikilia watuhumiwa watano kwa kosa la kujihusisha na matukio ya ujangili. Alisema kutokana na mahojiano yaliyofanywa na kamati hiyo kwa kuwahusisha watu mbalimbali kampuni hiyo imetuhumiwa kuhusika na ujangili wa wanyamapori wakiwamo twiga.

Aidha, alisema kamati ilipokea taarifa ya watu 25, wanaotajwa kuhusika na masuala ya ujangili wilayani Longido na kati ya hao, watano wanashikiliwa na Jeshi la Polisi na watuhumiwa wangine walipoona uchunguzi umeanza wamekimbilia nchi ya Kenya.

"Baadhi ya watu walioitwa mbele ya kamati kwa mahojiano hawakuweza kupatikana, hivyo kamati inawataka wawekezaji wote na wamiliki wa vitalu kufika mbele ya kamati kwa mahojiano," alisema.

Akifafanua alisema, taarifa ya kamati hiyo kwa kipindi cha miaka miwili imeonyesha twiga 35, wamekufa kutokana na mazingira tofauti, lakini twiga 25, wameuawa kwa ujangili na wengine walikufa kwa kugongwa na magari, kupigwa shoti ya umeme na kuanguka kwenye makorongo.

# Waomba mitaala kufundisha lugha za alama

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

BAADHI ya wanafunzi wanaosoma Chuo cha Ustawi wa Jamii Kisangara, wilayani Mwanga mkoani Kilimanjaro, wameiomba Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuanzisha mitaala maalumu ya lugha za alama kwa maofisa hao, ili waweze kuwahudumia watu wenye ulemavu.

Akizungunza na Nipashe kwa niaba ya wenzake, Emakulata Kilama, alisema wamebaini changamoto hizo baada ya kwenda katika mazoezi ya vitendo katika taasisi mbalimbali hapa nchini.

Alisema kukosekana kwa lugha hizo za alama kumekuwa changamoto kwa maofisa hao na watendaji wengine kwa kuwa wanashindwa kuwaelewa wateja wao wanapofika ofisi zao.

“Unaweza kukuta mteja kafanyiwa unyanyasaji, lakini tunashindwa kumwelewa kutokana na sisi hatujui lugha za alama ... tunaiomba serikali kuangalia uwezekano wa kuanzisha mitaala maalumu, ili kuweza kutokomeza ukandamizaji wa haki kwa watu wenye ulemavu,” alisema Emakulata.

Ester Samson alisema iko haja kwa wizara kukaa na kuona namna bora ya kuandaa mitaala itakayofundishwa katika ngazi zote za elimu, ili kuhakikisha tunawatendea haki watu wenye ulemavu hapa nchini.

“Sisi kama watendaji tunaowahudumia wananchi moja kwa moja, tunakabiliwa na changamoto za kushindwa kuwaelewa wateja, hivyo tunaomba kupata mafunzo ya alama ili kuweza kuwahudumia,” alisema Ester.



Mkurugenzi wa Fedha wa Benki ya Biashara ya DCB, Zacharia Kapama (wa pili kushoto), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam. Wengine kutoka kushoto ni Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Mawasiliano, Rahma Ngassa, Mkurugenzi wa Biashara, James Ngaluko na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Ndani, Deogratius Thadei. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TRA yakunjua makucha, yadaka mali za magendo

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

MAMLAKA ya Mapato nchini (TRA), Mkoa wa Kilimanjaro, imekamata bidhaa zilizoingizwa nchini bila kibali (magendo), zenye thamani ya Sh. milioni 171.56, huku ikishikilia magari manane na pikipiki 12 kwa kusafirisha bidhaa hizo.

Hayo yalisemwa jana na Meneja Msaidizi wa mamlaka hiyo mkoa, anayeshughulikia masuala ya forodha, Edwin Iwato, alipozungumza na waandishi wa habari ambapo alisema kuwa, kwa sasa biashara ya magendo imepungua kwa kasi kubwa kutokana na kuwapo kwa vikosi vya doria katika maeneo ya mpakani mwa Tanzania na Kenya.

Alisema katika kipindi cha kati ya Julai hadi Desemba mwaka jana, bidhaa za magendo zenye thamani ya Sh. milioni 171.56 zilikamatwa.

Aidha, alisema Sh. milioni 45.37 zilikusanywa kama faini zilizotozwa kwa bidhaa ambazo hazikukidhi viwango vya ubora na usalama, huku Sh. milioni . 27.15 zilikusanywa kama kodi.

“Kwa sasa wafanyabiashara wameshaanza kutambua kuwa kuingiza bidhaa nchini bila kufuata utaratibu ni kosa kisheria na pindi utakapokamatwa bidhaa zinataifishwa pamoja na chombo cha usafiri kilichotumika kusafirishia, hali ambayo imesababisha biashara hii kupungua, ” alisema Iwato.

Kwa upande wake, Meneja wa TRA Mkoa wa Kilimanjaro, Msafiri Mbibo, alitumia nafasi hiyo kuwataka wamiliki wa vyombo vya moto kutoruhusu kubeba bidhaa za magendo, kwa kuwa vikikamatwa hutaifishwa na kuuzwa kwa mnada au hutolewa bure kwa taasisi za serikali.

Mbibo alisema kuwa, mamlaka hiyo itaendelea na operesheni maalum ya kuwatafuta watu wote wanaofanya shughuli za magendo, kwa kuwa wamekuwa wakichangia kuzorotesha uchumi wa nchi kwa kuviua viwanda vya ndani.

“Kwa sasa tumeimarisha vituo vya boda ya Holili na Tarakea, ili kuhakikisha hakuna bidhaa zisizo salama zinapita na bidhaa zitakazoingia nchini pasipokuwa na nyaraka za uingizwaji tutazikamata,” alisema Mbibo.

# Wafanyabiashara waomba kuboreshewa usafi

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

WAFANYABIASHARA wa soko la Sanya Juu Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, wameomba halmashauri hiyo kuboresha suala la usafi wa eneo hilo ili iweze kupata mapato zaidi Ester Maro, mfanyabiashara wa mazao ya mboga katika soko hilo aliambia Nipashe kuwa bado miundombinu ya eneo hilo siyo rafiki licha halmashauri kukusanya mapato mara kwa mara. “Imefika mahali sasa uongozi wa wilaya hiyo, kufanyia ukarabati miundombinu ya soko hilo... tuondokane na kero tunazopata hasa za uwepo wa uchakavu wa vyoo, ukosefu wa vizimba jambo linalohatarisha usalama wa afya za watumiaji wa soko,” alisema Ester.

Cecilia John alisema Wilaya ya Siha chini ya Mkurugenzi wake, Valerian Juwal, hawapo tayari kutekeleza sera ya uchumi wa viwanda kwa vitendo kwa kuwa wanashindwa kuboresha vyanzo vya mapato na badala yake kuendeleza siasa za chuki katika Baraza la Madiwani. “Hali ya soko la Sanya Juu bado ni mbaya ... hasa katika upande wa miundombinu ... tunaomba mkurugenzi kuangalia uwezekano wa kutenga bajeti kwa ajili yetu ili kuweka mazingira bora ya wafanyabiashara,” alisema Cecilia. Abeid Abdalla alisema kuwa soko hilo ni moja kati ya masoko ambayo yakiboreshwa vyema yanaweza kuwasaidia wakulima wanaotoa mboga shambani pamoja na wauzaji wa nafaka.

Akizungumzia hali ya ukusanyaji mapato kwa Halmashauri ya Wilaya ya Siha, Mkurugenzi Mtendaji wa wilaya hiyo, Valerian Juwal, alisema kuwa wapo katika hatua za kufanya marekebisho katika soko hilo na kuwataka wafanyabiashara kuwa watulivu.

“Tutaboresha ukusanyaji wa mapato na kuboresha miundominu mbalimbali inayochangia kuongeza upatikanaji wa mapato,”alisema mkurugenzi.


Ukurasa 19

Siku Waziri Mgalu alipowasha taa ya historia kijijini


Ukurasa 14

Hifadhi Ruaha katika staili mpya, utalii kutoka angani kwenye puto



## Boti iliyotengenezwa kwa mabaki ya plastiki kufanya safari ya kihistoria

Ukurasa 15


# BUFE

Ijumaa Februari 1, 2019

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA




# PRISCA Muuguzi mtarajiwa aliyejikuta anaangukia kuomba mitaani

**Na Elizabeth Zaya**

HAO ni watoto kama walivyo wengine, lakini kundi hili linaonekana 'limezirwa' au kusahaulika. Huenda ni matokeo ya mambo ambayo aidha yanatokana na tabia zao watoto wenyewe, au mtazamo uliopo katika jamii.

Baada ya kusahaulika kutoka katika jamii zao, wamebatizwa jina 'watoto wa mitaani,' ingawa ukweli unabaki si jina sahihi au wanayostahili kuitwa. Tafsiri yake ya awali, ni wanaoangukia lindi la umasikini.

Tasfiri ya utetezi kwa vijana hao, inaanzia uhalisia kwamba kuna ukweli wana mahali walikozaliwa, kama ilivyo kwa watoto wengine, wakiwa na ama wazazi; baba na mama au walezi.

Uzoefu unabainisha kuwapo maisha hayo kwa wengi, ni matokeo ya kadhia ya ama kufiwa na wazazi au wazazi

INAENDELEA UK.16

UCHUMI

## Habari katika picha


Ukurasa 17

KIUCHUMI ZAIDI Ukurasa 19

Umuhimu wa Muda kwenye Biashara Ukurasa 20

Muhtasari wa Soko

**Biashara**

Jumla ya Mauzo (bln) 22,136.24

Mauzo 109,584,255.00
Hisa 58,317

**Kielezo**

| | | |
|---|---|---|
| TSI | 4,207.58 | +0.00 |
| DSEI | 2,296.50 | -37.11 |

**ZILIZOPANDA**

| KAMPUNI | Bei | Badiliko% |
|---|---|---|
| KA | 180 | -2.70% |
| JHL | 9,500 | +1.06% |
| SWIS | 3,760 | +7.43% |
| EABL | 5,320 | -1.66% |

**ZILIZOSHUKA**

| KAMPUNI | Bei | Badiliko% |
|---|---|---|
| TCCL | 1,200 | -11.76% |
| ACA | 5,550 | -2.63% |
| NMB | 1400 | -1.41% |
| NMG | 2,510 | -1.57% |
| KCB | 840 | +2.44% |

BIASHARA

# Hifadhi Ruaha katika staili utalii kutoka angani kweny

• Marubani wake wana leseni za kimataifa

**Na Beatrice Shayo,** aliyekuwa Iringa



Hivi ndivyo unavyofanyika utalii wa maputo katika Hifadhi ya Taifa Ruaha, mkoani Iringa. **PICHA: MTANDAO.**

KATIKA Hifadhi ya Taifa Ruaha, mkoani Iringa, kama vilivyo vivutio vinginevyo vya kitalii, ni kawaida yake kuwa na utaratibu wake, watalii wanazungushwa na magari kushuhudia vilivyoko, yakiwamo makundi makubwa ya wanyama kama tembo.

Sasa katika hatua ya 'kujiongeza,' watalii hao wamekuja na jingine la ziada la kuwawezesha watalii kuruka angani wakitumia puto maalumu, jambo ambalo sasa ni kivutoa kikubwa kwa watalii.

Inaelezwa kwamba, Ruaha inayoongoza kwa ukubwa Tanzania na Afrika Mashariki, ikilinganishwa na nyingine. Ina ukubwa wa kilomita za mraba 20,226.

Mbali na kuwapo wanyama hao wanaonekana kwa urahisi hifadhini, katika eneo hilo lenye uoto wa mimea upande wa Kaskazini mwa Afrika, inayokutana na uoto wa mimea Kusini mwa Afrika. Ni sifa inayochangia kuwa na aina nyingi ya mimea na wanyama.

**UTALII WA PUTO**

Ofisa Utalii na Masoko katika Hifadhi ya Ruaha, Antipas Mgumgusi, anasema hifadhi hiyo ina wanyama wengi na haihitaji mwendo mrefu kuwaona wanyama.

Anasema utalii wa kuruka na puto, ambao hupanda juu wa kikapu na kurushwa angani, ni huduma iliyoanza mwaka jana na inazidi kupata umaarufu kwa kupendwa.

"Mazingira ya Ruaha ni mazuri, ikilinganisha na mazingira mengine, wakafikiria utalii wa aina hii kuuleta hapa hifadhini," anasema Mgungusi na kuongeza: "Sisi tumeupokea vizuri na tunautangaza tunatarajia idadi ya wanaoruka kwenda angani kuongezeka siku hadi siku."

Anausifu utalii huo wa maputo ni mzuri, kwani unamwezesha mtalii kuwaona wanyama mbalimbali kutoka umbali mrefu.

Ofisa Masoko huyo anafafanua kuwa, mtu akiwa angani ana tofauti na aliye chini, kwa maana ya

> **"Rubani akiona mnyama, anaweza kushusha puto kwa kiwango fulani na kuona kwa ukaribu, kwani anajua jinsi ya kuchezesha chombo hicho vizuri na mtalii kufurahia.**

kuwa kuna miti inayoziba asimuone mnyama vizuri, kuliganisha na aliyepo angani.

Mgungusi anasema, utalii wa puto una uwezo wa kuona wanyama kwa karibu zaidi, kwa sababu wataalamu wana uwezo wa kuchezesha na kufurahia aina ya utalii huo.

"Rubani akiona mnyama, anaweza kushusha puto kwa kiwango fulani na kuona kwa ukaribu, kwani anajua jinsi ya kuchezesha chombo hicho vizuri na mtalii kufurahia," anasema

Mgungusi anasema, puto hilo lina uwezo wa kubeba watu 12 na kuna nyingine zenye uwezo mkubwa, ila katika hifadhi hiyo wameanza na yenye uwezo huo.



Ofisa Utalii na Masoko katika Hifadhi ya Ruaha, Antipas Mgumgusi.



Mkuu wa Kanda ya Utalii Mk inga, Tully Kulanga. **PICHA Z TRICE SHAYO.**

UCHUMI

**Muuguzi mtarajiwa aliyejikuta anaangukia kuomba mitaani**

Ukurasa 16

UCHUMI

**Boti iliyotengenezwa kwa mabaki ya plastiki kufanya safari ya kihistoria**


Ukurasa 15

BIASHARA

**Siku Waziri Mgalu alipowasha taa ya historia kijijini Kisarawe**

Ukurasa 19

# mpya, ...e puto





...koa wa Ir- ...OTE: BEA-

Anasema wastani wa kuzunguka angani ni saa moja na endapo mtalii akihitaji muda zaidi, anaongezewa. Ofisa huyo anafafanua:

"Anayeendesha chombo hicho ni rubani, ana utaalamu amepewa cheti cha kimataifa cha urushaji wa vyombo vya anga, kwani kuna waliosomea masuala hayo nje ya nchi na kwa hapa hifadhini, Mtanzania ndiye anarusha angani puto."

Kutoka na hilo, Mgungusi anawahakikishia abiria usalama wa chombo, kwani kinaendeshwa na wataalamu wabobezi wa puto.

Mgungusi, anataja namna nyinginezo za usafiri wa kitaalii ni wa kutumia magari; kutembea kwa miguu wakiongozwa na askari; na utalii wa ndege.

Anasema wapo katika mchakato wa kuanzisha utalii wa boti, utakofanyika mtoni katika eneo la Usangu, ikitarajiwa hadi mwakani huduma hiyo itakuwa imeshaanza.

**CHANGAMOTO**

Ofisa Masoko huyo, anataja changamoto zilizopo, ni uelewa duni wa umma kuhusiana na hifadhi za taifa na taratibu zake kwa wananchi.

"Watu wanawaza mambo ya utalii ni masuala ya Wazungu watoke nje ya nchi, lakini sisi kama hifadhi tunaendelea kupambana, ili kuwasaidia watu kuwapatia taarifa.

"Tuna kampeni nyingine ya nyumba kwa nyumba. tunaenda vyuoni, shuleni na taasisi, kuwaelimisha umuhimu wa kutembelea hifadhi," anasema.

Anakumbusha, iwapo Watanzania wengi wangewaeleza watu wengine kuhusiana na hifadhi za Tanzania au ya Ruaha aliko, ingewasaidia Watanzania wengi wasafiri nje ya nchi, hivyo mtu akiulizwa kuelezea Hifadhi ya Taifa Ruaha, bado anabaki kuwa na uwezo mdogo kueleza.

"Kama watu wengi wangekuwa na uelewa, ingetusaidia katika kupata soko kupitia biashara zao. Sisi ndio kilio chetu, kuhakikisha wananchi wanauelewa utalii na kutembelea vivutio vyao na utalii sio bei kubwa kama wanavyodhani," anasema

Mgungusi anasema kufika katika Hifadhi ya Ruaha, ni wastani wa saa tatu na umbali wa kilomita 130 kutoka mjini Iringa na kwa wenye vipato vya chini, wanaweza kujiunga kwenye vikundi vya familia, kirafiki, kazini , michezo na wakakodisha gari kwa gharama nafuu kufika Ruaha.

Anataja ada ya kiingilio ni Sh. 5,900 kwa mtu mzima na mtoto mwenye umri wa chini ya miaka 16 hadi mitano, anatozwa Sh. 2,000.

Mgungusi anasema, kuna huduma za malazi hifadhini, ikichukua watu zaidi ya 100 kwa mara moja na anaongeza: "Kuna huduma mbalimbali za kulala, kama kuna kikundi cha watu 50 wanatupatia taarifa.

"Kuna nyumba za kiasili, ambazo tumejenga kwa mfumo wa mapipa kwa nje na gharama yake ni Sh. 20,000; kwa hosteli kulala na Sh. 23,600 kwa mtu mmoja; na kuna nyumba ya familia ambayo ni Sh. 59,000."

**RC IRINGA**

Mkuu wa Mkoa, Ally Hapi, anasema Iringa ina vivutio vingi na kwa sasa wanafanya juhudi za kuvitangaza, ili kuongeza idadi ya utalii na kukuza uchumi wa mkoa kwa ujumla.

Anasema, kuna mradi wa kukuza utalii Kusini ambao unatarajiwa kupanua uwanja wa ndege kuwa wa kisasa na kuanza kupokea ndege kubwa kama Bombardier ya Shirika la Ndege Tanzania (ATCL).

"Katika huo mradi kutajengwa barabara ya lami kutoka Iringa hadi hifadhi ya Ruaha yenye kilometa 104, hii itakuwa ni sehemu ya mradi wa utalii wa Kusini na kutatua changamoto ya usafiri," anasema

Hapi anaeleza kwamba, kutajengwa Kituo cha Utalii cha Nyanda za Juu Kusini, kitachokuwapo mkoani Iringa, kwa ajili ya kufuatilia na kukuza sekta ya utalii.

"Sisi kama mkoa zipo juhudi ambazo tunazifanya kutangaza mkoa wetu. Bado tunakazi ya kufanya ya kuvitangaza vivutio vya mkoa wa Iringa ili viweze kujulikana ndani na nje ya nchi," anasema Hapi.

Anasema ifikapo Machi mwezi ujao, wataanza kupokea ndege za ATCL kutokana na maboresho walofanya katika uwanja wa ndege na itasaidia kuongeza utalii na kukuzauchumi.

Hapi anasema, wameshaanza kuukarabati uwanja wa ndege wa Iringa, kwa matarajio ya kupokea ndege kubwa na kwa sasa ndege zinazotua ni ndege ndogo na gharama zake ni kubwa, akitoa mfano mtu anayetoka kutalii mkoa wa Kilimanjaro, kuja Ruaha kunamgharimu Dola za Kimarekani 800 au si chini ya Sh. milioni 1.8.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Tungamalenga, kilichopo jirani na Hifadhi ya Taifa Ruaha, Fredrick Funzila, anasema wamekuwa wakiwaelimisha wenzao umuhimu wa kulinda hifadhi na kutembelea vivutio.

Pia, anasema wanashirikiana nao katika miradi ya maendeleo ya kijiji, kama vile ujenzi wa shule na zahanati.

**MRATIBU UTALII**

Mkuu wa Kanda ya Utalii mkoa wa Iringa, Tully Kulanga, anasema idara yao inasimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Utalii, inayolenga kukuza utalii endelevu.

Kulanga anataja jukumu lao lingine ni kubaini vivutio katika maeneo mbalimbali, wakishirikiana na mkoa husika, wakifanya kazi ya kuvitanagaza.

Anasema kumekuwapo changamoto ya barabara, ambayo wadau wa magari ya utalii wanalalamikia magari yao kuharibika na kutumia muda mrefu kufika hifadhini.

Kwa mujibu wa Kulanga, mbali na tatizo hilo, kuna walakini katika ukusanyaji takwimu za watalii wa ndani na anafafanua zaidi:

"Ukusanyaji takwimu kwa watalii wa nje ya nchi ni rahisi, kwa kuwa tunazipata katika viwanja vya ndege na mipaka ni kwa kushirikiana na Idara ya Uhamiaji .

"Watalii wa ndani, inaleta changamoto kwa sababu zile takwimu wanazichukua kwenye vivutio ambavyo huenda mgeni kaenda kutembelea, lakini utakuta mtu huyo huyo mmoja ametembelea Ruaha, Kalenga Isimila ukipata takwimu inakuwa inajiongeza mara mbili."

Anasema, kwa sasa Kitengo cha Takwimu cha Wizara ya Utalii, kinafanya utafiti kuona ni namna gani wataweza kuwahesabu watalii wa ndani bila kuwarudia.

## Boti iliyotengenezwa kwa mabaki ya plastiki kufanya safari ya kihistoria



BOTI ya asili iliyotengenezwa kwa kutumia mabaki ya plastiki yaliyokusanywa kutoka katika fukwe za Kenya, mwezi ujao inatarajiwa kufanya safari yake ya kwanza ikitokea kwenye mji wa Lamu kuelekea visiwani Zanzibar nchini Tanzania.

Boti hii itasafiri umbali wa kilometa zaidi ya 500 na itasimama katika visiwa kadhaa ili kueneza uwelewano kuhusu madhara yanayotokana na matumizi ya plastiki kwa bahari.

Kwa upande wake, Juliette Biao, Mkurugenzi wa Shirika la Umoja wa Mataifa kuhusu mazingira, ukanda wa pwani, anasema mpango huu wa kulinda mazingira ya bahari, unafaa kuigwa na mataifa mengine ulimwenguni.

Hassan Shafi, mmoja wa waliounda mashua hii, anasema kilichowavutia katika ubunifu huu ni takataka nyingi za plastiki ambazo zimekuwa zikipatikana katika mazingira ya bahari.

Mashua hiyo iliyoundwa na kikundi cha Plastic Revolution, ilitengenezwa Kisiwani Lamu, Kaskazini mwa pwani kwa kutumia plastiki na sasa iko safarini kuelekea visiwa vya Pemba na Zanzibar nchini Tanzania.

Katika siku chache zijazo, boti hiyo itaanza safari kuelekea Pemba na Zanzibar na kurejea ilipotoka ambapo mafundi watajaribu kutafakari zaidi kuhusu namna bora ya matumizi ya boti hiyo. (CHANZO: RFI Kiswahili).



Boti nyingine kama ya nchini Kenya, zilizotengenezwa kwa pastiki nchini. **PICHA: MTANDAO.**



**BEI YA MAZAO** >> MCHELE 182826.09/- | ULEZI 145750.00/- **FEDHA** >> RAND 168.31 | KSH 22.71 | USH 0.62

UCHUMI

# Muuguzi mtarajiwa aliyejikuta anaangukia kuomba mitaani

**Inatoka Uk.13**

• Baba kafa, mama akaugua, wakanitesa • Asimulia mimba, bangi, ubakaji wa mitaani • Hashawishiki, ndoto ya 'kutoka' palepale



Watoto ombaomba wakiwa katika nyendo zao katikati ya jiji la Dar es Salaam, anakopatikana Priska Kizito. **PICHA: MTANDAO**

wanapotengana, kukosa malezi bora au mikasa inayochangia wao kukimbilia mitaani kama mbadala wa kuishi.

**CHA KUJULIZA**

Cha kujiuliza, ni nani ajuaye wanakopita na wanayokutana nayo katika nyendo zao, ambako hawana wa kuwaongoza, kuwaelekeza na kuwaonya?

Inasadikiwa, huenda wanayokutana nayo mtaani, shida zao, uchanga wa akili zao na utoto, ndizo zinachangia kufikia hatua walizo nazo. Kwa sasa hawaelekezeki au kufundishika na jamii .

Upande wa pili, jamii imekata tamaa kuwasaidia na kuwarejesha katika hali zao, wakiachwa kuangukia hadhi ya 'kuzirwa.'

Kuna swali la jamii kujiuliza, wamethubutu kutenga hata siku moja kuwasikiliza na kufahamu sababu za wao kukimbilia mitaani kuomba misaada? Kama wapo, hatua gani zimechukuliwa?

Walikofikia watoto hao, wanakosa haki muhimu wanastahili kuzipata kijamii, pia kisheria.

**MKASA WA PRISKA**

Nipashe katika jijini Dar es Salaam, ilikutana na baadhi ya watoto wanaopita mitaani, ikiwadodosa kufahamu sababu za kufikia hatua hiyo, lakini wengi hawakuwa tayari kuzungumzia, isipokuwa Priska Kizito, mwenye umri miaka 17.

Akiwa na wenzake, Priska anaeleza maeneo yao wanakopita ni mitaa katikati ya jiji; Mnazi Mmoja na Kisutu, wakiwaomba wasamaria wema wawasaidie chochote, wapate mlo na mahitaji mengine madogo.

Priska anaeleza uzoefu wake, kwamba hakutarajia maishani wangejiunga na maisha hayo, jina lake kubadilika kuwa 'mtoto wa mitaani.'

Anatambulisha maisha yake kwamba anaishi na mama pekee, tangu baba yake alipofariki akiwa na umri wa miaka mitano, sasa imeshapita miaka 12.

Priska anasema, alipokuwa anasoma darasa la nne, mama yake alipatwa na maradhi hata akashindwa kumhudumia, ikiwamo kumpatia mahitaji ya shule, hivyo ikabidi apelekwe kwa bibi yake mkoani Dodoma, kuendelea na masomo.

"Nilisoma katika Shule ya Msingi Majani ya Chai, iliyopo Kipawa (Dar es Salaam) mpaka darasa la nne. Mama alianza kuugua sana

> **"**
> **Nilianza masomo kama kawaida katika shule ya msingi ya Pentagon hukohuko Dodoma, lakini nilipoingia darasa la tano, nilianza kupata visa vidogo vidogo kutoka kwa ndugu zangu.**

akashindwa kunihudumia, ndiyo akanihamishia kwa bibi Dodoma na kule nilikuwa naishi na ndugu wengine katika nyumba hiyo ya bibi akiwamo mama mdogo,"anasimulia Priska.

"Nilianza masomo kama kawaida katika shule ya msingi ya Pentagon hukohuko Dodoma, lakini nilipoingia darasa la tano, nilianza kupata visa vidogo vidogo kutoka kwa ndugu zangu niliokuwa naishi nao pale nyumbani kwa bibi lakini nilindelea kuvumilia."

Priska anasema, kadri siku zilivyosonga na visa vilikuwa vinaongezeka, akisingiziwa mengi ikiwemo 'kukomba mboga' na vitu vinavyopotea nyumbani, aliambiwa yeye mwizi.

Anasema alipokuwa darasa la sita, hali ilikuwa mbaya hata akapatwa na hisia za kupakimbia nyumbani, kwa sababu kuliongezeka vipigo kutoka kwa ndugu zake, akimtaja zaidi mama yake mdogo, aliyehusika na mipango yote ya nyumbani kwa bibi huyo, zikiwamo taratibu za chakula.

Priska anasema, hali ilifikia pabaya hata majirani waliamua kuingilia kati wakitaka nyumbani kuacha nyendo hizo za kumwonea mtoto huyo.

"Mimi kukaa kwa bibi hakukumfurahisha mama mdogo, kwa sababu kila siku alikuwa lazima anisingizie kwa chochote. Nilijitahidi kuvumilia, siku moja akaniita kabisa akaniambia wazi kwamba, lazima niondoke hapo nyumbani, la sivyo atakachonifanyia sitakisahau," anasema Priska

"Nilimwomba anisamehe, kama kuna jambo ninakosea, lakini alikuwa haelewi. Akaniambia, kama nataka anisamehe niondoke hapo nyumbani nirudi Dar es Salaam.

"Nikamwambia huko sina msaada, nitashindwa kusoma kwa sababu mama yangu hawezi kunihudumia, anaumwa," anasimulia Prisa, akisema baada ya mazungumzo hayo na mama mdogo, manyanyaso yalipungua.



Mwandishi wa Nipashe, akiwa katika picha ya pamoja na Prisca na mdogo wake, ambaye hakuwa tayari kumtaja jina. **NA MPIGAPICHA WETU.**

**WIZI NA UGANGA**

"Tuliendelea kuishi angalau nikajua labda ameacha, lakini kumbe alikuwa anatafuta njia ya kuniondoa pale. Siku moja nilirudi shuleni, kabla sijapumzika akaniita na kuanza kuniambia nirudishe pesa nilizochukua. Nilishtuka, nikasema sijui chochote ndipo akaanza kunipiga makofi.

"Mama mdogo aliendelea kunipiga huku akiwa anazungumza kwamba, ameibiwa Sh. 80,000 ambazo alitumiwa na mume wake kwa ajili ya kununulia mlango wa nyumba, lakini eti mimi ndiyo nimeingia ndani nikaiba. Nilisikitika sana na nililia sana," anaeleza

Priska anasimulia kwamba katika siku hiyo hakupewa hata chakula na kuambiwa kwamba, mpaka arudishe fedha anayodaiwa kuiba licha ya kwamba alijieleza kutoiba.

Anasema nyumbani hapo kwa bibi yake walikuwa wanaishi wengi, lakini alishangaa kuambiwa yeye ndiye aliyeiba. Priska anaendeleza simulizi: "Nilivyokataa kwamba sijaiba ile pesa, mama mdogo hakuridhika na akasema ananipeleka kwa mganga wa kienyeji kuagua na nikibainika tu atanifukuza nyumbani ama kuniua.

"Baada ya kunishinikiza na kuona ninaendelea kukataa, alinipeleka kweli kwa mganga wa kienyeji na wakati mganga anaendelea 'kusemasema' pale, akawa ananipiga. Lakini, mganga naye akamwambia atulie.

"Baadae nikasikia mganga anamwambia mama mdogo, kwamba anamwambia kwamba aliyechukua siyo mimi, hivyo akanichukua pale kwa hasira tukarudi nyumbani."

Priska anasimulia kwamba, pamoja na mganga kumwambia kwamba hakuchukua hela, lakini waliporudi nyumbani alianza kumpiga tena na kumwambia atamchoma moto, labda ama arudishe hiyo Pela au arejee kwa mama yake Dar es Salaam.

"Yaani nilivyosikia hivyo, nilikuwa nalala usiku kwa wasiwasi nikiogopa kwamba lolote laweza kunitokea. Nilikuwa naenda shuleni huku sina amani, mwalimu alikuwa akifundisha darasani hata sielewi vizuri,"anasimulia Priska.

Anasema, alilazimika kukimbia vitisho vya mama yake mdogo usiku bila ya kuaga, alipoenda kuwaomba walinzi kulala katika baraza la duka, mjini Dodoma na asubuhi walinzi hao walimuombea lifti katika gari ya mizigo, hadi Dar es Salaam kwa mama yake.

"Nilifika Dar es Salaam nimechoka sana. Nilikuta mama yangu bado ana hali ngumu, alikuwa ameugua kwa muda mrefu na hana nguvu za kufanya kibarua chochote na alikuwa anasaidiwa na majirani tu chakula na akipata nguvu mara moja moja, anaenda kufanya vibarua vya kufanya usafi kwa majirani.

"Nilipata wakati mgumu sana na nilianza kutafuta kazi yoyote hata za ndani, ili mradi tupate chakula mimi na mama yangu na wakati huo nilikuwa na miaka 11 tu. Shule ilibidi niache," anasimulia mkasa, akifafanua:

"Nilibahatisha kupata kazi ya ndani, lakini ilikuwa kama mkosi. Nilifanya mwezi mmoja tu, baba mwenye nyumba akawa anataka kunibaka, nilikimbia na sikutamani tena kufanya kazi za ndani"

**ALIVYOANZA KUOMBA**

Anasimulia kwamba hali ilipozidi kuwa mbaya, hakuna chakula ndani na mama yake hali ya afya haikuwa imeimarika vizuri, aliamua kwenda katikati ya jiji la Dar es Salaam, eneo analolitaja la Posta, kuanza uombaji misaada.

"Huko nilikutana na wenzangu wengine ambao wengine walikuwa na matatizo kama ya kwangu, nikawa naandamana nao na hapo ndipo nikawa naenda kuomba kila siku.

"Nikawa nabahatisha kupata Shilingi 5000 au Shilingi 2000 kwa siku, ikawa inatusaidia chakula mimi na mama yangu. Mpaka sasa ndiyo naendelea na kazi hii," anasema Priska.

"Huwa namlaumu sana mama yangu mdogo. Naona kama yeye ndiye alikatisha ndoto zangu, nilikuwa nasoma nikiamini nitamaliza halafu niwe muuguzi niwasaidie wagonjwa lakini haikuwa hivyo. "

**MKASA MITAANI**

Akisimulia maisha ya kuomba msaada mitaani, Prisha anasema amekuwa akikumbana na changamoto mbalimbali ambazo hata hivyo Mungu amekuwa akimsaidia kuzikabili.

"Wakati mwingine huku mtaani, huwa nakumbana na vikwazo vikubwa. Nikija kuomba huku, nakutana na 'wa-baba' wakubwa wanataka kwamba wafanye mapenzi na mimi, ndiyo wanipe hela na mwingine anakufuata kabisa anakuonyeshea kitita cha hela.

"Anasema niende naye nikafanye mapenzi ili anipe. Nikiona hivyo, nakimbia na ukikataa wakati mwingine, wanakutukana matusi. Wanasema; shauri yako utaendelea kuomba hivyo mpaka uzeeni," anasimulia Priska.

Anasema wapo baadhi ya wenzake aliokuwa anaomba nao

**INAENDELEA UK.18**

# Biashara katika picha



Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Wilaya ya Nyamagana, Joyce Kotecha (kushoto), akimkabidhi jaketi ya usalama Mwenyekiti wa Bodaboda Mkoa wa Mwanza, Gerald Nyerembe, wakati wa uzinduzi wa kampeni ya kampuni ya bia ya Serengeti ya Don't Drink and Drive iliyozinduliwa jijini Mwanza juzi. **NA MPIGAPICHA WETU**



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Charamila (kulia), akiwakabidhi vitambulisho vya wafanyabiashara wadogo Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Paul Ntinika (katikati) na Mkurugenzi wa Mbeya Jiji, James Kasusura. **PICHA: KENNETH NGELESI**



Mchuuzi wa mikate akiwa ameisheheni kwenye pikipiki yake wakati akisaka wateja kando ya Barabara ya Sam Nujoma, eneo la Ubungo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

BEI YA MAZAO >> MAHINDI 52979.17/-| MAHARAGE 171739.13/-

UCHUMI

# Muuguzi mtarajiwa aliyejikuta anaangukia kuomba mitaani



Mama anayedaiwa kuomba, katika Barabara ya Ali Hassan Mwinyi, akiwa na mwanawe. **PICHA: MTANDAO**

**INATOKA UK.17**

mtaani, ambao walishawishika na 'wa -baba' hao ambao waliwadanganya kwenda kufanya nao mapenzi, ili wawape pesa nyingi.

"Wapo watoto ambao nilikuwa naomba nao, walirubuniwa, hivyo hivyo na hao 'wa-baba' wakubwa wenye pesa, wakaenda kufanya nao mapenzi, lakini hata hela yenyewe hawakupewa.

"Wengine wamepata na mimba na wanaomba na watoto wao humu tunawaona na wengine waliamua kuhamia mitaa mingine kwa aibu. Mimi walikuwa wanaiona kama 'mshamba,' lakini nikawaambia 'sawa.' Sasa hivi wanaona aibu na wanahangaika vilevile," anasimulia Priska.

Priska anasema, huko mtaani wanakoomba msaada, kuna baadhi ya watoto wanaharibikiwa kujiunga na makundi ya kuvuta bangi, matumzi ya dawa za kulevya na hata udokozi.

"Dada yangu (mwandishi) nakwambia kukaa huku mtaani yataka moyo, ni shida tu ndiyo zinasababisha tufanye hivi. Yaani kuna tabia za ajabu huku, nimeshuhudia mengi sana.

"Kuna watoto wanavuta bangi, dawa za kulevya na ni wadokozi na wana matusi. Kama huna roho ngumu unaweza kuharibikiwa sana. Lakini, mimi nilishajiwekea msimamo kwamba sitakubali kudanganyika kwa lolote. Huwezi kuamini eti wananiita mgumba... hahahaaaa....."anasimulia, huku akiangua kicheko.

Priska anaeleza hisia zake, akitamani kuachana na maisha hayo, endapo atatokea mtu wa kumsaidia kumpatia mtaji hata wa kuuza biashara ndogo au kwenda kujifunza ufundi wa kushona nguo.

> **"Haya maisha ya mtaani yamenichosha sana. Yaani akijitokeza mtu akanisaidia hata mtaji wa biashara ndogo au nikaenda kusoma ushonaji, mimi nitaondoka. Sitamani kabisa kazi hii.**

"Haya maisha ya mtaani yamenichosha sana. Yaani akijitokeza mtu akanisaidia hata mtaji wa biashara ndogo au nikaenda kusoma ushonaji, mimi nitaondoka. Sitamani kabisa kazi hii," anasema Priska.

Pia anasema kwamba watoto ambao wako katika maisha ya kuomba, ni wagumu kusaidiwa. Anasimulia: "Kuna watoto wengine humu tulishuhudia kabisa, wamepewa hela ya kutosha kufanyia biashara ndogo, lakini cha kushangaza tuliwaona wamerudi tena.

"Unajua dada, watoto wengine kutokana na kukaa muda mrefu humu, inaonekana kama wameharibikiwa. Hata ukiwasaidia vipi, hawasaidiki, wameshazoea. Yaani watoto wanaharibikiwa jamani humu...." anaeleza kwa mshangao.

Anaendelea kusimulia katika hali ya tahadhari: " Kama unavyowaona, hao wengine wamekuwa kama chizi, wana makundi ya ajabu ya kuvuta bangi na ukijaribu kuwasogelea wanaweza kukufanya vibaya. Usidhubutu dada."

"Mimi sijabahatika kupata mtu wa kunisaidia, kama ambavyo baadhi ya wenzangu wamebahatika. Siku nikibahatika, nitafurahi sana. Natamani kuondoka mitaani kabisa, nisahau haya maisha na ibaki historia.

"Ila nakuhakikisha dada, siwezi kuingia kwenye hayo makundi kama walivyoingia wenzangu wakaharibikiwa. Ninachoamini ipo siku moja nitafanikiwa niondoke humu," anasimulia.

**MAMA PRISKA JE?**

Jitihada za Nipashe, zilifanikiwa kuzungumza na mama wa Priska, Tatu Mgome, anaeleza maisha yake ya sasa ni kwamba, kazi inayomsaidia kuendesha familia ni kufanya kazi ndogo katika majumba ya watu.

"Priska ni mwanangu pekee na baba yake alifariki akiwa ni mdogo sana. Kwa hiyo, mimi ndiyo nilihangaika kumlea hadi alipofikia umri wa kwenda shuleni na kuna kipindi niliugua sana, ikabidi nimpeleke kwa bibi yake Dodoma. Huko alipata matatizo makubwa, ikabidi arudi na kama unavyomuona hivyo hayo maisha ndiyo anaishi,"anasema.

"Maisha yetu kwa kweli bado ni magumu sana. Tumepanga chumba kimoja cha Shilingi 30,000 na ninaishi na Priska mwenyewe. Mimi na mtoto mdogo wa miaka saba, ambaye mdogo wangu amemtelekeza na sijui alipo.

"Maisha yangu ni kufanya vibarua vidogo kwenye nyumba za watu, ambao huwa wananiita nikafanye na kama hawajaniita siku hiyo maisha yanakuwa magumu zaidi. Priska ndiye huwa ananisaidia anachopata mtaani. kinatusaidia kula siku nikikosa," anaeleza

Anasema kikuu anachomhusia mtoto wake, ni kumwelekeza asirubunike na pesa. Mama huyo anasema: "Nashukuru Mungu kwamba mwanangu ananisikiliza. Kama unavyomuona anahangaika kuomba na anasikiliza. Sijawahi kushuhudia mabadiliko ya tabia na wapo wenzake ambao wameharibikiwa kabisa."

"Wamerubuniwa wakazalishwa watoto na wanapata nao tabu. Walikuwa wanamwita Priska 'mgumba' eti kwa nini na yeye asizae mtoto kama wao. Ni jambo la kushangaza sana, hivi dada unashuhudia haya maisha tuliyo nayo, halafu eti akazae tena mtoto? anahoji Mama Priska katika hali ya mshangao.

Anasema aliwahi kupata mtaji akaanzisha biashara ya kuuza genge, lakini ana kisia cha kufilisika kwake: "Si unajua majirani walivyo, walikuwa wanakuja kunikopa, mtu anakuambia nakuletea sasa hivi, unashindwa kumnyima, lakini walikuwa hawanilipi, mpaka nikafilisika."

**WAZIRI JAFO**

Akizungumza na Nipashe, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Tawala za mikoa na Serikali za Mitaa), Selemani Jafo, anafafanua dhana ya 'watoto wa mitaani' akitamka:

"Hakuna watoto wa mitaani. Kila mtoto ana baba na mama yake. Jamii lazima ijue kwamba jukumu la malezi kwa watoto ni lake, tuache utamaduni wa kuzaa halafu unaacha kulea watoto. Kila jamii ihakikishe ina jukumu la kulea watoto.

"Maelekezo yangu ni kwamba, jamii itafakari kwamba hakuna mtaa unaozaa mtoto wa mitaani, isipokuwa inatokana na tofauti zilizopo katika familia zetu.Ukiona hata kama mtoto ni yatima, lakini kuna ndugu zake wa karibu. Tujitahidi kulea watoto wetu, jamii ihakikishe inaimarisha malezi. Kwa pamoja, iwasaidie watoto hawa."

Wakati binafsi alikiri mwaka juzi kuwepo janga la watoto wa mitaani, Waziri Jafo anasema ameshawaelekeza wakuu wa mikoa kuhakikishe wanaratibu mkakati bora ya kuwasaidia na kuondoa janga la watoto hao wanaotaabika.

"Wanaotoa huduma za jamii waangalie wanafanya kazi yao vya kutosha, ikiwamo kutoa elimu na mambo mengine mtambuka na kila mkoa kuweka mkakati kuhakikisha tunaondoa tatizo hili,"anasema Jafo.

Katika takwimu hizo za mwaka 2017, katika mkoa wa Dar es Salaam, ikionyesha ongezeke kwa asilimia 28, likiwa na jumla ya watoto wa mitaani 1568.

Haki za Mtoto nchini, zinalindwa na kusimamiwa na sheria na miongozo kadhaa, ikiwamo Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009, inayojumuisha ukuzaji, ulinzi, kuhifadhi na ustawi wa mtoto

***• Ijumaa ijayo usikose makala nyingine ya mkasa kama huu.***

**FEDHA >>** USD 2294.81| Pauni 3001.15| Euro 2622.05

UCHUMI

KISARAWE

# Siku Waziri Mgalu alipowasha taa ya historia kijijini Kisarawe

- Ashuhudia maji baridi mara ya kwanza
- Diwani ajitutumua kwa kituo cha basi

**Na Amri Lugungulo,** Kisarawe

UMEME unaosambazwa sasa katika vijijini mbalimbali katika wilaya ya Kisarawe, mkoa wa Pwani na Wakala wa Umeme Vijijini (REA), umeanza kuwa kichocheo cha maendeleo katika wilaya hiyo.

Nishati hiyo ni kwamba imeunganishwa kwenye makazi ya watu binafsi, taasisi za kiserikali na watu binafsi, pia kwenye miradi ya maendeleo ya kijamii.

Ni mambo yaliyojiri katika ziara ya Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, alipotembelea kwa siku moja hivi karibuni wilayani hapa, akiwa katika vijiji vitano vya; Kibuta, Masanganya, Chang'ombe B, Mfuru na Mengwa.

Huko alizindua nyumba sita za wakazi binafsi, ambako walionekana kuanza kujiendesha kiuchumi kwa kutumia nishati hiyo.

Umeme huo pia umeboresha huduma katika vituo vya afya na shule, ikiwa ni utekelezaji wa ahadi ya awali kwamba ziara yake imedhamiria kuwahamasisha wananchi waondokane na matumizi ya vibatari na taa za kandili.

Katika shule alizozuru, Naibu Waziri Subira, alishuhudia wanafunzi kuanza kupata unafuu kwa kujisomea usiku wakinufaika na nishati ya umeme, pamoja na kupunguza kasi ya matukio ya ubakaji wasichana nyakati za usiku. Ni ushuhuda ulioanika kioo cha mafanikio hayo, hali kadhalika kichocheo zaidi cha maendeleo ya wajasiriamali, kwa kuwaongezea kiasi cha uzalishaji wa bidhaa na uboreshaji wake.

Katika ziara hiyo ya Naibu Waziri Subira, moja ya makazi yaliyokuwa kioo cha uzinduzi huo ni ni kwenye nyumba ya mwanakijiji wa Kibuta, Zainabu Rashidi, aliyeanza kufaidika kwa kuanza kunywa maji baridi yaliyotoka kwenye friji kwa mara ya kwanza nyumbani kwake, tangu Uhuru wa nchi mwaka 1961.

NaibuWaziri alimpongeza mwananchi huyo na kumtaka aongeze bidii za kupanua ukubwa wa mradi wake wa kuuza maji baridi na vinjwaji vinginyevyo, kama vile soda baridi, ili kuzidi kujiendesha kiuchumi.

"Zidisha juhudi za kupanua shughuli zako za ujasiriamali, ili uzidi kujiendesha kiuchumi kwa kutumia nishati hii," anasema Kibuta.

Mbunge huyo wa Viti maalum, katika ziara yake hiyo, alizindua miradi ya matumizi ya umeme katika vijiji vitano na kuwapongeza na kuwahimiza kupanua miradi yao, huku akiwataka wananchi wengine kuingiza umeme katika nyumba zao, ili waishi katika kiashiria cha kimaendeleo.



Mhandisi Emanuel Manlabona, akimwonyesha Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, uwezo wa kituo hicho cha kusambaza umeme. Kulia ni Mkurugenzi Msaidizi wa Usafirishaji Umeme, Mhandisi Bishaija Kahitwa. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

> **"Msikae maofisini, waunganishieni umeme wananchi na taasisi zote, zikiwamo shule na vituo vya afya kwa ajili ya kuleta maendeleo.**



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, akionyesha ishara ya kuwasha umeme katika nyumba mojawapo Kijiji cha Kisanga, wilayani Kisarawe, mkoa wa Pwani.

Katika kijiji cha Kibuta, Naibu Waziri huyo alitembelea kituo kipya cha mabasi ya abiria kinachojengwa kwa msukumo mkubwa wa Diwani wa Kata yua Kibuta, Mhandisi Mohamed Kilumbi, akimmiminia pongezi diwani huyo.

Diwani Kilumbi alimwambia kituo kiko mbioni kuingiza umeme, hali itakayonufaisha kufanya kazi usiku na mchana, ikiwa na usalama wa kutosha.

Anasema kituo kitakuwa kinapokea mabasi kutoka sehemu mbalimbali jirani, akizitaja baadhi kuwa ni Chanika, Msanga, Maneromango na Mzenga kitakuwa kikifanya kazi saa 24.

Naibu Waziri aliyewahi kuwa Mkuu wa Wilaya hiyo, anawahimiza wananchi wa Kisarawe, kuanza kutumia nishati hiyo kwa manufaa yao wajiwezeshe kupiga hatua kiuchumi.

Naibu Waziri Subira, ameliagiza Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (Tanesco) na REA, kufanya kazi kwa bidii kusambaza umeme katika vijiji vyote, ili zichangie kuchiochea maendeleo ya wananchi wa Kisarawe.

"Msikae maofisini, waunganishieni umeme wananchi na taasisi zote, zikiwamo shule na vituo vya afya kwa ajili ya kuleta maendeleo," anasema Naibu Waziri Subira.

Anazitaka mamlaka hizo kumalizia maeneo yaliyobaki ili kuepuka kugombanisha serikali na wananchi.

"Maeneo yaliyobaki yamalizwe, msije mkagombanisha wananchi na serikali," anasema.


# Takwimu za Biashara

Na Edward Ntwale & Elias Samweli

Bei ya Mazao Ya Chakula kwa Sh/kilo 100 Januari 28, 2019

| Mkoa | Arusha | D'Salaam | Dodoma | Geita | Kagera | Kilimanjaro | Kigoma | Manyara | Morogoro | Mwanza |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mahindi | 43000 | 70000 | 43000 | 56000 | 60000 | 50000 | 50000 | 54000 | 50000 | 65000 |
| Mchele | 200000 | 230000 | 195000 | 160000 | 185000 | 180000 | 160000 | 200000 | 170000 | 170000 |
| Mtama | 35000 | 60000 | 35000 | 125000 | 100000 | 80000 | 70000 | 42000 | 95000 | NA |
| Uwele | 45000 | 70000 | 41000 | NA | 110000 | NA | 60000 | 100000 | 95000 | 150000 |
| Ulezi | 75000 | 140000 | 85000 | 185000 | 150000 | 180000 | 150000 | 120000 | 160000 | 160000 |
| Ngano | 75000 | 150000 | 160000 | 165000 | NA | 106000 | 150000 | 120000 | 175000 | NA |
| Maharage | 160000 | 210000 | 160000 | 160000 | 150000 | 160000 | 145000 | 150000 | 180000 | 170000 |
| Viazi Mviringo | 80000 | 80000 | 70000 | NA | 75000 | 70000 | 90000 | 100000 | 82500 | 80000 |

## Mwenendo wa Shilingi




## Mafuta

Bei : Kuanzia Januari 2, 2019

| MKOA | DSM | Arusha | Kibaha | Dodoma | Geita | Iringa | Katavi | Kigoma | Mwanza | Ruvuma |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Petroli | 2,295 | 2,255 | 2,300 | 2,354 | 2,461 | 2,359 | 2,503 | 2,527 | 2,445 | 2,419 |
| Dizeli | 2,224 | 2,299 | 2,228 | 2,283 | 2,389 | 2,288 | 2,432 | 2,455 | 2,374 | 2,347 |
| M'Taa | 2,202 | 2,286 | 2,206 | 2,260 | 2,367 | 2,266 | 2,410 | 2,433 | 2,352 | 2,325 |

## Soko la Hisa la Dar es Salaam Kikao cha Januari 30, 2019

### Muhtasari

| | | |
|---|---|---|
| TSI | 3,615.22 | +0.00 |
| DSEI | 2,120.77 | +6.10 |
| Thamani za Hisa (bln) | 20,442.00 | |
| Mauzo | 63,378,240.00 | |
| Hisa | 234,633 | |

### Zilizopanda na Zilizoshuka

| Kampuni | Bei | Badiliko |
|---|---|---|
| JHL | 9,750 | -1.02% |
| NMG | 1,400 | -4.11% |
| KA | 210 | +5.00% |
| ACA | 5,700 | +0.88% |
| ACA | 5,250 | +1.94% |

### Viwango vya kubadilisha

| Fedha | Nunua | Uza |
|---|---|---|
| EUR | 2,591.28 | 2,617.65 |
| USD | 2,268.07 | 2,290.76 |
| KES | 22.38 | 22.56 |
| GBP | 2,947.82 | 2,977.52 |

## Bei za hisa hadi kikao cha Januari 30, 2019

| Kampuni | Bei ya mwisho | Bei Iliyopita | Ba'liko % |
|---|---|---|---|
| ACA | 5,700 | 5,650 | +0.88 |
| CRDB | 135 | 135 | +0.00 |
| DCB | 340 | 340 | +0.00 |
| DSE | 1,340 | 1,340 | +0.00 |
| EABL | 4,760 | 4,760 | +0.00 |
| JHL | 9,750 | 9,850 | -1.02 |
| KA | 210 | 200 | +5.00 |

| Kampuni | Bei ya mwisho | Bei Iliyopita | Ba'liko % |
|---|---|---|---|
| KCB | 900 | 900 | +0.00 |
| MBP | 500 | 500 | +0.00 |
| MCB | 500 | 500 | +0.00 |
| MKCB | 800 | 800 | +0.00 |
| MUCOB | 400 | 400 | +0.00 |
| NICO | 265 | 265 | +0.00 |
| NMB | 2,340 | 2,340 | +0.00 |

| Kampuni | Bei ya mwisho | Bei Iliyopita | Ba'liko % |
|---|---|---|---|
| TBL | 12,400 | 12,400 | +0.00 |
| TCC | 17,000 | 17,000 | +0.00 |
| TCCL | 640 | 640 | +0.00 |
| TICL | 385 | 385 | +0.00 |
| TOL | 660 | 660 | +0.00 |
| TPCC | 2,060 | 2,060 | +0.00 |
| TTP | 120 | 120 | +0.00 |

## VIWANGO VYA KUBADILISHA FEDHA

| FEDHA | KUNUNUA | KUUZA |
|---|---|---|
| KENYA SHS | 22.53 | 22.71 |
| UGANDA SHS | 0.58 | 0.62 |
| RWANDAN FRANC | 2.53 | 2.56 |
| BURUNDI FRANC | 2.18 | 2.19 |
| USD | 2272.09 | 2294.81 |
| POUND STG | 2970.53 | 3001.15 |
| EURO | 2595.18 | 2622.05 |
| CANADIAN $ | 1719.07 | 1735.73 |
| SWITZ. FRANC | 2276.41 | 2298.49 |
| JAPANESE YEN | 20.75 | 20.95 |
| SWEDISH KRONOR | 249.95 | 252.37 |
| NORWEG. KRONOR | 267.78 | 270.33 |
| DANISH KRONOR | 347.73 | 351.16 |
| AUSTRALIAN $ | 1633.63 | 1650.20 |
| INDIAN RPS | 31.93 | 32.23 |
| PAKISTAN RPS | 15.59 | 16.28 |
| ZAMBIAN KWACHA | 188.63 | 191.63 |
| MALAWIAN KWACHA | 2.91 | 3.10 |
| MOZAMBIQUE-MET | 36.50 | 36.81 |
| ZIMBABWE $ | 0.43 | 0.43 |
| SDR | 3174.49 | 3206.24 |
| GOLD (T/O) | 2978617.94 | 3008656.32 |
| S. AFRICAN RAND | 166.83 | 168.31 |
| UAE DIRHAM | 618.61 | 624.78 |
| SINGAPORE $ | 1681.91 | 1698.10 |
| HONK KONG $ | 289.62 | 292.51 |
| SAUD ARABIAN RIAL | 605.83 | 611.85 |
| KUWAIT DINAR | 7493.70 | 7566.14 |
| BOTSWANA PULA | 216.98 | 220.99 |
| CHINESE YUAN | 338.52 | 341.39 |
| MALAYSIA RINGGIT | 553.49 | 558.35 |
| SOUTH KOREA WON | 2.03 | 2.05 |
| NEWZEALAND | 1550.93 | 1567.58 |

## Interbank Foreign Exchange Market (IFEM)

| Tarehe | Idadi (Mn USD) | Juu | Chini | Wastani |
|---|---|---|---|---|
| **30/Jan/2019** | **1.75** | **2,304.00** | **2,293.60** | **2,294.81** |
| 29/Jan/2019 | .70 | 2,302.00 | 2,293.55 | 2,294.78 |
| 28/Jan/2019 | .80 | 2,302.00 | 2,293.50 | 2,294.59 |
| 25/Jan/2019 | .80 | 2,300.65 | 2,293.50 | 2,294.41 |

## Inter-bank Local Money Markets

| Tarehe | Kiasi (million-TZS) | Juu | Chini | Wastani (WAR) |
|---|---|---|---|---|
| **30/Jan/2019** | **9,500** | **4.00** | **3.50** | **3.53** |
| 29/Jan/2019 | 11,000 | 4.25 | 3.50 | 3.76 |
| 28/Jan/2019 | 7,500 | 3.50 | 3.50 | 3.50 |
| 25/Jan/2019 | 17,000 | 4.40 | 3.50 | 3.78 |
| 24/Jan/2019 | 17,500 | 4.25 | 3.00 | 3.61 |
| 23/Jan/2019 | 44,500 | 4.20 | 2.50 | 3.38 |

MGOGORO WA KIBIASHARA:

## Marekani na China zaanza duru mpya ya mazungumzo

DURU nyingine ya mazungumzo juu ya kutatua mgogoro wa kibiashara baina ya Marekani na China ilianza jana. Wajumbe wa ngazi za juu wa kutoka nchi mbili hizo wanakutana mjini Washington.

Wajumbe hao wanatarajiwa kutafuta njia za kuepusha kupanuka kwa mgogoro huo wa kibiashara kati ya nchi mbili hizo. Marekani na China zimebakiwa na mwezi mmoja hadi mwisho wa muda wa siku 90 walizokubaliana mnamo mwezi Desemba mwaka uliopita, kusimamisha mvutano wa kibiashara baina yao.

Ikiwa mazungumzo hayo hayatafanikiwa, itakapofika tarehe 2 Machi, Marekani itaziongezea ushuru wa thamani ya dola bilioni 200 bidhaa kutoka China.

Wachumi wanahofia kwamba mvutano huo unaweza kusababisha athari kubwa katika uchumi wa dunia. Kutokana na mgogoro huo wa kibiashara, Kamishna wa Idara ya Takwimu wa China, Ning Jizhe amesema mgogoro huo unaathiri uchumi wa China huku Marekani ikikiri kuwa uchumi wake umeathirika kwa sababu hiyo hiyo.

Kiongozi wa ujumbe wa watu 30 kutoka Beijing, ambaye ni Makamu wa Rais wa China, Liu He alimweleza mwakilishi wa biashara wa Marekani kwenye mazungumzo hayo, Robert Lighthizer juu ya kutofurahishwa na hatua ya kufunguliwa mashtaka kampuni kubwa ya mawasiliano ya China Huawei, hatua ambayo amesema ni kinyume cha sheria.

Hatua hiyo huenda ikayavuruga mazungumzo ya biashara kati ya nchi mbili hizo. Marekani na China, nchi zenye nguvu kubwa za kiuchumi duniani zinapigania udhibiti wa baadaye katika sekta muhimu ya teknolojia.

Miaka mitatu iliyopita, China ilizindua mpango wa kimkakati unaoitwa "Bidhaa za China kufikia mwaka 2025" ambao unalenga kulifanya taifa hilo kuwa kiongozi wa kimataifa katika uhandisi wa teknolojia ya anga, matumizi ya maroboti, na utengenezaji wa mashine zenye kutumia teknolojia ya akili ya bandia.

Hali kadhalika, ubunifu mpya katika utengenezaji wa magari na maeneo mengine yanayohusiana na teknolojia ya kisasa, sekta ambayo Marekani inasema ni eneo la taifa hilo kubwa ambalo linaamini kuwa linaongoza katika masuala ya teknolojia, ubunifu na uvumbuzi.

Rais wa Marekani, Donald Trump amesema mara kwa mara kwamba sio haki kwa uchumi wa China kuendelea kukua kwa gharama ya biashara na ujuzi wa Marekani. Nchi hiyo inailaumu China kwa kutokuzingatia haki katika biashara, kutokana na wizi wa hati fungani za raia wa Marekani na vitendo vya udukuzi wa teknolojia.

Ili kuishinikiza China, Marekani imeitoza nchi hiyo ushuru wa dola bilioni 250 kwa bidhaa zake zinazoingia Marekani. Kwa upande wake China inazitoza ushuru wa dola bilioni 110 bidhaa zinazotoka Marekani.

Waziri wa fedha wa Marekani Steven Mnuchin amesema kutokana na ugumu wa masuala hayo, makubaliano ya kuumaliza mgogoro huo hayatazamiwi kufikiwa kwenye mkutano huo wa siku mbili wa mjini Washington lakini anatarajia watapiga hatua kubwa.

**CHANZO: DW**



Wajumbe wa mkutano wa biashara China na Marekani, walipokutana jana, kikao kinamalizika leo . **PICHA ZOTE: MTANDAO.**



**HABARI MBEYA**

# Mkoa wa Mbeya wajipanga kukabiliana tishio la kutokea mauaji ya watoto

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

SIKU chache baada ya Mkoa wa Njombe kukabiliwa na jinamizi la mauaji ya watoto, Serikali ya Mkoa wa Mbeya imeanza kuchukua tahadhari ya kuzuia vitendo hivyo ikidai kuwa matukio hayo yanaweza kuwakumba.

Akizungumza jana wakati wa Mkutano na Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi na watendaji wa Halmashauri zote za Mkoa huo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila alisema kuna baadhi ya Wilaya zina kiwango kikubwa cha mauaji.

Alizitaja Wilaya hizo kuwa ni Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Chunya, Kyela na Mbarali ambapo alidai kuna mauaji ya ajabu yanayoweza kuupelekea Mkoa huo kuzua hofu miongoni mwa wananchi wa Mkoa huo.

Chalamila aliwataka Wakuu wa Wilaya zote za Mkoa huo kutengeneza mikakati ya pamoja ya kukabiliana na matukio ya mauaji ya watu pamoja na matukio mengine yanayokiuka haki za binadamu ikiwemo ubakaji wa watoto unaohusishwa na imani za kishirikina.

"Wenzetu Njombe tumesikia kuwa wanakabiliwa na janga la mauaji ya watoto ambayo yanahusishwa na imani za kishirikina na kati ya watoto waliouawa watatu ni wa familia moja, sasa hata sisi tunatakiwa tuweke mikakati ya kujihami," alisema Chalamila.

Alisema mbali na mauaji hayo lakini pia baadhi ya Wilaya za Mkoa huo zinakabiliwa na ubakaji wa watoto na kwamba yote hayo yanatakiwa kudhibitiwa ili wananchi waendelee kuishi kwa amani.

Alisema Wilaya ya Chunya ndiyo inayoongoza kwa kuripotiwa vitendo vya ubakaji ambavyo vinahusishwa pia na imani za kishirikina hasa kutokana na Wilaya hiyo kuwa na migodi mingi ya dhahabu.

Hivi karibuni Mkoa wa Njombe ulijawa na taharuki baada ya kuripotiwa taarifa za watoto 10 kuuawa na watu wasiojulikana huku mauaji hayo yakihusishwa na imani za kishirikina kutokana na watoto hao kukutwa wamenyofolewa baadhi ya viungo.

Kutokana na mauaji hao Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, alifika katika Mkoa huo na kufanya Mkutano wa hadhara na wananchi kwa ajili ya kuwafariji wafiwa na kuwaeleza mikakati ya serikali ya kumaliza mauaji hayo.

Katika mkutano huo, Naibu Waziri alimwagiza Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP), Simon Siro kuunda tume ya wataalamu kwa ajili ya kwenda kuchunguza mauaji hayo.




Mchuuzi wa parachichi akimhudumia mteja kando ya Barabara ya Bibi Titi Mohamed, eneo la Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam jana. Parachichi moja aliiuza kwa bei ya 1,500/-. Kwa sasa kuna uhaba wa matunda hayo jijini Dar es Salaam, hivyo bei kupaa. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Halmashauri yapoteza ml. 72/- za ushuru wa kakao

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

BARAZA la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya, limesema limepoteza zaidi yaSh. milioni 72 kwenye ushuru wa zao la Kakao kutokana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika kuweka bei maalumu ya zao hilo kinyume cha matakwa ya sheria ya ushuru.

Akizungumza kwenye kikao cha kawaida cha kujadili mapendekezo ya bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020, Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Hunter Mwakifuna, alisema sheria inawataka kutoza ushuru wa asilimia tatu kwa kilo moja ya zao la kakao, lakini tume imeweka kiwango maalumu cha Sh. 126.

Alisema kwa sasa Wilaya ya hiyo inapoteza shilingi tisa kwa kila kilo kutokana na zao hilo kupanda bei huku kiwango cha ushuru kikiendelea kuwa kilekile cha shilingi 126 badala ya kuwa 135 kama sheria inavyotaka. Mwakifuna alisema Wilaya hiyo kwa sasa inazalisha kilo 8,000,000 na kwamba inapoteza shilingi tisa kwa kila kilo hivyo kuifanya kupoteza shilingi milioni 72 zingetumika kwenye miradi ya maendeleo kwa wilaya hiyo.

"Tume ya ushirika imetufanya tupoteze mapato mengi, kwa sasa kakao imeuzwa kwenye minada imeuzwa zaidi ya shilingi 4,500 lakini kiwango cha ushuru kimebaki kilekile ambacho kimewekwa na tume ya maendeleo ya ushirika sasa tunaomba tume isitufunge," alisema Mwakifuna.

Alisema lengo la serikali kutaka mazao ya biashara yauzwe kupitia vyama vya ushirika ilikuwa ni kuhakikisha wananchi wanapata faida na serikali inakusanya mapato lakini baadhi ya changamoto bado zinasumbua ikiwemo hiyo ya Halmashauri kupoteza fedha.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Lucy Mganga alisema endapo ukusanyaji wa mapato utaimarishwa wilayani humo itakuwa rahisi kutekeleza miradi ya maendeleo inayokusudiwa kutekelezwa katika bajeti inayokisiwa. Alisema katika wilaya hiyo Kakao ni miongoni mwa mazao makubwa yanayoingiza fedha nyingi na hivyo akawataka watendaji kusimamia vizuri ili kuhakikisha mfumo wa ushirika unakuwa na tija iliyokusudiwa na Serikali.

Mganga alisema kila kiongozi wakiwemo madiwani wanatakiwa kuhakikisha mapato ya serikali yanakusanywa kwenye maeneo yao ili wanapodai miradi ya maendeleo wawe na uhakika wa utekelezaji wake.

"Tumekadiria kutumia shilingi bilioni nne kwenye miradi ya maendeleo katika maeneo ya kata zetu, sasa hatuwezi kufikia malengo kama hatutasimamia ukusanyaji wa mapato kwenye vyanzo vyetu hivyo kila mtu lazima ashiriki," alisema Mganga.

Alisema kwa sasa wanaendelea kutathimini ufanisi wa mfumo wa kuuza mazao kwa mfumo wa ushirika ili tuone namna ya kuboresha maana mfumo huu kwetu ni mpya.

Nao baadhi ya madiwani wa Halmashauri hiyo walisema watahakikisha wanashirikiana na watendaji wa serikali katika kuhimiza ukusanyaji wa mapato ili kuwezesha miradi ikamilike kwa wakati na kuwanufaisha wananchi.

## Hospitali yakabidhi vyerehani kwa mlemavu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HOSPITALI ya Kanda ya Rufaa ya Mbeya imemkabidhi msaada wa vyerehani viwili vya kushona na kufuma vitambaa mlemavu wa macho, Upendo Tebela mkazi wa Mkwajuni katika Wilaya ya Songwe ili kutatua changamoto za maisha zinazomkabili kutokana na ulemavu wake.

Akizungumza wakati wa kumkabidhi msaada huo kwa upendo ambaye aliambatana na ndugu zake, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa hospitali hiyo Dk. Paul Lawala alisema hospitali hiyo ni miongoni mwa taasisi zinazotoa huduma za afya kwa watu wote wakiwemo walemavu.

Alisema taasisi hiyo inatambua jitihada za Rais Dk. John Magufuli za kuwajali wananchi wa hali ya chini kwa kuhakikisha wanapata huduma bora za afya na kuwawezesha kiuchumi hivyo wao wakiwa kama wasaidizi wake wanawajibu wa kumuunga mkono.

Alisema vifaa hivyo vya kushonea vitamsaidia Upendo kutimiza ndoto zake kwani mashine hizo za kushonea nguo ni kiwanda kidogo hivyo mbali na kumsaidia pia imetekeleza azma ya serikali ya awamu ya tano ya kufikia uchumi wa viwanda ifikapo mwaka 2025.

"Upendo alimsikia Mkurugenzi wa hospitali Dk. Godlove Mbwanji akitoa ufafanuzi kwenye vyombo vya habari juu ya huduma za afya zinavyotolewa na hospitali yetu,lakini baadae aliamua kumtafuta Mkurugenzi kwa njia ya simu ili ampatie kibali cha kuuza soksi na nguo za Watoto katika eneo la hospitali," alisema Dk. Lawala.


Alisema Uongozi wa hospitali hiyo chini ya Mkurugenzi ilipokea ombi lake na kulifanyia kazi na kuamua kumnunulia mashine mbili za kushonea na kufumia vitambaa ili kumfanya asiwe tegemezi.

Alisema hospitali hiyo imekuwa ikiwahudumia watu wenye ulemavu wa viungo mbalimbali ikiwemo wasioona na kwamba ni hospitali ya kwanza nchini kuwa na mtafsiri wa lugha za alama kwa watu wenye ulemavu wa kusikia hatua iliyopelekea kujijengea uhusiano mzuri na watu kutoka makundi maalum.

Hata hivyo baada ya kupokea msaada huo, Upendo aliishukuru serikali kupitia uongozi wa hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya huku akiahidi kuutumia vizuri kwa ajili ya kujiongezea kipato na kujiinua kiuchumi pamoja na watu wengine atakaowaajiri.

Upendo alisema atatumia mashine hizo kwa kuongeza wigo wa kushona nguo kwa wingi kwa kuwaajiri watu wengine hivyo aliomba wadau wengine wamuunge mkono hasa katika eneo la kutafuta soko.

"Ninawaomba walemavu wenzangu waachane na tabia ya kuwa ombaomba na badala yake waanze kufikiria kufanya shughuli ndogo ndogo za kujiingizia kipato,"alisema Upendo.





# Waziri Biteko ashuhudia madudu uchenjuaji dhahabu

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

WAZIRI wa Madini, Dotto Biteko, ameshuhudia madudu yanayofanywa na wafanyakazi wa Ofisi ya Madini mkoani Dodoma, ikiwamo kushindwa kujaza gramu za dhahabu wanazozipokea kwa ajili ya kuzichenjua kabla hazijauzwa.

Kutokana na madudu hayo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini, Profesa Simon Msanjila, amemsimamisha kazi Ofisa Madini mkoani Dodoma, Ashen Daniel, ili kupisha uchunguzi.

"Ofisa Madini, Ashen, ameshindwa kujaza kwa makusudi gramu za dhahabu ambazo zimeletwa kuchenjuliwa ili wazifanyie utaratibu mwingine wa kuliibia taifa, kuacha kujaza gramu jambo ambalo ni kinyume na utendaji wa kazi ambao ameagizwa na serikali," alisema.

Vigogo hao wa Wizara ya Madini walifanya ziara ya kushtukiza katika ofisi za kuchenjua madini eneo la Kizota jijini Dodoma, ambapo walikutana na madudu hayo.

Aidha, alisema ofisa huyo atakuwa mfano kwa wengine wote wanaofanya kazi kwa kuiibia serikali, hawatakuwa katika mikono salama kwa kuwa atakwenda nao sambamba na hilo ni zoezi endelevu.

Alisema lengo ni kuhakikisha wezi wote wa madini wanaondoka ili kuiacha sekta hiyo ikiwa salama.

Akihojiwa ofisa huyo wa madini alisema ni kweli amepima madini, lakini hakujaza kutokana na changamoto mbalimbali ambazo pia alishindwa kuziainisha mbele ya viongozi hao na kusababisha kusimamishwa kazi ili kupisha uchunguzi uendelee.

Alisema ofisa huyo atakuwa mfano kwa maofisa wengine kutokana na utendaji mbovu wa kazi ya madini, jambo linalosababisha upotevu mwingi wa madini ambayo yanauzwa bila kujulikana.

Mbali na hivyo alimwagiza apeleke kazi zake zote za madini za miezi sita ambazo zimefanywa zikiwamo za kuchenjua na uuzaji unaofanywa na wanunuzi wa madini mbalimbali.

Profesa Msanjila alisema amemsimamisha ofisa huyo kwa muda usiojulikana ili kupisha uchunguzi uendelee kutokana na vitendo wanavyofanya katika ofisi hizo, ikiwamo kutofuatilia watu wanaonunua madini bila kuwa na leseni.

"Kuanzia leo nakusimamisha kazi ili uwaache watu wafanye uchunguzi kubaini ukweli wa mambo," alisema Profesa Msanjila.




Mwenyekiti wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, Dk. Titus Kaman (kulia), akikata utepe kuashiria uzinduzi rasmi wa magari ya vyama hivyo, juzi jijini Dodoma. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Halmashauri Kondoa yang'ara ukusanyaji mapato

**Na Paul Mabeja,** KONDOA

HALMASHAURI ya Mji wa Kondoa imepongezwa kwa ukusanyaji wa mapato kwa kipindi cha robo ya pili ya mwaka wa fedha 2018/2019 na kufikia asilimia 67 ya lengo la mwaka.

Pongezi hizo zilitolewa na Peter Gujenji, kwa niaba ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani lililofanyika katika ukumbi wa Kondoa Irangi.

Alisema kuwa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa inatambua na inathamini juhudi zinazofanywa katika ukusanyaji wa mapato na inawapongeza kwa juhudi hizo na inandaa barua ya kulithibitisha hilo. "Mwaka jana hadi robo ya pili inaisha halmashauri ya mji ilikusanya Sh. milioni 200 sawa na asilimia 23 ya makisio ya bajeti ya mwaka 2017/2018, lakini kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019 hadi robo ya pili inaisha halmashauri imekusanya zaidi ya Sh. milioni 500 sawa na asilimia 67 kwa kweli mnastahili pongezi," alisisitiza.

Aliwasihi viongozi wa halmashauri kuendelea kubuni mbinu zaidi za ukusanyaji wa mapato na kuongeza uwajibikaji na upendo ili kufikia malengo yaliyowekwa. Akizungumza katika kikao hicho Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji, Hamza Mafita, alisema kuwa mapato yameongezeka baada ya kupata mkurugenzi mpya ambaye amewezesha kufikia hapo na hiyo imetokana na kufanya kazi kwa ushirikiano kati ya madiwani na menejimenti.

"Tumeongeza mashine za kukusanyia mapato hadi kufikia 25, ambazo zimegawanywa katika kata mbalimbali kwa ajili ya kukusanya mapato na tuna mpango wa kufikisha mashine 50, ili kuhakikisha maeneo yote yenye mapato yanafikiwa," alisema Hamza.

Akielezea siri ya ukusanyaji wa mapato Mkurugenzi wa Mji wa Kondoa, Msoleni Dakawa, alisema mafanikio hayo yamefikiwa kutokana na ushirikiano uliopo kati ya watendaji na mikakati iliyowekwa katika ukusanyaji wa mapato.

"Tumeunda timu mbalimbali za ukusanyaji wa mapato kwa kuweka mameneja, ambapo kuna meneja wa masoko na mageti ya mazao, pamoja na hizo timu pia tumetenga siku maalum ya ukusanyaji wa mapato ambayo wakuu wa idara hujigawa na wasaidizi wao na kwenda kukusanya mapato," alisema Dakawa.

Alitoa wito kwa wafanyabiashara kuendelea kutoa kodi, kwa kuwa wakifanikisha hilo watawezesha halmashauri kujiendesha yenyewe pia itasaidia serikali kupata mapato na kuacha kutegemea misaada kutoka kwa wahisani.

# Mifumo imara ya Tehama itasaidia utendaji serikalini

**Na Renatha Msungu,**

DODOMA

SERIKALI imesema mifumo imara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, itasaidia utekelezaji wa malengo katika utumishi wa umma hapa nchini.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Mick Kiliba kwa niaba ya Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma, Laurean Ndumbaro, katika mkutano wa pili wa serikali mtandao.

Aidha, alisema kwamba serikali imefanya maboresho ya mifumo ya utendaji kazi katika programu ya maboresho ya utumishi wa umma.

Alifafanua kuwa kuna haja ya kuendelea kutumia Tehama, ili kuboresha mifumo hiyo na kufanya mapitio ya mara kwa mara kwa lengo la kuimarisha maboresho.

"Inabidi tuwe wabunifu katika suala hili kwa sababu tunahitaji kuona kila kitu kinakwenda sawa kupitia Tehama," alisema Kiliba.

Alifafanua kuwa uwezeshaji wa wananchi kupata huduma mbalimbali kama vile uanzishaji wa biashara, uombaji vibali mbalimbali na huduma ambazo zinahusiana na shuguli za kiuchumi za wananchi unategenea kuwa na mifumo imara ya utendaji wa kazi.

"Mtakubaliana na mimi ya kwamba iwapo mifumo na miundombinu ya Tehama itakuwa imewiwanisha na kuwezeshwa kubadilisha taarifa, itasaidia uboreshaji wa shughuli mbalimbali," alisema Kiliba.

Alisema lengo lao ni kuona mifumo hiyo inakuwa imara na ina uwezo wa kufanya kazi kwa haraka hasa pale wanapokuwa wanatoa huduma kwa wateja mbalimbali ikiwamo kufanya shughuli zao za kila siku.

Aidha, aliwataka washiriki kusikiliza mada zote kwa umakini na kwenda kuzifanyia kazi na siyo kufikiria kusaini mshiko pekee badala ya kujifunza ili kwenda kuelimisha jamii kwa ujumla.

# Halmashauri yatenga fedha kukarabati vyoo vya shule

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kusini Unguja, imetenga Sh. milioni 10 kwa ajili ya ukarabati wa ujenzi wa vyoo katika Shule ya Kusini Makunduchi.

Vyoo 12 vilivyopo shuleni hapo kwa sasa havitumiki kutokana na kuchakaa pamoja na kubomoka hali ambayo ni hatari kwa watumiaji ambao ni wanafunzi.

Uamuzi huo wa halmashauri kujenga vyoo hivyo unatokana na agizo la Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, ambaye alitembelea shule hiyo alipofanya ziara mwishoni mwa mwaka jana.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Kassim Mtoro, alisema kuwa fedha zimetokalewa na Mfuko wa Jimbo kupitia mbunge wa jimbo hilo.

Alisema kuwa vyoo hivyo vinahitaji matengenezo makubwa, hivyo fedha hizo hazitoweza kumalizia gharama za ujenzi wa vyoo hivyo hadi kukamilika kwake.

"Fedha ya mfuko wa jimbo zitazotumika katika ujenzi wa vyoo ni Shilingi milioni 10, ambazo zimetolewa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupitia Mbunge wa Jimbo la Makunduchi, lakini fedha hizi hazitoshi, hivyo tunawaomba watu wenye uwezo kuongeza nguvu ili kuweza kumaliza ujenzi huo," alisema. Aidha, alieleza kuwa halmashauri imekuwa ikisimamia vizuri matumizi ya fedha za mfuko wa jimbo kwa majimbo yaliyomo katika eneo hilo ili ziweze kutumika vizuri katika miradi mbalimbali ya maendeleo kwa wananchi.

Kwa upande wao wanafunzi wa Shule ya Kusini Makunduchi, walisema kukamilika kwa ujenzi wa vyoo kutawaondolea usumbufu wanaoupata kwa sasa.

Akizungumza kwa niaba ya wanafunzi wenzake, Mariyam Makame, alieleza kuwa hivi sasa shuleni hapo vyoo vinavyotumika ni vichache hali ambayo inasababisha msongamano kusubiria huduma hiyo.

Aidha, aliomba serikali kuharakisha ujenzi huo, ili kuweza kukamilika katika muda uliokusudiwa kwa kuwa majengo ya vyoo hivyo hayapo salama.



Mhandisi Mkuu wa Shirika la Umeme (Tanesco) Kibaha, Seleman Mgwira, akitoa maelezo kwa wawakilishi wa wananchi wa Kijiji cha Vikuge na Dengwa, Mkoa wa Pwani jana, kuhusu kuchelewa kwa kuunganishiwa umeme zaidi ya miaka minne. **PICHA: MUHIDINI MSAMBA**

# Rais Shein afikiria taasisi ya utafiti uvuvi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema serikali yake inakusudia kuanzisha taasisi ya utafiti ya uvuvi na mazao ya bahari ili kwenda sambamba na sera ya uchumi wa bahari.

Akizungumza na uongozi wa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi Ikulu mjini Zanzibar, alisema kuwa kuna umuhimu kwa Serikali ya Zanzibar kuwa na taasisi hiyo hasa ikizingatiwa mazingira ya visiwa hivyo na uchumi wake. Alieleza kuwa tayari Zanzibar ni mwanachama wa jumuiya ya nchizinazopakana na Bahari ya Hindi (IORA), hivyo kuna umuhimu mkubwa wa kuweka mikakati madhubuti katika kufikia malengo. Dk. Shein alieleza juhudi za makusudi zinazoendelea kuchukuliwa na serikali yake katika kuanzisha viwanda vya uvuvi na Chuo cha Ubaharia na kampuni yake ya uvuvi. Aidha, alisema kuwa umefika wakati kwa Zanzibar kuongeza ukubwa wa eneo la kilimo cha umwagiliaji, kwa kuwa mradi huo una umuhimu kwa Wazanzibari hasa ikizingatiwa kuwa chakula cha wali ndiyo kilichopewa kipaumbele na jamii.

Alieleza kuwa matarajio ya serikali ni kuongezeka kwa kiwango cha uzalishaji wa mpunga kutokana na mradi huo.

Naye Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Rashid Ali Juma, alieleza maendeleo ya mradi wa usimamizi wa shughuli za uvuvi wa Kanda ya Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIOFish) ambao ni mradi wa miaka sita.

## Vijana watakiwa kupenda kujitolea kusaidia jamii

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

VIJANA wameshauriwa kuendeleza utamaduni wa kujitolea katika kuisaidia jamii kwenye masuala mbalimbali ya kiuchumi, kijamii, kisiasa na kimaendeleo.

Ushauri huo umetolewa jana na Mwenyekiti wa kikundi cha Hamasa cha Ofisi Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Zanzibar, Shaaban Ali Othman, wakati akikabidhi majokofu mawili kwa uongozi wa Hospitali ya Kivunge ya Wilaya Kaskazini 'A' Unguja.

Alisema vifaa hivyo vimetolewa kwa ajili ya kusaidia uhifadhi wa vifaa tiba vya hospitali hiyo hasa dawa za matumizi ya binadamu zinazohitaji hali ya baridi muda wote.

Aliutaka uongozi wa hospitali hiyo kuvitunza na kuvitumia katika matumizi yaliyokusudiwa ili vitoe huduma endelevu kwa wananchi mbalimbali wanaofika hopitalini hapo kwa ajili ya matibabu.

Alieleza kuwa vifaa hivyo ni sehemu ya kuunga mkono juhudi zinazofanywa na viongozi wa CCM.

Alisema kwamba vijana wana wajibu wa kutekeleza kwa vitendo masuala mbalimbali ya kijamii kwa lengo la kuwasaidia wananchi wanaokabiliwa na changamoto katika mazingira wanayoishi.

Mwenyekiti huyo alisema endapo vijana wa Zanzibar wataweka mbele dhana ya uzalendo, umoja, mshikamano na kuelekezana mambo mema ya kuisaidia jamii, itasaidia Zanzibar kuwa nchi bora zaidi duniani iliyopiga hatua kubwa za kimaendeleo.

Katibu wa kikundi hicho, Suleiman Mohamed Rashid, alisema wataendelea kusaidia masuala mbalimbali ya kijamii katika maeneo yote Unguja na Pemba.

Alisema CCM kiko mstari wa mbele kushughulikia changamoto zinazoikabili jamii katika maeneo ya mijini na vijijini.

Akizungumza baada ya kupokea vifaa hivyo, daktari wa hospitali hiyo, Dk. Tamim Hamad Said, alisema wamefurahi kupokea vifaa hivyo, kwa kuwa vilikuwa ni miongoni mwa mahitaji muhimu.

Dk.Tamim aliahidi kuvitumia kwa malengo yaliyokusudiwa hasa kuhifadhi

dawa na vifaa mbalimbali vinavyotumika katika matibabu ili wananchi wapate huduma bora za afya.

## Kiongozi upinzani Cameroon ahojiwa

**YAOUNDE,** Cameroon

KIONGOZI mkuu wa upinzani nchini Cameroon, Maurice Kamto, amehojiwa na polisi wa mahakama ikiwa ni siku mbili baada ya kukamatwa akiwa nyumbani kwa mmoja wa wafuasi wake huko Douala.

Mgombea huyo wa zamani wa kiti cha urais bado anaendelea kushikiliwa huko mjini Yaoundé.

Mashtaka dhidi ya Maurice Kamto ni mazito, ambapo anatuhumiwa kuunda kikundi cha uasi, uadui dhidi ya nchi, kuhamasisha umma kuasi.

Mamlaka pia inawatuhumu wafuasi wa chama chake cha MRC na kuwataka kuwajibika kutokana na uharibifu dhidi ya balozi za Cameroon huko Paris na Berlin mwishoni mwa wiki iliyopita.

Zaidi ya watu 100 ambao ni wafuasi wa mgombea huyo wa zamani wa kiti cha urais wanazuiliwa katika maeneo mbalimbali nchini Cameroon, ambapo baadhi ya kesi zao zimeanza kusikilizwa. **RFI**

## Upinzani Venezuela ulifanya mikutano ya siri

**CARACAS,** Venezuela

KIONGOZI wa upinzani aliyejitangaza kuwa rais wa mpito wa Venezuela, Juan Guiado, amefichua kuwa amekuwa na mikutano ya siri na viongozi wakuu wa upinzani na wawakilishi wa jeshi.

Katika maoni yaliyochapishwa jana na gazeti la Marekani la New York Times, Guaido alisema hatua ya jeshi kuondoa uungaji mkono wao kwa Maduro ni muhimu katika kuwezesha mabadiliko ya serikali, na wengi wanaohudumu wanakubaliana kuwa matukio ya karibuni nchini humo hayakubaliki.

Guaido mwenye umri wa miaka 35, jana aliwaongoza maelfu ya waandamanaji wa upinzani mjini Caracas, akisema uamuzi wa mahakama ya juu nchini humo wa kumzuia kuondoka nchini haumpi wasiwasi wowote, akiongeza kuwa watu hawataki kuondoka nchini humo. Wanachotaka ni watu kurudi nchini humo.

Mamilioni ya wananchi wa Venezuela wamekimbia nchi hiyo tangu uongozi wa Hugo Chavez, na kwa sasa hali imezorota nchini humo na kusababisha hali mbaya ya kiuchumi ambayo imesababisha mfumuko wa bei. **DW**

# Marekani, China wakutana kutatua mgogoro kibiashara

**WASHINGTON,** Marekani

WAJUMBE kutoka ngazi za juu wa nchi za Marekani na China wamekutana kutatua mgogoro wa kibiashara baina ya nchi hizo, uliozuka hivi karibuni.

Wajumbe hao wanatarajiwa kutafuta njia za kuepusha kuongezeka kwa mgogoro huo wa kibiashara kati ya nchi hizo mbili.

Marekani na China zimebakiwa na muda wa mwezi mmoja hadi mwisho wa muda wa siku 90 walizokubaliana mnamo mwezi Desemba mwaka jana, kusitisha mvutano wa kibiashara baina yao.

Ikiwa mazungumzo hayo hayatafanikiwa, itakapofika Machi 2 mwaka huu, Marekani itaziongezea ushuru wa thamani ya dola bilioni 200 bidhaa kutoka China.

Wachumi wanahofia kuwa mvutano huo unaweza kusababisha athari kubwa katika uchumi wa dunia.

Katika mgogoro huo wa kibiashara kamishna wa Idara ya Takwimu wa China, Ning Jizhe, amesema mgogoro huo wa biashara unaathiri uchumi wa China, huku Marekani ikikiri kuwa uchumi wake umeathirika kutokana na mgogoro huo.

**Marekani pia inailaumu China kwa kutokuzingatia haki katika biashara, kutokana na wizi wa hati fungani za raia wa Marekani na vitendo vya udukuzi wa teknolojia.**

Kiongozi wa ujumbe wa watu 30 kutoka Beijing, ambaye ni Makamu wa Rais wa China, Liu He, alimweleza mwakilishi wa biashara wa Marekani kwenye mazungumzo hayo, Robert Lighthizer, juu ya kutofurahishwa na hatua ya kufunguliwa mashtaka kampuni kubwa ya mawasiliano ya China Huawei.

Alisema hatua hiyo ni kinyume cha sheria na kwamba huenda ikayavuruga mazungumzo ya biashara kati ya nchi mbili hizo.

Marekani na China nchi zenye nguvu kubwa za kiuchumi duniani zinapigania udhibiti wa baadaye katika sekta muhimu ya teknolojia.

Miaka mitatu iliyopita, China ilizindua mpango wa kimkakati unaoitwa bidhaa za China kufikia mwaka 2025, ambao unalenga kulifanya taifa hilo kuwa kiongozi wa kimataifa katika uhandisi wa teknolojia ya anga, matumizi ya maroboti, utengenezaji wa mashine zenye kutumia teknolojia ya akili ya bandia.

Pia kwenye ubunifu mpya katika utengenezaji wa magari na maeneo mengine yanayohusiana na teknolojia ya kisasa, sekta ambayo Marekani inasema ni eneo la taifa hilo kubwa ambalo linaamini kuwa linaongoza katika masuala ya teknolojia, ubunifu na uvumbuzi.

Rais wa Marekani, Donald Trump, alisema mara kwa mara sio haki kwa uchumi wa China kuendelea kukua kwa gharama ya biashara na ujuzi wa Marekani.

Marekani pia inailaumu China kwa kutokuzingatia haki katika biashara, kutokana na wizi wa hati fungani za raia wa Marekani na vitendo vya udukuzi wa teknolojia.

Ili kuishinikiza China, Marekani imeitoza nchi hiyo ushuru wa dola bilioni 250 kwa bidhaa zake zinazoingia Marekani. Kwa upande wake China inazitoza ushuru wa dola bilioni 110 bidhaa zinazotoka Marekani.

Waziri wa Fedha wa Marekani, Steven Mnuchin, alisema kutokana na ugumu wa masuala hayo, makubaliano ya kuumaliza mgogoro huo hayatazamiwi kufikiwa kwenye mkutano huo wa siku mbili wa mjini Washington, lakini anatarajia watapiga hatua kubwa. **DW**



Wajumbe wa Marekani na China wakiwa kwenye mazungumzo ya kutatua mgogoro wa kibiashara baina ya nchi hizo. **PICHA: ALLIANCE**

# Jukwaa launga mkono ushindi wa Felix Tshisekedi

**KISHANSA,** Congo

JUKWAA la kisiasa liitwalo Alternance pour la Republique AR, ambalo limekuwa karibu na mwanasiasa, Moise Katumbi, limetangaza kumtambua Rais Felix Tshisekedi kuwa rais wa nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Alter-nance pour la Republique limekuwa likimuunga mkono aliyekuwa mgombea urais kwenye uchaguzi mkuu uliofanyika Desemba mwaka jana, Martin Fayulu.

Taarifa iliyotolewa jana na Jean Bertrand Ewanga, ambaye alikuwa bega kwa bega na Martin Fayulu wakati wa kampeni za uchaguzi.

Muungano wa Alternance pour le changement AR bado ni miongoni mwa vyama vinavyounda vuguvugu la pamoja kwa ajili ya mabadiliko linaloogozwa na Moise Katumbi Chapwe.

Wajumbe wengine kutoka upande wa Martin Fayulu kama vile Delly Sessanga aliamua kujiunga na upande wa Felix Tshisekedi wakati wa kampeni.

Hata hivyo, mpasuko huo ndani ya muungano wa pamoja kwa ajili ya mabadiliko umeendelea kudhihirika, huku Moise Katumbi, akiwa bado hajazungumzia lolote hadi sasa.

Kwa upande wake Jean Pierre Bemba, ambae alimuunga mkono Martin Fayulu kwa asilimia 100 amekanusha taarifa kwamba amejiunga na kambi ya Felix Tshisekedi.

Kupitia mtandao wake wa kijamii wa Twitter, Bemba alisema ni habari za uongo wakati huu katibu wake mkuu, Eva Bazaiba, akithibitisha kuwa chama chake cha MLC kitashiriki katika mkutano wa hadhara wa Februari 2 unaotarajiwa kufanywa na Martin Fayulu. **RFI**

# Benki ya wakulima yakopesha bil. 224/-

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kipindi cha robo ya nne ya mwaka kilichoisha Desemba 31, 2018, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), imeeleza kuwa imetoa mikopo ya jumla ya Sh.bilioni 223.8 kwa wadau, ili kuinua na kuboresha kilimo nchini.

Taarifa ya benki hiyi jijini Dar es Salaam jana, ilisema inazidi kuimarika na imekuwa na uwezo wa kupanua na kuboresha huduma kwa wateja wake.

Ilisema katika miezi mitatu ya mwisho imetoa fedha zaidi ikilinganishwa na jumla ya Shilingi bilioni 17.1 iliyotoa katika robo ya mwaka huo iliyotangulia kipindi hiki. Idadi ya wafanyakazi, taarifa inasema, imekua kutoka wafanyakazi 44 mwishoni mwa Septemba 30, 2018 na kufikia 72 mwishoni mwa mwaka jana.

Taarifa hiyo imetiwa saini na Mwenyekiti wa Benki hiyo, Rosebud Violet Kurwijila na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Japhet Justine, Januari 30, 2019 na imetolewa kwa mujibu wa kanuni ya 7 na 8 ya kanuni za benki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) za mwaka 2014.

"Benki yetu imetoa mikopo kwa mikoa mitano mipya katika kipindi hiki.

Kadhalika, jumla ya Shilingi bilioni 1.64 zimetolewa kwa utaratibu wa dhamana kupitia mfuko wa dhamana na idadi ya wakulima wadogo waliodhaminiwa kupitia mfuko huu ni 814," inaeleza taarifa hiyo.

Taarifa hiyo inaonyesha kwamba wakulima 521,717 wamenufaika na mikopo iliyotolewa na benki hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, katika kipindi hicho wakulima 862 wamepewa mafunzo na miradi mipya saba ya kilimo imekopeshwa.

Katika robo ya mwisho ya 2018, TADB imepongezwa na wadau kwa kuwa karibu na wakulima pamoja na kuwatembelea kujionea na kusikiliza changamoto zinazowakabili na kuzitafutia ufumbuzi.



Mkurungezi Huduma za Kinga taasisi ya saratani ya Ocean Road hospitali, Dk. Crispin Kahesa, akizungumza kwenye semina ya saratani kwa waadishi wa habari, iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Gereza lalamikia vyombo vya haki

**Na Daniel Limbe,** CHATO

GEREZA la Wilaya ya Chato mkoani Geita, limevilalamikia vyombo vya utoaji haki kushindwa kutoa haki kwa wakati, hali inayosababisha mrundikano wa mahabusu katika gereza hilo.

Hali hiyo imekuwa ikiongeza mzigo kwa serikali kuwahudumia watu ambao hawafanyi kazi za uzalishaji mali kutokana na kesi zao kutomalizika.

Akitoa elimu kwa niaba ya Mkuu wa Gereza la Chato, Mkuu wa Kitengo cha Sheria wa gereza hilo, Sajent Reubern Andrew, kwenye maadhimisho ya ufunguzi wa wiki ya sheria wilayani humo, alisema ucheleweshaji wa kusikiliza kesi mahakamani kwa mahabusu ni changamoto kubwa ambayo inapaswa kutatuliwa na vyombo husika ili kupunguza manung'uniko katika jamii.

Mbali na hilo, alisema tatizo la kutotoa nakala za hukumu kwa wakati imekuwa ikisababisha baadhi ya wafungwa ambao hawajaridhika na vifungo vyao kukosa fursa ya kukata rufani kwenye mahakama za juu.

Kadhalika, kuchelewa kwa upelelezi wa kina na kwa wakati kwa mahabusu waliopo gerezani imekuwa ikisababisha msongamano mkubwa usio wa lazima gerezani na kutaka vyombo vinavyohusika kuchukua hatua za haraka ili haki kwa jamii ionekane inatendeka.

Kwa upande wake, Kaimu Hakimu Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Chato, Gabriel Kurwijila, amekiri uwapo wa mahabusu na washtakiwa ambao hufungwa jela kwa uonevu kutokana na kutotambua haki zao kisheria. Kutokana na hali hiyo, alisema ndiyo sababu serikali ikaruhusu uwapo wa mawakili kwa ajili ya kuwatetea wananchi wenye uhitaji wa sheria, huku akiwataka wananchi kujitokeza kwa wingi kwenye viwanja vya mahakama hiyo, ili wapate elimu kuhusu haki zao badala ya kulalamika.

"Ili haki itendeke katika jamii hatunabudi mahakama na wadau wengine kushirikiana kwa pamoja wakiwamo Ofisi ya Mwendesha Mashtaka, Polisi,Takukuru, Magereza, Mawakili na jamii ambayo hasa ndiyo watoa ushahidi mahakamani," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Chato, Mtemi Msafiri, alieleza kusikitishwa na kitendo cha mahabusu kujaa kwenye gereza hilo licha ya vyombo vyenye dhamana ya kufanya uchunguzi na kutoa haki vipo.

ITV

KIPIMA JOTO: SAA 3:05 USIKU

**Katika kipindi hiki kinachokujia mubashara kutoka studio fuatilia mada ya leo "Kuendelea kwa vitendo vya udanganyifu katika matokeao ya mtihani wa kidato cha nne. Je, wanafunzi wanaandaliwa ipasavyo?". Watazamaji mnakaribishwa kupiga simu na kuuliza maswali au kutoa ushauri kwa jopo letu. Mnakaribishwa kushiriki kwa kupiga kupiga simu namba 0767 444701 na kuuliza maswali.**

# Serengeti yazindua kampeni kuzuia ulevi

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Bia ya Serengeti (SBL), imezindua kampeni inayolenga kutoa elimu kwa umma juu ya unywaji wa kistaarabu, ikiwa moja ya hatua muhimu zinazochukuliwa na kampuni hiyo kuzuia ajali nyingi zinazosababishwa na madereva wanaoendesha wakiwa wametumia vilevi.

Kampeni hiyo inayobeba ujumbe wa 'usitumie kilevi na kuendesha chombo cha moto' ilizinduliwa jana jijini Mwanza na ilianza na kongamano lililojadili unywaji wa kistaarabu ambalo liliwaleta pamoja wadau kama vile Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, Mamlaka ya Usafirishaji wa Majini na Nchi Kavu (Sumatra), madereva, abiria na wadau wa sekta ya usafirishaji.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kampeni hiyo, Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Mwanza, Mkaddam Hamis Mkaddam, alisema kwa kulishirikisha Jeshi la Polisi, SBL imeiunga mkono serikali katika kuelimisha umma juu ya unywaji wa kistaarabu na kusisitiza umuhimu wa kutatua tatizo hilo.

Mkaddam alisema baadhi ya watu na hasa madereva hunywa kiasi kikubwa cha pombe bila kujali madhara yanayoweza kusababishwa na kitendo hicho na kuonya kuwa, vitendo vya aina hiyo vinaweza kusababisha ajali mbaya.

"Sote tunafahamu kuwa matumizi ya vileo yana uhusiano mkubwa na uendeshaji mbovu ambao unaweza husababisha ajali mbaya za barabarani zenye athari kubwa kwa jamii zetu. Athari zake si tu zinawagusa watumiaji wa vilevi bali hata maisha ya wengine na kusababisha upotevu wa maisha na ulemavu kwa watu ambao wangeweza kuchangia uchumi wa nchi," alisema Mkaddam.

Alisema pamoja na kusababisha vifo visivyotarajiwa na majeraha, unywaji usiokuwa wa kistaarabu una madhara makubwa kwenye sekta ya afya kwa kuwa kiasi kikubwa cha fedha kinatumika kwa ajili ya huduma, dawa na vifaa tiba kwa waathirika wa ajali za barabarani, hivyo kuwa mzigo kwa serikali.

"Ajali hizi pia ni mzigo kwa vyombo vyetu vya utekelezaji wa sheria kwa kuwa maofisa wanalazimika kuzishughulikia wakati zinaweza kuzuilika ambazo zinasababishwa na madereva wanaoendesha wakiwa wametumia vilevi," Mkaddam aliongeza.

Kuhusu kampeni hiyo itakavyosaidia jamii, Mkaddam alisema: "Sote kwa pamoja ikiwamo sisi polisi, madereva, jamii na wadau wengine tuna jukumu la kutafuta suluhisho la kumaliza tatizo la kutumia vilevi na kuendesha vyombo vya moto. Ninayo furaha kuona SBL pamoja na kwamba biashara yao ni kuuza vilevi, wameona wanawajibu wa kuhimiza unywaji wa kistaarabu."

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## HUDUMA MBALIMBALI

**MKOPO WA HARAKA NA NAFUU** Pata mkopo wa dharura ndani ya siku 2. Kwa wafanyakazi na Wafanyabiashara kutoka ENTERPRISE FINANCE LIMITED (EFL). Kwa mawasiliano Zaidi piga: 0768 928516 / 0653 258662. KARIBU EFL.

**KIBO FARM,** Tunauza vifaranga wa mayai,kuchi,pamoja na wanyama,wenye kuimili magonjwa . Pia tunauza mbwa wa walinzi kwa bei nafuu. Wasiliana nasi 0766607992.

**NDOA NZURI UNAITAKA?** Tunafundisha taratibu kwa wachumba, ndoa yoyote, kudumisha mapenzi, furaha, raha amani. Mwalimu Stanley 0717 178585

## ELIMU/MAFUNZO

**NAFASI ZA MASOMO:** Tanzania research and Career development institute.Reg pwf/041.Certificate na diploma za kilimo,mifugo, na maendeleo ya jamii.Mawasiliano:0767574701/0758753063.www.tracdi.ac.tz

## NAFASI ZA KAZI

**TUNAAJIRI WASICHANA WA MAUZO (SALES).** SIFA KIDATO CHA NNE. UMRI KUANZIA MIAKA 25 – 38 AWE MTANZANIA. MASLAHI MAZURI. PIGA SIMU NAMBA 0714 634046.

---

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**MWEBANGIRA P. KAMUHANDA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T. 189 BKD TOYOTA HARRIER.** Chassis namba **MCU150217083.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya polisi: MS/RB/0333/2019.**

115040902

---

JAMHURI A MUUNGANO WA TANZANIA
KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA
MAHALI DODOMA
MAOMBI Na 83 A 2018
BAINA YA
RENATUS BONIFACE
MALINGILA.............................................MUOMBAJI
DHIDI YA
DODOMA CITY COUNCIL
ANDERSON ISAYA
DAVID MANENO ......................WADAIWA
VERIDIANA R.MLIMBA
ANNA ALBIN MASSAWE

KWA:-ANDERSON ISAYA, DAVID MANENO, VERIDIANA R.MLIMBA NA ANNA ALBIN MASSAWE
POPOTE MLIPO

YAH: KUITWA SHAURINI

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya Maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.

Kwa hiyo unatakiwa /mnatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili Wewe binafsi,Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 04.03.2019 saa 3.00 asubuhi.Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.

ANGALIZO:-Kama hukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu,Baraza likithibitisha kuwa umepokea Hati ya Wito,Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 25 ya Mwezi wa Januari 2019.

MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya,
DODOMA.

115041402

---

### KADI YA GARI IMEPOTEA

**JULIETH DAVID LYIMO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA VITZ yenye namba ya usajili T152 CCR,Chasis no SCP103118883, Engine no.ISZ1818335C,

yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu nae.

**KJN/RB/621/2019**

115041502

---

SHERIA YA UANDIKISHAJI WA ARDHI (SURA 334)
KUPOTEA KWA BARUA YA TOLEO

BARUA YA TOLEO YENYE KUMBUKUMBU NA:
HMD/LA-15/53332

MMLIKI ALIYEANDIKISHWA: IRENE ANGELINA KADUSHI

ARDHI: KIWANJA NA.21 KITALU 'D' ENEO LA ITEGE

MUOMBAJI: IRENE ANGELINA KADUSHI

**TAARIFA IMETOLEWA,** kwamba Barua ya Toleo iiyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa hati Milki mpya badala hakuna kipingamizi kwa muda wa siku thelethini (30) tokeo tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika gazeti la Serikali.

**BARUA YA TOLEO NAKALA HALISI** ikionekana, irudishwe kwa

**Mkurugenzi,**
**Halmashauri ya Jiji,**
**P.O BOX 1249,**
**DODOMA**

**Imetolewa na;**

**Pirmin P. Mzenga**
**Afisa Mteule**
**Kny: Mkurugenzi wa Jiji**
**Dodoma**

115040302

---

### KUPOTELEWA KWA KADI YA GARI

**MR. JUMANNE SELEMANI MHANDI P.O.BOX 1992 SINGIDA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Toyota Dyana yenye namba za usajili T509 BAX. Chassis namba Bu66-0006898. Engine namba 14B-3660-CC.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya polisi: SI/TR/RB/8820/2018.**

115041102

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA MOROGRO.

MADAI NA.296 YA MWAKA 2018.

SOPHIA SAID TANDARA............................MWOMBAJI

DHIDI YA

(1) ADAM A.YATERA
(2) MONIKA JOHN MARIRE
(3) NEEMA MBINHE
(4) TANZANIA POSTAL BANK
(5) MARK RECOVERIES CO.LTD..........WAJIBU MAOMBI

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA**

(1) ADAM A.YATERA
(2) MONIKA JOHN MARIRE
(3) NEEMA MBINHE
(4) TANZANIA POSTAL BANK
(5) MARK RECOVERIES CO.LTD.............WAJIBU MAOMBI

Popote Mlipo mnaarifiwa mfike ktk baraza la ardhi na Nyumba la wilaya ya Morogoro tarehe 05 mwezi 02 mwaka 2019 wenyewe binafsi au mwakilishi wenu bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa. Endapo hamtaudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yenu na kutolewa uamuzi.

Imetolewa kwa mkono wangu leo tarehe 21 Mwezi Novemba, 2018.

115040202

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA

USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M.1984 NYONGEZA)
YA 5 KANUNI YA 2

Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO

Usimamizi wa mirathi No;12/2019

Ombi la MICHAEL MORIS BANZI Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu HONORATA MORIS MRUTU

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 01/02/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 30/01/2019.

215040102

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA

USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M.1984 NYONGEZA)
YA 5 KANUNI YA 2

Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO

Usimamizi wa mirathi No;19/2019

Ombi la PETER STANLEY NGOYE Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu JACKOB AMIN MZAVA

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 04/02/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 22/01/2019.

215040002

---

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**JOSHUA MUROWE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T. 244 AYU** NISSAN NAVARA. Chassis namba **VSKCVAD40200746331.** Engine namba **70000121.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **KMR/RB/1094/2019.**

---

### KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**WUZHOU INVESTMENT CO.LTD** Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba **MC. 763 BQA** aina **SANLG** MOTORCYCLE yenye chassis namba **LBRSP-JB50H9004151,**

Engine namba SL157FMI17903940.

Yeyote atakaeiona atoe taaarifa kituo cha polisi kilichopo karibu yake.

Taarifa ya polisi
KAH /TR /RB/072/019

---


*Uza,*

*Chenye Thamani Kubwa*

*Kwa Kutangaza Nasi*

*Kwa Bei Poa*

*Tupigie 0767 223311*

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*

*Tupigie 0767 223 311*


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# VAN PERSIE ASIFIA MOLARI FEYENOORD IKIIFUMUA AJAX




**ASMTERDAM,** Uholanzi

ROBIN van Persie amepaza sauti kusifia molari iliyoonyeshwa na Feyenoord wakati wakipigana kuibuka na ushindi wa 6-2 dhidi ya Ajax ambao ni wapinzani wao wakuu kwenye soka la Uholanzi, juzi Jumapili.

Akiwa amefanya kazi ya ziada ya kusaidia kupatikana kwa mabao mawili ya kwanza ya Feyenoord, Van Persie alifunga mara mbili, huku Tonny Vilhena na Yassin Ayoub kila mmoja akifunga moja.

Mara baada ya mchezo huo Van Persie, alisisitiza kwamba molari ya wachezaji wa Feyenoord ilikuwa juu zaidi na kuweza kufunga mabao hayo sita dhidi ya Ajax ikiwa ni mara ya kwanza tangu Novemba mwaka 1964.

"Ilihamasisha," alisema Van Persie, ambaye ameonekana kurudi kwenye kiwango chake hivi sasa.

"Mchezo huu ulikuwa na kila kitu. Magoli, soka zuri, hamasa, kupigana kwa nguvu. Najisikia fahari kwa namna tulivyopigana kupata matokeo haya.

"Kila mmoja uwanjani alipigania matokeo. Molari yetu ilikuwa juu zaidi.

"Wakati tulipokuwa mbele kwa 3-2, niliangalia nyuma na kuona kwamba kuna kitu kizuri zaidi kinakuja. Kwa uhakika tulicheza kwa umakini mzuri na kufanikisha kupata ushindi huu mtamu.

"Nawaamini wachezaji hawa. Wanaweza kucheza vizuri. Tulicheza kwa umakini na utulivu mkubwa zaidi."

Lasse Schone aliifungia Ajax bao la kuongoza dakika ya nane, lakini mabao ya Jens Toornstra na Steven Berghuis yakaiweka mbele Feyenoord katika kipindi cha kwanza.

# Familia ya Emiliano Sala yachangisha euro 300,000

**LONDON,** England

FAMILIA ya mchezaji aliyepotea na ndege, Emiliano Sala imefikisha kiasi cha euro 300,000 ilizochangisha kwa watu kwa ajili ya kutaka zoezi la kumtafuta mchezo huyo wa Cardiff City liendelee.

Polisi wa kisiwa cha Guernsey eneo iinapodaiwa kupotea ndege hiyo ndogo, Alhamisi iliyopita walisitisha zoezi la kumtafuta Sala, ambaye alipotea na akiwa na rubani David Ibbotson wakati wakitoka Nantes Ufaransa Jumatatu iliyopita.

Sala alikamilisha usajili wa kujiunga na Cardiff wikendi hiyo kabla ya kurudi Ufaransa kwa ajili ya kukamilisha mambo mengine pale Nantes na Jumatatu alikuwa akirejea kwenye timu yake mpya.

Zoezi la kumtafuta yeye na ndege hiyo lilidumu kwa siku tatu bila kupata chochote na hivyo wakaamua kusitisha.

Baada ya hapo familia ya Sala ikaamua kuanzisha ukurasa maalumu kwenye mtandao wa kijamii kwa ajili ya kuchangisha fedha za kuendeleza zoezi la kumtafuta mchezaji huyo.

Watu mbalimbali walitoa michango yao na kufikia euro 300,000 Jumapili, huku mchezaji wa Klabu ya Paris Saint-Germain akitoa kiasi cha euro 30,010 kwa ajili ya kufanikisha zoezi hilo.

Mbappe sio mchezaji pekee aliyejitolea kutoa kiasi hicho cha fedha, kwani mchezaji mwenzake wa PSG, Adrien Rabiot alichangia 25,000 Jumamosi na nyota wa Marseille, Dimitri Payet aliahidi kutoa euro 10,000.




# Ole Gunnar Solskjaer: Sanchez atatisha




**MANCHESTER,** England

KOCHA wa muda wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer anatarajia mambo makubwa zaidi kutoka kwa mshambuliaji wa klabu hiyo, Alexis Sánchez ambaye alianza kuwasha cheche dhidi ya Arsenal.

Gazeti la Daily Mail limemnukuu Solskjaer akisema kwamba, Sanchez ameonyesha uwezo mkubwa kuanzia mazoezini tangu alipopewa nafasi ya kuiongoza Man United, na kwamba anaamini mashabiki watafurahia yajayo kutoka kwa mchezaji huyo.

"Sawa, kwa Kiingereza changu kibovu na Kiingereza chake kibovu... unajaribu kukaa naye chini na kuzungumza, lakini ni mchezaji anayechapa kazi, wa kujivunia, na amejikita katika kuonyesha thamani yake," alisema Solskjaer.

"Naamini mashabiki watafurahia zaidi kinachokuja kutoka kwake, amekuwa vizuri tangu mazoezini. Na kiwango chake kimekuwa kizuri zaidi," aliongeza.

Sanchez ambaye alihamia Man United akitokea Arsenal Januari mwaka jana, alifanikiwa kufunga goli la kwanza dhidi ya klabu yake hiyo ya zamani, timu hizo zilipokutana kwenye Kombe la FA Ijumaa iliyopita, ambapo waliwazamisha washika bunduki hao wa London 3-1.

Sanchez alikuwa katika wakati mgumu wa kujitibu majeraha na saikolojia kiasi cha kwenda mapumzikoni nyumbani kwao nchini Chile kwa muda, enzi za kocha Jose Mourinho, lakini ameanza kugeuka lulu akiwa na Solskjaer.

Hilo lilikuwa goli lake la pili kwa Manc United tangu Machi mwaka jana.

## HABARI MICHEZO

# SARRI: KIPIGO CHA CHELSEA NILAUMIWE MIMI



**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Maurizio Sarri amesema anabeba lawama zote baada ya kikosi chake kukubali kipigo kizito kutoka kwa Bournemouth cha mabao 4-0 juzi Jumatano usiku.

Kipigo hicho ni kikubwa zaidi kwa Chelsea kwa kipindi cha miaka 23 kwenye Ligi Kuu ya England, ambacho Chelsea ilifungwa idadi kubwa zaidi ya mabao Septemba mwaka 1996 wakati walipopigwa 5-1 na Liverpool.

Sarri amesema wachezaji wake hawakucheza kama timu kipindi cha pili na walikuwa wazito kukubali kutanguliwa.

"Labda sina uwezo wa kuwafanya wawe na ari ya kujituma wachezaji hawa," amesema kocha huyo raia wa Italia wakati akizungumza na waandishi wa habari mara baada ya mchezo huo.

"Wakati tunaenda mapumziko ilikuwa ni vigumu kufikiria kuwa kipindi cha pili kingekuwa majanga na nitaka kujua kwa nini imekuwa hivyo, kama miezi miwili iliyopita tulikuwa tukicheza kama watu 11 tofauti na si timu moja.

"Nilifikiri hali hiyo ilibadilika tulipowafunga Tottenham wiki iliyopita, lakini bado. Kuna kitu lazima kibadilike."

Chelsea walianza msimu kwa kutofungwa katika michezo 12 lakini sasa wameshapoteza michezo minne kati ya 12 waliyocheza hivi karibuni.

Wakati huo huo, Liverpool imepoteza nafasi ya kutanua pengo kati yake na Manchester City kileleni mwa Ligi kwa alama saba baada ya kukubali sare ya 1-1 dhidi ya Leicester City. Sadio Mane aliwatanguliza Majogoo wa Jiji Liverpool katika dakika ya tatu ya mchezo lakini goli hilo lilisawazishwa na Harry Maguire mwishoni kabisa mwa kipindi cha kwanza.

Laiti Liverpool ingelipata ushindi, wangelifikisha alama 63 na kuwaacha mbali City wenye alama 56 baada ya kufungwa na Newcastle Jumanne usiku.

Sasa Liverpool wameongeza wigo wa uongozi kwa alama moja na kufikisha alama 61 na kufanya tofauti yao na City kuwa alama 5.

Kocha wa Liverpool Mjerumani Jurgen Klopp amelaumu theluji zilizodondoka uwanjani Anfield zimechangia timu yake kutokuwa na mchezo mzuri na kufanya wapate matokeo ya sare.

"Umeona mpira ulikuwa hauendi kwa kasi kabisa, na kama unamiliki mpira kwa asilimia 70 mpaka 80 basi mambo ndio yanakuwa magumu kabisa," alisema Klopp.

# Neymar sasa kukaa nje wiki 10

**PARIS,** Ufaransa

MIAMBA ya soka ya Ufaransa klabu ya Paris Saint-Germain, imethibitisha kuwa mshambuliaji wake raia wa Brazil, Neymar kutokana na kupata majeraha kwenye kifundo cha mguu ule ule ambao aliwahi kuumia na kumkosesha raha kwenye michuano ya kombe la Dunia mwaka jana nchini Urusi, atakaa nje ya uwanja kwa muda wa wiki 10.

Kuumia kwa nyota huyo kulizua hofu miongoni mwa wapenzi wa soka kuwa huwenda akaukosa mchezo wake wa Ligi ya mabingwa Ulaya dhidi ya Manchester United mwezi huu.

Lakini kwa taarifa hizi sasa atakosa michezo yote miwili dhidi ya miamba hiyo ya Uingereza ambayo michezo yake inatarajia kupigwa Februari 12 katika uwanja wa Old Trafford.

Mchezaji huyo ghali zaidi duniani aliumia kwenye mchezo wa kombe la Ufaransa dhidi ya timu ya Strasbourg ambapo waliibuka na ushindi wa mabao 2-0.



# Fellaini atimkia kucheza China



**MANCHESTER,** England

KIUNGO wa Manchester United, Marouane Fellaini ameridhia mkataba wa kibinafsi na Klabu ya Shandong Luneng kwa lengo la kuhamia katika timu hiyo ya nchini China.


United wamekataa kutoa tamko lolote ikiwa malipo yoyote yamefikiwa kumnunua mchezaji huyo raia wa Ubelgiji ambaye alitia saini nao mwaka 2018.

Fellaini mwenye umri wa miaka 31, alikuwa mchezaji mkubwa wa kwanza aliyesajiliwa baada ya enzi ya Sir Alex Ferguson, akijiunga na Manchester United kwa kiasi cha pauni milioni 27.5 mwaka 2013 akitokea Everton.

Mwisho wa dirisha la uhamisho wa wachezaji katika ligi ya China ni Februari 28.

Fellaini alitia saini mkataba mpya ya miaka miwili Old Trafford Juni mwaka jana, lakini hajawahi kukubalika na mashabiki wa United licha ya kukonga nyoyo za makocha, David Moyes, Louis van Gaal na Jose Mourinho.

## DOND SOKA
## MAGA LAYA




# PSG YATANGAZA KUMWANIA WILLIAN

## ●●● Lengo ni kubeba mikoba ya Neymar ambaye atakuwa nje kwa muda wa wiki 10…

**PARIS,** Ufaransa

PARIS Saint-Germain imewasilisha ofa ya kutaka kumsajili kiungo wa Chelsea, Willian ikiwa ni muda wa lala salama wa dirisha la usajili.

Mabingwa hao wa Ligi Kuu Ufaransa wamemtaja Mbrazili huyo ambaye klabu yake maarufu kwa jina la Blues limetaja thamani yake kuwa ni zaidi ya pauni milioni 40, kuwa ndiye mchezaji sahihi anayeweza kuziba pengo la Neymar anayetajwa atakuwa nje ya uwanja kwa muda wa wiki 10 kutokana na kupata majeraha.

PSG pia ilimtaja nyota wa Arsenal, Mezut Ozil kutua klabuni hapo kwa mkopo lakini inafahamu kuwa Mjerumani huyo amekacha ofa hiyo.

Neymar anatakiwa achague kama atakubali kufanyiwa operesheni, atakosa mechi mbalimbali za timu hiyo ikiwamo michezo miwili ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Manchester United.

**Michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya imetajwa kuwa ndio mashindano muhimu kwa sasa kwa PSG ambayo inajipanga kufanya vizuri.**

Kukosekana kwa Neymar katika klabu hiyo kutaathiri mipango yao lakini Wafaransa hao wanaamini kwamba Willian anaweza kuziba nafasi hiyo kikamilifu. Willian ambaye ana umri wa miaka 30 amebakisha miezi 18 katika mkataba wake na tayari ameonyesha kuvutiwa na ofa iliyowasilishwa na Barcelona, ambayo tayari imeshakataliwa huku pia klabu ya Dalian Yifang ya China ikijipanga zaidi kumnasa kiungo huyo.

Chelsea imekuwa ikijipanga pia kukiimarisha kikosi chake kilichoko chini ya Maurizio Sarri, wakati kikikataa ofa nyingine kutoka kwa Bayern Munich ambao wanataka kumsajili, Callum Hudson-Odoi kwa dau la pauni milioni 35.

Katika dirisha dogo lililotarajiwa kufungwa jana usiku, Chelsea inajipanga kuwauza wachezaji wake kadhaa wakiwamo, Michy Batshuayi, Danny Drinkwater na Gary Cahill.

Ofa ya Willian ina nafasi ndogo ya kukubaliwa na kama mchakato huo utafanyika, basi suala la mwongozo katika udhibiti wa fedha litahusika kwenye usajili huo.

## ZISIKUPITE

### RASHFORD ANUKIA MADRID

REAL Madrid inajiandaa kutoa pauni milioni 100 kwa ajili ya kumnasa straika wa Timu ya Taifa ya England, Marcus Rashford (21), kabla nyota huyo hajasaini mkataba mpya na klabu yake ya Manchester United katika kipindi cha majira ya joto. ***(Sun)***

### SARRI AMRUHUSU HAZARD

KOCHA wa Chelsea, Maurizio Sarri amesema kuwa kiungo mchezeshaji wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Eden Hazard (28), anaweza kuondoka katika klabu hiyo katika kipindi cha majira ya joto kama atahitaji kufanya hivyo. ***(Sky Sports)***

### PSG YAMTAKA OZIL

PARIS St-Germain imewasilisha ofa ya kumsajili kwa mkopo kiungo mchezeshaji wa Arsenal Mjerumani, Mesut Ozil ambaye ana umri wa miaka 30 katika dakika za lala salama. ***(Metro)***

### GIROUD AINGIA SOKONI

WEST Ham imewasilisha maombi ya kutaka kumsajili mshambuliaji wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Olivier Giroud, ambaye ana umri wa miaka 32. ***(Mail)***

### WEST WAMTAKA DRINKWATER

KIUNGO wa Chelsea, Danny Drinkwater (28) ametajwa kutakiwa kwa mkopo na klabu ya West Ham. ***(Talksport)***

### BATSHUAYI KUONDOKA CHELSEA

WEST Ham imeweka wazi nia yake ya kumsajili kwa mkopo straika wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Michy Batshuayi (25). ***(Sky Sports)***

### NANI KUTUA MAREKANI

WINGA wa zamani wa Manchester United Mreno, Nani (32), ambaye sasa anacheza katika klabu ya Sporting Lisbon, anajiandaa kujiunga na klabu moja inayoshiriki Ligi Kuu Marekani. ***(beIN Sport USA, via ESPN)***

### ROWE ANUKIA LEIPZIG

KIUNGO wa Arsenal, Emile Smith Rowe (18), anatarajia kusafiri kuelekea RB Leipzig kwa ajili ya kufanya vipimo vya afya kwa ajili ya kutua kwa mkopo kwenye timu hiyo mpaka mwisho wa msimu huu. ***(Sun)***

### VALENCIA YABANIWA

WEST Ham imekataa kupokea ofa ya pauni milioni saba kutoka Valencia kwa ajili ya kumuuza straika wake ambaye pia anaichezea Timu ya Taifa ya Mexico, Javier Hernandez (30). ***(Sky Sports)***

### JANSSEN AKARIBIA CARDIFF

CARDIFF imeweka wazi nia yake ya kumsajili mshambuliaji wa Tottenham na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Vincent Janssen (24), ambaye anahitaji kuwa kwenye kikosi cha kwanza katika mechi mbalimbali. ***(Sun)***

### UNITED KUMSAJILI JOAO

MANCHESTER United inatarajia kuacha mchakato wa kumsajili kiungo mchezeshaji wa Benfica Mreno, Joao Felix (19), baada ya kuvutiwa na kiwango chake wakati ilipoenda kumtazama na kushuhudia timu yake ikipata ushindi wa mabao 5-1 dhidi ya Boavista. ***(Talksport)***

## Makambo: Tuzo zinanipa mzuka kufanya vyema

**Na Faustine Feliciane**

MSHAMBULIAJI wa Yanga, Heritier Makambo amesema kuwa tuzo anazopata kutokana na uchezaji wake zinachangia kwa kiasi kikubwa kufanya vizuri kwenye timu hiyo.

Makambo hivi karibuni alitangazwa kuwa mchezaji bora wa ligi kuu wa mwezi Desemba pamoja na kocha wake kwenye timu hiyo Mwinyi Zahera.

Makambo ambaye jana aliiongoza Yanga kuwavaa Biashara ya Mara kwenye mchezo wa kombe la FA, alisema kuwa tuzo hiyo imempa mzuka wa kuenedelea kufanya vizuri na mashabiki wasishangae akiipata tena.

Alisema kuwa kupewa kunampa tamaa ya kujituma zaidi kuhakikisha anaisaidia timu yake kupata matokeo mazuri kwenye kila mchezo.

"Suala la tuzo ya mchezaji bora nimeweka pembeni, lakini inazidi kunipa hamasa ya kuendelea kujituma zaidi uwanjani kuhakikisha naendelea kufanya vizuri na kuisaidia timu yangu," alisema Makambo.

Alisema kuwa moja ya malengo yake ni kuhakikisha Yanga inafikia malengo yake ya kutwaa ubingwa wa ligi kuu msimu huu na kukata tiketi ya kushiriki ligi ya Mabingwa Afrika.

## Z'bar yajipanga kuongeza viwanja

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

UHABA wa viwanja ni moja ya changamoto zinazochangia kurudisha nyuma maendeleo ya michezo visiwani hapa ukiwamo soka, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Baraza la Michezo Zanzibar (BMTZ), Khamis Ali Mzee alisema uhaba wa miundombinu hiyo inapelekea kuwa na mwamko mdogo wa michezo tofauti na ilivyokuwa katika miaka ya nyuma.

Mzee alisema hivi sasa katika soka kuna timu nyingi ingilinganishwa na idadi ya viwanja vya michezo vilivyopo hapa kisiwani Zanzibar hali ambayo inapelekea baadhi ya timu kukosa viwanja vya kufanya mazoezi.

Alisema kuwa changamoto hiyo inafanya timu kushindwa kufanya mazoezi kwa wakati na kutekeleza programu za maendeleo zilizoandaliwa na benchi la ufundi.

'Ili michezo iweze kukuwa na kufanya vizuri lazima kuwapo na miundombinu ya kutosha, ikiwamo viwanja vya michezo hiyo kama vile soka, mpira wa mikono na michezo mingine ili kuzipa fursa timu kujiandaa vizuri katika ligi zao na hata mashindano makubwa yanapowakabili," alisema kiongozi huyo.

Aliongeza kuwa baraza hilo kwa kushirikiana na Serikali tayari wameshaandaa mipango mbalimbali itakayosaidia kufufua michezo yote iliyokuwapo Zanzibar pamoja na kuifanyia kazi changamoto ya viwanja iliyopo visiwani hapa.

# YANGA YAPIGA HESABU KALI IKIIFUATA COASTAL

**Na Somoe Ng'itu**

UONGOZI wa Yanga umesema kuwa unakwenda jijini Tanga kuwafuata Coastal Union huku wakiwa na tahadhari kutokana na ratiba "ngumu" waliyokuwa nayo ya mechi za Kombe la FA na za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Coastal Union inatarajia kuikaribisha Yanga katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayofanyika keshokutwa Jumapili kwenye Uwanja wa Mkwakwani jijini humo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mratibu wa Yanga, Hafidh Saleh alisema kuwa kikosi cha timu hiyo kinatarajia kusafiri leo kuelekea Tanga huku kikijipanga kukabiliana na ratiba hiyo waliyonayo.

**Saleh alisema kuwa wameandaa wachezaji wao kujituma na hatimaye kupata matokeo mazuri ambayo yatawafanya waweze kutimiza malengo waliyojiwekea katika msimu huu.**

"Leo (jana) tunacheza na Biashara United, halafu kesho (leo) Ijumaa tutaondoka kwenda Tanga, ratiba sio rafiki lakini tunaamini tutapambana bila kuchoka," alisema kiongozi huyo.

Alisema kuwa baada ya mechi hiyo ya Jumapili, kikosi chake kitaanza safari ya kuelekea Singida kuwafuata wenyeji wao, Singida United kwa ajili ya kukutana katika mchezo mwingine wa Ligi Kuu Bara.

"Katika mechi hizi zote za ugenini tutaendelea kuwakosa wachezaji wawili tu (Japhary Mohamed na Baruan Akilimali), wengine wote waliosalia watakuwapo katika msafara," Saleh aliongeza.

Yanga wenye pointi 53 ndio vinara wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 20 na inayotoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.




Mratibu wa Serengeti Safari Marathon, Henry Kimambo, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu mbio hizo, zitakazotangaza utalii wa Tanzania, zitakazofanyika Novemba 16 mwaka huu, ambapo washiriki wametakiwa kuanza kujisajili kwa njia ya mtandao kupitia www.serengetimarathon.or.tz. Kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) Devota Mdachi. **PICHA: JOHN BADI**

# *Watanzania wachangamkia Serengeti Marathon*

**Na Elizabeth Zaya**

WATANZANIA wameanza kuonyesha mwamko katika ushiriki mbio za Serengeti Marathon kutokana na kujitokeza kwa wingi kuliko raia wa nje.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mtendaji wa Serengeti Marathon, Henry Kimambo alisema katika msimu wa mwaka jana Watanzania wengi ndio waliojitokeza zaidi kuliko wageni tofauti na matarajio.

Alisema msimu wa Serengeti Marathon mwaka huu unatarajiwa kufanyika kitofauti kwa kufanyika katika hifadhi na kwamba kilele chake kitafanyika katika geti la hifadhi ya Serengeti mkoani Simiyu.

Alisema kwamba mwaka huu wanatarajia kuwa na washiriki zaidi 3,000 huku zaidi ya Sh.milioni 50 zikitengwa kwa ajili zawadi kwa washindi wake.

Kimambo alisema mwaka huu wanatarajia kuwa na makundi tofauti ya wakimbiaji, likiwamo kundi la viongozi linaloshirikisha wabunge, wakurugenzi na watu wengine wenye nafasi za aina hiyo.

Kundi jingine ni la wafanyakazi wa kati kutoka katika taasisi mbalimbali, na kundi la wakimbiaji wa mbio ndefu.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Utalii Tanzania(TTB), Devotha Mdachi aliwataka waandaji wa Marathoni kila mwaka kuboresha maandalizi yao kwa kuangalia vivutio mbalimbali vilivyomo ndani ya nchi.

"Wito wangu kwa waandaaji wa marathoni, nataka wawe wabunifu, wahakikishe kila mwaka wanakuwa na kitu tofauti cha kivutio na siyo kutumia kivutio kile kile kila mwaka kwa sababu lengo ni kukuza na kupanua utalii wa ndani kupitia michezo,"alisema Mdachi.

# Michezo

Ijumaa Fabruari 1, 2019

Nipashe




Solskjaer: Sanchez atatisha

HABARI UK. 28



Mshambuliaji wa Liverpool, Mohamed Salah (kulia), akichungwa na mabeki wa Leicester City wakati wa mchezo wao wa EPL juzi usiku, timu hizo zilifungana bao 1-1. **PICHA: MTANDAO**

## Zahera: Ratiba imebana lakini tutapambana

**Na Faustine Feliciane**

KOCHA wa Yanga, Mwinyi Zahera, amesema kuwa licha ya kuwa ratiba ya ligi kuu imewabana, bado watapambana mpaka jasho la mwisho kuhakikisha wanafanya vizuri kwenye michezo yao.

Zahera, alisema kuwa ukweli ni kwamba ratiba sio rafiki kwao lakini hakuna namna watapambana katika kila mchezo kuhakikisha wanafanya vizuri.

"Ratiba ni ngumu sana kwetu, leo (jana) tunacheza kombe la FA, baada ya hapo tunatakiwa kusafiri kwenda Tanga kucheza, lakini hatuna namna tutacheza na kupambana," alisema Zahera.



Alisema kuwa ingekuwa vyema kama wangemaliza michezo yao miwili mkoani Tanga kabla ya kuelekea Singida.

Aidha, Mratibu wa klabu hiyo, Hafidh Saleh, alisema kuwa ratiba inaonyesha baada ya mchezo wa leo (jana) dhidi ya Biashara, leo timu hiyo inaelekea Tanga kucheza mchezo wa ligi kuu dhidi ya Coastal Union.

"Tukitoka Tanga tunatakiwa kwenda Singida kucheza Jumatano dhidi ya Singida United baada ya hapo tunatakiwa kurejea tena Tanga kucheza na JKT," alisema Saleh.

Alisema hawana namna zaidi ya kukubaliana na ratiba hiyo na kocha wa timu hiyo amewaandaa wachezaji wake kukabiliana na changamoto hiyo ya ratiba.

Yanga inaongoza msimamo wa ligi ikiwa na pointi 53 walizovuna kwenye michezo 20 waliyocheza, vinara hao wamepoteza mchezo mmoja (dhidi ya Stand United) na kutoka sare michezo miwili na kushinda michezo 17.

# Mazoezi Simba yapamba moto

### ●●● Inaamini ushindi dhidi ya Waarabu hao wa Misri unawezekana endapo...

**Na Somoe Ng'itu**

INAWEZEKANA! Licha ya Simba kuonekana kutokuwa na nafasi ya kufanya vizuri katika mechi ya Kundi D ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa kesho dhidi ya Al Ahly, uongozi wa mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara umesema kuwa wanaweza kuwashangaza Waarabu hao wakiwa nyumbani kwao.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, alisema kuwa kikosi cha timu hiyo kinafahamu vema ubora wa wapinzani wao, hivyo wanajipanga kuwakabili kwa tahadhari.

**Rweyemamu alisema kuwa Simba imetua Misri ikiwa haina hofu yoyote na inaendelea na programu zake kuelekea mchezo huo utakaochezwa kwenye Uwanja wa Borg El Arab kuanzia saa 4:00 kwa saa za Tanzania.**

"Tunaendelea vema, programu yetu ya mazoezi ni mara moja tu, jana (juzi) tulifanya usiku na leo (jana) pia tutafanya mazoezi usiku kuanzia saa 1:30 ya huku, ila tumetafuta uwanja mwingine na si ule utakaotumika Jumamosi," alisema Rweyemamu.

Meneja huyo aliongeza kuwa wachezaji wote wako salama na hali ya baridi iliyoko nchini humo ni jambo ambalo walilitarajia kabla ya kuanza safari.

"Kuhusu baridi isiwatie hofu, tunafahamu hali hii, kwa sasa (jana mchana) wachezaji wamepumzika, hadi sasa wote ni wazima jambo ambalo tunaendelea kumshukuru Mungu," aliongeza meneja huyo.

Kikosi cha Simba kilitua salama Misri na kupokelewa na Balozi wa Tanzania nchini humo, Issa Suleiman Nassor ambaye aliwaambia wachezaji wa Simba wanatakiwa kujituma zaidi kwa sababu wanaiwakilisha Tanzania katika mchezo huo.

Simba ilianza vyema hatua hiyo ya makundi kwa kuwafunga JS Saoura ya Algeria mabao 3-0 lakini mechi yake ya pili ikiwa ugenini Kinshasa ikakumbana na kichapo cha magoli 5-0 kutoka kwa AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasia Kongo.

Al Ahly yenye pointi nne ndio wanaongoza katika kundi hilo wakiwa na pointi nne, wakifuatiwa na AS Vita yenye pointi tatu sawa na Simba huku JS Saoura yenye pointi moja ikiburuza mkia.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >